ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Piliwa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma naUtawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri waMiundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni

28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasiza Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais

51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 24 Julai, 2012

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika, (Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita Mhe. Waziri ili kuwasilisha hati, na leo kuna wageni wetu ambao wako pale ukumbi wa juu. Wageni wa leo ni wageni wa Waheshimiwa Mawaziri wetu ambao wamekuja kututembelea kama kawaida. Wageni hao ni kama ifuatavyo.

Kwanza kuna wageni wa Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Wageni hao wako katika makundi matano. Kwanza kuna Kamati ya Rais ya Kuchangia Fedha. Naomba wageni hao wanyanyuke. Inaonekana hawakuja.

Pili, kuna wawakilishi kutoka mashirika mbali mbali ya kimataifa wakiwemo ILO, UNDP na IFAD.

Could excellences present here standup to salute the members. The representatives from ILO, UNDP and IFAD. They are not present yet. And the representatives of the Save the Children. And they are present here? No.

Kundi la tatu lilikuwa ni wawakilishi kutoka Vyama vya Wafanyakazi, kama wapo nawaomba wasimame. Inaonekana hawapo.

Vile vile kuna Vikundi vya Ushirika, Wajasiriamali na SACCOS mbali mbali, kama wapo nawaomba wasimame. Kuna mmoja yule pale juu. Wageni wengine ni kutoka Jimbo la Makunduchi, kama wapo nawaomba wasimame. Ndio wapo, wale pale juu. Nawashukuru sana. Tukae. Kama wasingekuwepo hawa, basi ningesema kwamba Mhe. Haroun kama kawaida yake amenifanyia mzaha na kwa bahati mbaya wala sio mwezi wa Aprili mosi leo.

Wageni wengine ambao wapo katika ukumbi wa juu ni wageni wa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ambao ni wanamichezo wa UMISETA, jumla yao ni 17. Kama wapo nawaomba wasimame. Wapo, karibuni sana na wamekuja katika sura halisi ya wanamichezo, tena wana na kombe lao lile pale wamelishika. Wenzetu hawa wamefanya vizuri katika mashindano ya UMISETA ya mwaka huu, wamepata nafasi ya kwanza katika mpira wa miguu, *table tennis* wanaume wamepata nafasi ya pili, *basket ball* wanawake wamepata nafasi ya tatu, *hand ball* wanaume wamepata nafasi ya tatu na riadha wamepata medali saba, dhahabu, fedha mbili na shaba moja.

Hayo ndio matokeo ya vijana wetu wanamichezo hawa wa UMISETA jinsi walivyofanya vizuri. Kwa hivyo, nawakaribisha sana wageni wote karibuni sana na nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe.

Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha mezani, naomba nimtakie kheri Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika Mhe. Maalim Haroun Ali Suleiman, kwa kutimiza miaka 59 leo. *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha mezani, kuhusu tukio la kuzama kwa meli ya Mv. Skagit, iliyotokea tarehe 18/07/2012 katika eneo la Bahari ya Chumbe. Naomba kuwasilisha Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Makamo Mwenyekiti: (Kny: Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwasilishe maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuhusu tukio la kuzama kwa meli ya Mv. Skagit, iliyotokea tarehe 18/07/2012 katika eneo la Bahari ya Chumbe. Naomba kuwasilisha, ahsante Mhe. Spika. *(Makofi).*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 1

Upotevu wa Pesa Shirika la Bima la Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako kabla ya kujibiwa swali langu, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani, nataka nimpongeze sana Mhe. Hamad Masoud Hamad, kwa uamuzi wake wa ujasiri wa kuamua kujiuzulu. Hatua hii imejenga hadhi yake na imejenga hadhi ya GNU na imejenga hadhi ya Wazanzibari. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba swali langu nambari moja lijibiwe.

Katika hatua isiyoridhisha, kumekuwepo na taarifa kwamba, Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) Tawi la Dar es Salaam limepata hasara kubwa baada ya upotevu wa mamilioni ya fedha yaliyosababishwa na baadhi ya Watendaji wake.

(a) Kwa kiasi gani taarifa hii ina ukweli na kiwango gani cha fedha kinachodaiwa kupotea.

(b) Je, ni kweli kwamba Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa upotevu wa fedha hizo.

(c) Je, kutokana na hali hiyo, ni kweli kuwa Uongozi wa Shirika umefanya uhamisho wa kawaida kwa baadhi ya wafanyakazi wake kutoka Dar es Salaam na kuwapeleka matawi mengine likiwemo Tawi la Shirika Dodoma.

(d) Je, kuna ukweli wowote wa taarifa kuwa, mfanyakazi mmoja wa Shirika hilo aliyepewa uhamisho kutoka Dar es Salaam kupelekwa Dodoma, ameamua kulishitaki Shirika na kudai fidia ya zaidi ya millioni 30 baada ya Shirika kumcheleweshea fedha zake za huduma baada ya uhamisho huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, baada ya ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija, kumpongeza sana Mhe. Hamad Masoud Hamad na mimi naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais kwa kumteua Mhe. Rashid Seif Suleiman, kuwa ni mrithi wa Mhe. Hamad Masoud Hamad, tupo tutamsaidia na tutafanya kazi na yeye kwa karibu zaidi kama tulivyokuwa tunafanya kazi kwa karibu na Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mjumbe swali lake nambari 1 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Biashara ya Bima ni kama zilivyo biashara nyengine ina faida na hasara, na ina matatizo yake katika kuiendesha. Hali hii ndio iliyopelekea Shirika la Bima la Zanzibar, katika mwaka 2010 kupoteza jumla ya shilingi milioni 9, 000,000.00 kwa kumlipa mteja ambaye siye aliyestahiki kulipwa. Kwa maana hiyo, taarifa ya kuwepo kwa upotevu kama ilivyoelezwa na Mhe. Mwakilishi ni ya kweli.

(b) Mhe. Spika, baada ya kuripotiwa upotevu huo, Jeshi la Polisi lilianza kuchunguza na bado limo katika hatua za uchunguzi juu ya upotevu wa fedha hizo. Hivyo ni kweli Jeshi la Polisi bado lipo katika uchunguzi.

(c) Mhe. Spika, ni kweli mnamo Novemba, mwaka 2011, Uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar ulifanya uhamisho kwa baadhi ya wafanyakazi wake, kutoka Ofisi ya Dar-es-Salaam na kuwahamishia matawi mengine ya Tanzania Bara, ikiwemo hilo la Dodoma. Uhamisho huo ni wa kawaida.

(d) Mhe. Spika, ni kweli mfanyakazi mmoja aliyepewa uhamisho kutoka Dar-es-Salaam kwenda Dodoma alifikiria kutaka kulishitaki Shirika la Bima la Zanzibar na kudai fidia ya shilingi 30,000,000 milioni, baada ya kucheleweshewa malipo yake ya kodi ya nyumba gharama nyengine za uhamisho.

Hata hivyo, kwa lengo la kuondosha mvutano na mfanyakazi huyu, uongozi kwa kushirikiana na Bodi ya Shirika, ulikaa na mfanyakazi huyo kwa mazungumzo. Baada ya mazungumzo mfanyakazi huyo alikubali kuondosha dhamira yake ya kulishitaki shirika, na hatimaye kulipwa stahiki zake zote. Kwa sasa anaendelea kulitumikia shirika kwa kushirikiana na watendaji wengine.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba anielimishe kidogo sana kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa kuwa hili Shirika la Bima ni shirika ambalo linaendelea kujitanua kibiashara, Tanzania kwa maana Zanzibar na Tanzania Bara. Kwa kuwa dosari iliyoingia, Mhe. Waziri amekiri kwamba imepoteza shilingi milioni 9.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri ni mtu makini na ni mtu ambaye yuko mstari wa mbele kusimamia Shirika la Bima. Je, amejifunza nini kutokana na wizi huu ambao umetia dosari kidogo katika Shirika letu la Bima, shirika ambalo ndio mategemeo ya Wazanzibari.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nimejifunza kuwepo kwa umakini, lazima shirika liwe makini, kutokuwa makini kunaweza kupoteza fedha nyingi sana za shirika.

La Pili nililojifunza ni kwamba licha ya kwamba tuna siku 45 tulizopewa na mamlaka inayosimamia Bima, kwamba baada ya vielelezo kukamilika mteja anatakiwa kulipwa haki yake, lakini shirika ni lazima lithibitishe kwa ukamilifu kwamba wanayemlipa ndiye, wamemuona na vielelezo vyote vinavyohitajika wameviona.

Nam. 55

Mamlaka ya ZRB

Mhe. Hija Hassan Hija: (Kny: Mhe. Ismail Jussa Ladhu) – Aliuliza:-

Wakati wa ufunguzi wa jengo jipya la makao makuu ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Kamishna wa Bodi hiyo alieleza kuwa Wazanzibari wanadhulumika katika ulipaji wa kodi kutokana na kuwepo kwa mamlaka mbili za kodi hapa Zanzibar ambayo ni ZRB na TRA.

Kwa kuwa ZRB imeonesha mafanikio makubwa katika ukusanyaji kodi Zanzibar, kwa nini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar isichukue hatua za kuipa ZRB mamlaka yote na pekee ya ukusanyaji wa kodi kwa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 55 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suala la *TRA* kukabidhi shughuli za ukusanyaji wa mapato ya Muungano kwa *ZRB* ni la kikatiba na kisheria. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, mnamo mwaka 2010/2011 ilifanya utafiti wa kuangalia faida, hasara na athari za kukasimu madaraka ya kusimamia baadhi ya kodi za Mamlaka ya Mapato Tanzania, na hasa kodi ya mapato kwa bodi ya mapato ya Zanzibar. Utafiti huo uliofanywa na wataalamu kutoka Kampuni ya *Unstand Young* na ripoti yake kukabidhiwa TRA, robo ya pili ya mwaka 2011 kwa mazingatio.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa utekelezaji wa masuala yaliyojitokeza ndani ya ripoti hiyo, Kamati ya pamoja ya *TRA* na *ZRB* iliundwa ili kuyafanyia kazi masuala muhimu yaliyojitokeza, yakiwemo yale ya sheria, pamoja na watumishi na stahiki zao. Ushauri wa kamati hiyo bado haujawasilishwa serikalini kwa mazingatio. Mara ushauri utakapowasilishwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaufanyia kazi na hatimaye kuutolea maamuzi. Namuomba Mhe. Mwakilishi avute subira.

Nam. 185

Uingizaji wa Bidhaa Zisizo na Viwango

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: (Kny: Mhe. Mohammed Said Mohammed) – Aliuliza:-

Kumekuwa na hali ya uingizaji wa bidhaa nchini zisizo na viwango na baadhi ya bidhaa hizo huwadhuru watumiaji.

Je, ni hatua gani zitachukuliwa dhidi ya tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika. Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 185, linalohusiana na hatua zinazochukuliwa dhidi ya uingizwaji wa bidhaa nchini zisizo na viwango kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kukabiliana na uingizaji wa bidhaa zisizo na viwango imechukua hatua zifuatazo. Mhe. Spika, kwa upande wa uingizwaji wa bidhaa hizo, wizara kwa kupitia kitengo cha kumlinda mtumiaji kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kupitia boda yake ya chakula, dawa na vipodozi, huwa zinafanya uchunguzi wa bidhaa hizo zinapofika bandarini kabla ya kuingia nchini kama bidhaa hizo zinafaa kwa matumizi ya binadamu. Bidhaa hizo huchukuliwa sehemu kwa ajili ya uchunguzi katika maabara ya Mkemia Mkuu kabla ya kuruhusiwa kuingia katika soko la Zanzibar.

Mhe. Spika, aidha kwa upande wa bidhaa nyengine wizara imeandaa sheria za viwango ya mwaka 2011, ambayo imeshapitiwa na Baraza lako hili tukufu kwa lengo la kujenga uwezo wa kisheria kupambana na tatizo la uingizwaji wa bidhaa hizo. Sheria ambayo inaanzisha taasisi ya usimamiaji wa viwango kwa bidhaa zinazoingia Zanzibar, zinazozalishwa na zinazosafirishwa nje ya Zanzibar.

Mhe. Spika, wizara tayari imeshapatiwa majengo maalum katika eneo lililokuwa Kiwanda cha Sigara, ili kuweza kuanzia na taasisi hiyo. Aidha, serikali inaendelea na taratibu za uteuzi wa mtendaji mkuu ili hatimaye basi tuweze kuajiri wataalamu wengine wa taasisi na kununua vifaa na samani kwa ajili ya taasisi ya viwango ya Zanzibar, pamoja na kuyafanyia ukarabati majengo ambayo yamekusudiwa kuwapo kwa taasisi hiyo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, nashukuru kwamba amesema kuwa

vyakula vingi vinavyoletwa hapa vinakaguliwa kisheria na bodi maalum. Swali langu liko hapa, hivi sasa wameibuka vijana wengi katika sehemu ya mjini wanaouza vitu vya mikononi.

Kwa mfano, dawa ya meno, tungule za vibati, mafuta ya kula na kadhalika na bidhaa zile nyingi zinategemewa kwamba hazina viwango. Je, kama hawa mtawachunguza kwa njia zipi ili muweze kuchukua hatua zinazofaa, ili wananchi wasipate madhara kwenye vyakula hivi.

Mhe. Naibu Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika. Napenda nikubaliane na Mhe. Mjumbe kwamba kweli wapo vijana ambao huzunguka na bidhaa za mikononi, na wizara imelifuatilia hilo na kugundua kwamba bidhaa hizo Mhe. Spika, huwa wafanyabiashara wanawapa vijana hao, pale ambapo wanagundua bidhaa hizo zinakaribia kumaliza muda wake wa matumizi.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na Wawakilishi wote katika Baraza lako tukufu, tushirikiane katika kulifuatilia suala hili ili kuongezea nguvu jitihada za wizara, lakini wizara inajitahidi kila inapogundua kwamba suala hili sasa linafanyika kwa kasi, basi wafanyakazi ndani ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, ambao wako katika kitengo hiki cha kumlinda mtumiaji huwa wanalifuatilia na wanapokamatwa huwa wanawajibishwa kisheria.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ni aina gani za bidhaa ambazo zimebainika zimemaliza muda wake pamoja na idadi na thamani yake kwa kiasi gani katika mwaka uliopita.

Mhe. Naibu Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita, bidhaa ambazo zimekamatwa na ambazo zimekwishapita muda wake wa matumizi, zilikuwa na thamani ya milioni 15.7 na bidhaa ambazo zimekamatwa Mhe. Spika, ni sembe, mchele, maharagwe na tende.

Mhe. Spika, tende zilikuwa ni tani 5, mchele tani 1.5, maharagwe tani 3.5, na sembe tani 2. Mhe. Spika, pamoja na vitu vyengine vidogo vidogo.

KAULI ZA SERIKALI

KAULI YA SERIKALI KUHUSU TUKIO LA KUZAMA KWA MELI YA MV. SKAGIT ILIYOTOKEA TAREHE 18.07.2012 KATIKA ENEO LA BAHARI YA CHUMBE

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutufikisha tena siku ya leo na kuendelea kutuwezesha na Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Aidha, nitoe mkono wa Ramadhan njema kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wote wa Zanzibar. Aidha, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Waziri mteule Mhe. Rashid Seif Suleiman wa Jimbo la Ziwani Pemba, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Vile vile nimpongeze sana Mhe. Hamad Masoud Hamad, kwa ujasiri wake na uzalendo wake aliouonesha wa kupenda nchi yake. Aidha, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuniwezesha tena kushiriki katika kikao hiki cha Baraza lako tukufu la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nichukue nafasi hii adhimu kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kutupatia fursa hii adhimu ili kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu taarifa ya maafa ya kuzama kwa meli ya MV. Skagit iliyotokea katika bahari ya Chumbe tarehe 18.07.2012.

Utangulizi

Mhe. Spika, Meli ya MV. Skagit ilitengenezwa nchini Marekani mwaka 1989 na imesajiliwa Zanzibar tarehe 25/10/2011, na kupewa nambari ya usajili 100144. Meli hiyo ina uzito wa GRT96 ambayo inamilikiwa na *Kampuni ya Seagull Sea Transport Limited* ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mnamo tarehe 18.07.2012 majira ya saa saba na nusu za mchana ilipatikana taarifa ya ajali ya kuzama kwa meli ya MV. Skagit katika bahari ya Chumbe nje kidogo ya mji wa Zanzibar. Meli hiyo ilikuwa katika safari zake za kawaida ya kutoka Dar-es-Salaam kuja Zanzibar.

Kwa mujibu wa *manifest* ya abiria iliyowasilishwa na wamiliki wa meli kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania (*Tanzania Ports Authority-TPA*), na Mamlaka ya Usafiri wa Baharini na Nchi Kavu Tanzania (*Surface and Marine Transport Authority-SUMATRA*), meli hiyo ilikuwa imechukua jumla ya watu 290 wakiwemo abiria watu wazima 250, watoto 31 na mabaharia 9.

Mhe. Spika, taarifa hii inaelezea kwa kina juu ya hali halisi ya tukio, pamoja na hatua zote zilizochukuliwa kuanzia tarehe 18/07/2012 hadi hivi sasa.

Mhe. Spika, mara baada ya tukio hili, Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Taifa ilikutana kwa ajili ya kuweka mikakati ya hatua za kuchukua, pamoja na kuandaa taarifa rasmi ya Serikali kwa wananchi kupitia vyombo vya habari. Aidha, Baraza la Mapinduzi lilikaa usiku wa tarehe 18.07.2012, na kutoa maagizo juu ya hatua za kuchukua ikiwemo kuwepo kwa matayarisho katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ya kupokea majeruhi, kutayarisha eneo la Maisara kwa ajili ya mapokezi na utambuzi wa maiti; kutayarisha eneo la kuzika miili ya marehemu huko Kama, kuweka takwimu sahihi za majeruhi na waliofariki katika ajali hiyo, pamoja na kutolewa kwa taarifa rasmi ya hali ya uokozi iliyokuwa inaendelea.

HATUA ZILIZOCHUKULIWA

Mhe. Spika, kufuatia maagizo hayo ya Serikali, hatua zifuatazo zilichukuliwa: -

- Vituo cha mapokezi ya wahanga wa ajali hiyo vilifunguliwa katika maeneo ya Bandari ya Malindi, Hospitali ya Mnazi Mmoja na uwanja wa Maisara.
- Vikosi vya Ulinzi na Usalama vilipelekwa katika maeneo mbalimbali ili kuimarisha huduma za ulinzi na uokozi wa haraka.

- Kazi ya uchimbaji wa makaburi katika eneo la Kama ilifanyika kwa mashirikiano makubwa ya viongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Vikosi vya Ulinzi na Usalama pamoja na wananchi. Jumla ya makaburi 80 yalichimbwa.
- Sala na dua maalum ya kuwaombea marehemu wote ilifanyika baada ya sala ya Adhuhuri jana tarehe 22.07.2012 katika misikiti yote ya Unguja na Pemba na Kitaifa ilifanyika katika Msikiti wa Mwembeshauri mjini Zanzibar.
- Kuorodhesha majina ya wale wote ambao wanasadikiwa walikuwemo ndani ya chombo kilichopata ajali na hadi sasa hawajulikani walipo. Taarifa hizi zinakusanywa kupitia ngazi ya Shehia na Wilaya kwa Unguja na Pemba na kwa Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa Tanzania Bara.
- Kutoa huduma ya kuwasafirisha majeruhi baada ya kupata matibabu kurudi makwao.
- Kutoa huduma za usafiri kwa walioshiriki katika shughuli zote za operesheni.

MATOKEO YA OPERESHENI

Shughuli za uokozi

Mhe. Spika, kutokana na operesheni iliyofanywa na vikosi vya ulinzi na usalama kwa mashirikiano makubwa ya wananchi yamepelekea hadi kufika jana tarehe 22.07.2012 kuwa na idadi ya watu waliookolewa wakiwa hai kufikia 146 na miili ya waliofariki dunia iliyopatikana kufikia 78. Lakini kwa taarifa za hivi asubuhi Mhe. Spika, ambazo zinaendelea kufanyiwa uchunguzi zaidi, kuna watu 5 inasemekana tayari wamepatikana wakiwa maiti. Kati ya maiti hizo 68 zilipokelewa kituo cha Maisara na maiti 10 zilipelekwa moja kwa moja katika makaburi ya Kama kwa vile maiti hizo zilikuwa zimeshaharibika.

Kwa waliookolewa wakiwa hai waliweza kufikishwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa uchunguzi na matibabu. Hadi hii leo, majeruhi wote walishatibiwa na kuruhusiwa kurudi majumbani mwao.

Mhe. Spika, katika kituo cha Maisara maiti zilipangwa ili kuwawezesha ndugu na jamaa kutambua maiti zao. Na kwa kurahisisha kazi hiyo, Shirika la Utangazaji kupitia kituo chake cha televisheni, kilichukua picha za sura za marehemu na kuzionesha zikiwa tayari zimewekewa nambari ili kurahisisha utambuzi na uchukuaji wa maiti hizo. Kupitia utaratibu huu, jumla ya maiti 50 zilitambuliwa na kukabidhiwa kwa jamaa na ndugu zao kwa ajili ya mazishi. Idadi ya maiti ambao hawakutambuliwa ni 28 na mazishi yao yalisimamiwa na serikali katika eneo la Kama.

Aidha, maiti mmoja aliyetambuliwa alilazimika kuzikwa Kama, kwa vile mwili wake ulikuwa umeharibika sana. Kila maiti alizikwa katika kaburi lake, chini ya usimamizi wa Mashekhe kutoka Ofisi ya Mufti na Wakfu na Mali ya Amana. Aidha, katika kituo cha Maisara huduma za uoshaji na sala ya maiti zilitolewa, na pia wale wote waliochukua maiti wao walipatiwa usafiri, sanda na ubao kwa ajili ya kuzikia.

Mhe. Spika, kwa wale wenye madhehebu mengine, dua zilifanywa kwa mujibu wa madhehebu yao.

Juhudi za Kuitafuta Meli na Watu Waliokuwa Hawajaonekana

Mhe. Spika, katika jitihada za serikali za kuhakikisha miili zaidi ya marehemu iliyotokana na ajali ya meli inapatikana, serikali ilivitaka vikosi vyake vya ulinzi na usalama vikiongozwa na KMKM kuendesha zoezi la kuitafuta meli na miili iliyosalia. Kazi ya kuendesha operesheni ya kuitafuta meli pamoja na abiria ilianza mara tu baada ya kusikia kutokea kwa ajali hiyo. Jumla ya watu walio hai 146 waliokolewa siku hiyo, na maiti 31 zilipatikana.

Asubuhi ya tarehe 19.07.2012, wazamiaji kutoka KMKM, Jeshi la Wananchi wa Tanzania na kampuni binafsi, walifika katika eneo la tukio kwa ajili ya kuendelea na kazi hiyo. Wazamiaji hao walifanikiwa kupata maiti nyengine 37 na hawakupata abiria aliye hai. Hata hivyo, wazamiaji hao hawakuweza kuiona meli hiyo.

Mhe. Spika, vikosi hivyo viliendelea na jitihada za kuitafuta meli na watu waliokuwa hawajaonekana kwa kujigawa katika makundi matatu. Makundi mawili yalihusika na kazi ya utafutaji wa watu katika maeneo ya ukanda wa eneo la tukio. Kundi jengine lilijihusisha na kazi ya uzamiaji (*diving*) kwa ajili ya kuitafuta meli chini ya bahari.

Kukusanya Taarifa za Watu Waliokuwa Hawajaonekana Kupitia Ofisi za Masheha na Wilaya

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliziagiza ofisi zote za Wilaya na Shehia kuorodhesha majina ya watu waliokuwa hawajaonekana na waliofariki na kuziwasilisha orodha hizo kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili kufanyiwa uhakiki na kupata orodha sahihi kwa ajili ya matumizi na kumbukumbu za baadae. Hadi kufikia tarehe 22.07.2012 zaidi ya watu 100 wameripotiwa hawakuonekana ama wakiwa hai au maiti. Hata hivyo, kwa uhakiki wa awali imebainika kwamba baadhi ya watu wameorodheshwa zaidi ya mara moja katika maeneo tofauti.

Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kutoa Mkono wa Pole

Mhe. Spika, Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na viongozi wengine wanatarajiwa kufanya ziara za kutoa pole na kuzifariji familia zilizofiliwa na zilizopotelewa na ndugu zao kwa maeneo yote yaliyoathirika Unguja na Pemba. Kazi hiyo inatarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Kuratibu Upokeaji wa Misaada

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa, iliendelea kupokea misaada ya kifedha na vifaa kutoka kwa watu binafsi, Mashirika ya Kimataifa, Mashirika ya Umma, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

Hadi kufikia tarehe 22.07.2012 jumla ya Shilingi 320,000,000/- milioni zimepokelewa na kuingizwa katika akaunti ya Mfuko wa Maafa Zanzibar (*Zanzibar Disaster Funds*) ilioko Benki ya Watu wa Zanzibar, ambayo imefunguliwa maalum kwa ajili ya michango ya aina hiyo. Aidha, vifaa na bidhaa mbali mbali zimepokelewa kwa ajili ya kusaidia shughuli za operesheni ya uokozi.

GHARAMA ZA OPERESHENI

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliipatia Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa jumla ya shilingi milioni ishirini (20,000,000/-) kwa ajili ya kugharamia shughuli za operesheni ambapo hadi kufikia tarehe 22.07.2012 fedha zote zilikwisha tumika.

TULICHOJIFUNZA KUTOKANA NA TUKIO HILI (*LESSONS LEARNED*)

Mhe. Spika, kutokana na tukio hili la kuzama kwa meli ya MV. Skagit tumeweza kujifunza mambo mbalimbali ambayo ni changamoto kwetu katika kuimarisha kazi na huduma za kukabiliana na maafa nchini. Miongoni mwa mambo hayo ni haya yafuatayo:-

- Umakini na maamuzi sahihi na ya haraka yaliyochukuliwa na viongozi wetu yameweza kuleta ufanisi mkubwa katika operesheni ya uokozi, na hivyo kupelekea kuokoa maisha ya wananchi wetu wengi.
- Muitikio wa haraka wa taasisi mbalimbali za kukabiliana na maafa, zikiwemo taasisi za Serikali, vyombo vya ulinzi na usalama, Sekta Binafsi na Jumuia za Kiraia umepelekea watu wengi kuweza kuokolewa wakiwa hai pamoja na kupatikana kwa maiti, hali ambayo imewezesha maiti wengi kuzikwa na familia zao.
- Kutokana na wananchi wengi kutumia mtandao wa mawasiliano wa Zantel, kulisababisha ugumu wa mawasiliano kutokana na minara ya kampuni hiyo kuzidiwa na matumizi.
- Udogo wa sehemu ya kuhifadhia maiti (***Mortuary***) ulipelekea maiti wasiotambuliwa na jamaa zao kuzikwa haraka na serikali, uhaba wa vifaa vya vifaa vya kisasa vya uokozi pamoja na wataalamu wa uzamiaji umepelekea zoezi la uokozi kuwa gumu na kuchukua muda. Kukosekana kwa taarifa za uwezo wetu wa ndani wa kukabiliana na maafa ikiwemo uwezo wa vifaa na wataalamu ni changamoto ambayo inapaswa kufanyiwa kazi.

Shukrani:

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena kwa niaba ya Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa, naomba nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa juhudi zake kubwa alizochukua, ili kuhakikisha maisha ya wananchi wanaokolewa. Tunamshukuru kwa maelekezo yake na miongozo aliyotupatia, ambayo kwa kiasi kikubwa ilitusaidia kufanikisha kazi za uokozi.

Vile vile tunamshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yao na msaada mkubwa walioutoa katika kukabiliana na maafa hayo.

Aidha tunamshukuru sana Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa msaada mkubwa aliotupatia kupitia ofisi yake.

Mhe. Spika, tunawashukuru pia Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, na Makamo wa Pili wa Rais ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na

Maafa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kutupatia miongozo ya mara kwa mara katika jitihada za kuokoa maisha ya wananchi na kupunguza athari za maafa yaliyotokea.

Pia tunatoa shukurani za dhati kwa Baraza la Mapinduzi na Baraza la Usalama la Taifa kwa maelekezo yao juu ya hatua za kuchukuliwa katika kukabiliana na janga hili na majanga yanayoweza kutokea baadae.

Shukurani za dhati pia zinatolewa kwa vyombo vya ulinzi na usalama, kwa hatua zao za haraka zilizosaidia kuokoa maisha ya wananchi wengi.

Mhe. Spika, tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa karibu nasi, na kwa michango yao ya hali na mali katika kukabiliana na tukio hili la kusikitisha.

Aidha shukurani maalum ziende kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa miongozo yao na ushiriki wao katika kukabiliana na tukio hili.

Shukurani pia zinatolewa kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri majini, angani na nchi kavu, kwa jinsi walivyoshirikiana na serikali katika kulikabili tukio hilo, wakiwemo wananchi wa maeneo ya jirani hasa wavuvi na wamiliki wa hoteli na kampuni za kitalii wanapewa shukurani za kipekee, kwa jinsi walivyoshiriki kikamilifu tokea hatua za awali baada ya kupatikana taarifa ya kuzama kwa Meli ya Skagit. Tunawashukuru Washirika wa Maendeleo na Wawakilishi wa Nchi Marafiki kwa jinsi walivyochukulia suala hili na kutuunga mkono katika msiba huu wa kitaifa.

Vile vile tunazishukuru taasisi za kidini hasa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Ofisi ya Mufti, kwa kusaidia maandalizi ya mazishi ya marehemu waliotokana na ajali hiyo.

Mhe. Spika, tunawashukuru madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa namna walivyoshirikiana na kamati. Tunawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa na wafanyakazi wa Idara ya Kukabiliana na Maafa kwa kazi kubwa waliyofanya kwa kipindi chote kilichotokea janga hili.

Tunawashukuru wamiliki wa vyombo vya habari, wanahabari na wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla kwa kupokea tukio hili kwa masikitiko makubwa na katika kukabiliana na janga hili.

Aidha tunawashukuru wale wote walioweza kuchangia kwa hali na mali katika msiba huu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda nitoe pole maalum kwa wale wote wafiwa na waliohusika na msiba huu. Baada ya kutoa maelezo hayo nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee taarifa hii.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Waziri kwa taarifa hiyo ya Tukio la Kuzama kwa Meli ya Mv. Skagit. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Tukio la Kuzama kwa Meli ya Mv. Skagit.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya hadhara hii, kuweza kutoa maoni ya kamati. Vile vile tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha tukiwa wazima kabisa wenye afya njema kuja kutekeleza majukumu tuliyotumwa na wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa kuwa mujibu wa Kanuni zetu, ripoti hii haitakiwa kuchangiwa na Wajumbe, isipokuwa ni kuulizwa maswali. Kwa hivyo, nitaomba uniruhusu kwanza kumpongeza Mhe. Rashid Seif Suleiman kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kushika nafasi ya Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, ambayo iliyoachwa na ndugu yetu kipenzi Mhe. Hamad Masoud Hamad. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunamuombea kila la kheri ndugu yetu huyu mwenzetu, na tunamuomba kama kawaida yetu, tumejenga mashirikiano makubwa na yeye, kwa hiyo tutazidi kujenga mashirikiano makubwa, ili kuhakikisha kwamba majukumu mapya aliyopewa aweze kuyatekeleza kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi. Mhe. Spika, tunamuombea kila la kheri katika hayo majukumu yake mapya.

Vile vile Mhe. Spika, naomba nimpongeze ndugu yetu Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa moyo wake wa kizalendo wa kuweza kuamua kwa makusudi kuachia nafasi hiyo, ili kuonesha uwajibikaji wake au kuguswa na tukio hilo, naamini kwamba amerudi kwetu katika upande wa *back benchers*. Tunaamini kuwa amekuja kuongeza nguvu na sisi tunaahidi tutampa mashirikiano makubwa katika utekelezaji wa majukumu yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama kawaida yetu kwa upande wa *back benchers* tumeamua kwa makusudi kuondoa itikadi pamoja na utashi wa kisiasa, na kufanya kazi yetu kwa kuisimamia serikali katika utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa naomba niende katika kutoa Taarifa ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Tukio la Kuzama kwa Meli ya Mv. Skagit, iliyotokea tarehe 18/07/2012 katika eneo la Kisiwa cha Chumbe nje kidogo ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine tena tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana mbele ya Baraza lako Tukufu, tukiwa wazima wenye afya njema kwa ajili ya kujadili mambo mbali mbali yanayohusu mustakbali mzima wa maendeleo ya nchi yetu.

Aidha tunaishukuru neema hii aliyotupa Mwenyezi Mungu ya kuendelea kutupa neema ya pumzi zake, ili kuweza kutekeleza majukumu yetu ambayo tulikula kiapo kwa kukamata Msahafu kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu kwa ukweli, uwazi na uadilifu mkubwa.

Vile vile tunamuomba tena atuzidishie uzima na afya njema, ili tuiokoe nchi yetu kutokana na janga la umasikini, na ninaamini kwa ukweli na uadilifu tunaoendelea nao hivi sasa, basi naamini si muda mrefu nchi yetu itapiga hatua kubwa za maendeleo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, aidha kwa niaba ya Kamati nakushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu tukio hilo la maafa.

Pia naomba niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura walionileta hapa kuja kuwawakilisha, na naomba waendelee kuniamini na ninawaahidi kwamba nitawatumikia na nitajitahidi kuhakikisha kuwa wanatumikia kwa uadilifu mkubwa na nitaishauri serikali yetu kila ambalo nahisi litaweza kuisaidia serikali yetu na wananchi wetu kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati nachukua fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi wale wote waliofariki kutokana na ajali hiyo, pia kuwataka kuwa na subira wale wote waliopoteza ndugu na jamaa zao, pamoja na wale walionusurika katika ajali hiyo tunawatakia afya njema na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awape afueni, ili tuweze kujumuika nao na kuweza kuendelea na majukumu ya kujenga taifa letu.

Mhe. Spika, sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wewe mwenyewe binafsi, tulipata mshtuko mkubwa baada ya kupata taarifa ya kuzama kwa meli mchana wa siku ya Jumatano tarehe 18/07/2012. Kwa masikitiko makubwa meli iliyokuwa ikitokea Dar-es-Salaam kuja Zanzibar, kwani ilitukumbusha machungu tuliyoyapata takriban mwaka mmoja uliopita, ukizingatia tuliweza kupata msiba mkubwa unaolingana na huu.

Mhe. Spika, Kamati yangu inasikitika sana kwa kuona kuwa Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba vimekumbwa na misukosuko mikubwa katika usafiri wa baharini, ukiacha suala la kuzama kwa meli hii. Kwa kweli kwa mtu yeyote aliyekuwa makini hakupigwa na mshangao kutokea kwa ajali hii, kwa sababu kulikuwa na dalili ya kutokea ajali ya baharini, kwani kumekuwa na mfululizo wa matukio mbali mbali yakiashiria kutokea ajali ya meli baharini. Kwa mfano, baadhi ya meli kuzimika ovyo *engine* mara kwa mara huko baharini zikiwa katika safari zake za kila siku wakati ndani yake zikiwa na abiria wengi.

18

Mhe. Spika, tukio la kuzama kwa meli limetupa funzo kubwa, kwani tatizo kubwa tulilonalo hapa Zanzibar ni kutokuwa waaminifu na waadilifu na kusimamia majukumu tuliyopewa na dhana tunayopewa na wananchi wetu. Aidha uzembe au tamaa binafsi inapelekea kutowajibika ipasavyo kwa umma, kwani kuna mamlaka iliyopewa jukumu la kusimamia, kuhakikisha usalama wa vyombo baharini.

Lakini inaonesha kuwa mamlaka hiyo imeshindwa kabisa kazi hiyo, uzembe mkubwa unaendelea kufanyika ikiwemo kutokagua vizuri *engine* za boti au meli hizo, upakiaji wa abiria kiholela, ukataji wa tiketi ovyo bila ya kutumia vitambulisho, pamoja na uuzwaji ovyo wa tiketi vichochoroni bila ya kutumia ofisi zinazotambulikana kisheria, kitu ambacho kinapelekea kupakia abiria wengi kuliko uwezo wake.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana hata takwimu inayotolewa wakati chombo kinapopata ajali inakuwa ni tofauti na hali halisi ya idadi ya watu wanaokuwemo katika ajali hiyo.

Kwa hiyo, tunaitaka serikali kuhakikisha kwamba inasimamia watendaji wake kutekeleza yale majukumu waliyopewa, ili kuepusha ajali kama hizo zisitokee tena katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, jengine tunalojifunza ni kwamba serikali yetu kutokuzifanyia kazi kwa haraka ripoti mbali mbali, aidha za Kamati inazoziunda wao wenyewe au zile za Baraza lako Tukufu, hata taasisi mbali mbali za serikali inazozipelekea, kwani ukiangalia mambo mengi yaliyoshauriwa, basi yanakuwa kwa faida ya nchi yetu na pale tu zinapodharauliwa matokeo yake wakati mwengine yanakuwa na athari kubwa kwa jamii yetu kwa jumla.

Mhe. Spika, funzo hilo kwa serikali yetu ililolipata kama kawaida yetu tunaishauri sasa wakati umefika kuzifanyia kazi ripoti zote ilizopelekewa serikali, licha zile za Baraza la Wawakilishi bali na ripoti zote zilizopelekwa serikalini na taasisi mbali mbali.

Mhe. Spika, jambo jengine inaonesha kuna udhaifu mkubwa katika ukaguzi na usajili wa meli kutoangalia historia ya meli hizo kuanzia pale mwaka ilipotengenezwa, kazi ambazo ilipangiwa kuzifanya na muda wa uhai wa kutumika vyombo hivyo.

Vile vile udhaifu wa *modification* zinazofanyiwa meli hizo, ili kuongeza nafasi za kubakia abiria bila ya kuzingatia uwezo wa *engine* za vyombo hivyo, kwa lengo la kutengeneza faida kubwa bila ya kujali maisha ya watu.

Mhe. Spika, imekuwa ni jambo la kawaida kwa hivi sasa kwa mtu akitaka kusafiri kwa boti au meli anawaza mara tatu tatu, kwani hana uhakika wa kufika salama safari yake. Hali hii inaonesha kuwa hakuna uhakika wa usalama wa maisha yake, leo hii imekuwa hata wanafamilia wanaposafirisha jamaa zao huwa *pressure* juu mpaka wahakikishe kwamba wale watu wao wamefika salama.

Kwa hivyo, hivi sasa serikali imeweka rehani maisha ya wananchi wake, kwani hakuonekani juhudi zozote na waliokabidhiwa majukumu ya kusimamia usalama wa abiria wetu kama wako makini kiasi hichi, hii ni kusema kwamba wameshindwa kazi.

Lakini kwa kuwa mara ya kwanza Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa imesikia kilio cha Wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar, kwa kumtaka Mhe. Waziri ajiuzulu ambapo suala hili tulilipendekeza tokea ilipotekezea ajali ya Meli ya mwanzo ya Mv. *Spice Islander* tulimtaka Mhe. Waziri ajiuzulu, ili kuonesha uwajibikaji wa kisiasa, lakini kwa bahati mbaya hakufanya hivyo.

Mhe. Spika, hivi sasa tunamshukuru, kwa kuwa ameamua kuwajibika ili kuonesha kwamba na yeye ameguswa katika tukio hili kubwa la kitaifa, na hili wala asione tabu wala aibu, kwani kwa Mfumo huu tuliokuwa nao hivi sasa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Demokrasia ya Uwazi na Ukweli, ni jambo la kawaida kabisa na tunawaomba wengine wanaposhindwa kusimamia majukumu yao, basi waamue mapema kuliko kusubiri kung'olewa kwa nguvu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha sana kwa wananchi wetu, kwamba hata kuna baadhi ya wahanga waliopata ajali katika Meli ya Mv. *Spice Islander* bado hawajapata ubani wao

uliotengwa na serikali, lakini leo tayari kuna msiba mwengine mkubwa ulioikumba nchi yetu, na inawezekana pia ni miongoni mwa familia waliopata maafa katika ajali hiyo na kwenye maafa haya ikawa yamewakuta tena.

Kwa hivyo, kama wapo watu hawa basi tunamuomba Mwenyezi Mungu awape subira, kwani mtihani huu ni mkubwa wao na inabidi washukuru, kwa sababu kila mtihani anaokupa Mwenyezi Mungu basi ukiwa na subira ujue kuna kheri inakuja mbele yako.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza hili la Wawakilishi pamoja na Watanzania wote kwa jumla, tuwaombee kila la kheri katika kukabiliana na mitihani hii, pia tumuombe Mwenyezi Mungu awaepushe na mitihani mingine.

Mhe. Spika, kwa tukio hili kuna baadhi ya maneno yanayozungumzwa na baadhi ya wanasiasa kuwa kuna kundi ndani ya Baraza lako Tukufu kwamba lina chuki za ubaguzi wa kisiasa au baadhi ya Mawaziri. Kwa hivyo, tunataka kuwahakikishia wananchi wote wa Zanzibar kuwa sisi sote ni kitu kimoja, na tunafanya kazi zetu kwa pamoja kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wetu bila ya chuki wala upendeleo wowote, isipokuwa ni kwa maslahi ya umma, kwani hivi sasa tumeamua kuweka kando itikadi zetu za kisiasa na kuamua kujenga nchi yetu kwa pamoja, kwa maslahi ya taifa letu pamoja na wananchi wetu kwa jumla.

Kwa maana hiyo, tunamuomba kila mmoja atimize majukumu yake aliyotumwa na wananchi wake kwa upande wa Wawakilishi, na kuisimamia ipasavyo serikali na kuhakikisha kwamba usalama wa maisha yao na mali zao, na kwa mujibu wa Katiba na Sheria zote za hapa Zanzibar na Tanzania nzima.

Vile vile kusimamia uwajibikaji kwa watumishi wote wa umma katika majukumu waliyokabidhiwa na serikali, pia mawaziri kwa upande wao kuhakikisha wanawasimamia walio chini yao, ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa ajili ya kuimarisha ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaishauri serikali kuendelea kulitumia eneo la Kama kuwa ni eneo la kudumu kwa ajili ya kuzikiwa, kwani inaonesha eneo hilo lilitelekezwa mara tu baada ya kuzikwa watu waliofariki katika ajali iliyopita katika ya Meli ya Mv. *Spice Islander*. Lakini ukizingatia kwa kuwa hivi sasa eneo la Makaburi la Mwanakwerekwe limeshajaa kwa muda mrefu, bado linaendelea kuzikwa maiti hadi hivi sasa jambo ambalo halipendezi hata kidogo.

Mhe. Spika, Kamati yangu kutokana na funzo la ajali hii ya tatu mfululizo ndani ya miaka mitano, tumeona iko haja ya kuwashauri wananchi wetu kujikatia Bima za Maisha, ili yanapotokea majanga kama haya waweze kulipwa Fidia ya Bima ya Maisha au Afya kwa wale waliojeruhiwa au kupoteza uwezo wa kufanya kazi tena katika maisha yao, kuliko kutegemea ubani unaotolewa na serikali na kama utakuwepo.

Mhe. Spika, Ripoti ya Serikali imeeleza kuwa wamewasaidia jamaa za marehemu gharama za mazishi, pamoja na usafirishaji wa maiti, sanda na ubao. Lakini Kamati yangu inaiomba serikali pia kuwasaidia na gharama za takhtimu, kwani hali ya familia zetu tunazijua kwamba nyingi zinaishi katika hali duni ya maisha, na pengine hao waliofariki wengine ndio tegemeo lao katika

familia hizo, kwa hiyo kwao wao inakuwa huu ni msiba mkubwa mara mbili zaidi. Kwa hivyo, tunaamini jambo hilo litawapunguzia machungu wakati wa kuomboleza msiba.

Mhe. Spika, katika Ripoti ya Serikali ametueleza kuwa kuna baadhi ya wasamaria wema wanaendelea kufika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa ajili ya kutoa ubani wa mkono wa pole kwa upande wa fedha taslim, na zimewekwa katika *Account* maalum iliyofunguliwa kwenye Benki ya Watu wa Zanzibar wakati ilipotokezea ajali ya Meli ya Mv. *Spice Islander*.

Lakini hadi leo serikali yetu bado haijaanzisha Mfuko wa Maafa ambao utaweza kutumika au kusaidia wakati wowote maafa yanapotokea, aidha kwa upande wa baharini au nchi kavu, kwani ajali ziko za aina nyingi, kama vile kuna mafuriko, moto, ajali za ndege, meli, upepo mkali na kadhalika.

Kwa hiyo, kamati yangu inaishauri serikali kuanzisha Mfuko wa Maafa, kwani si busara kuendelea kutumia fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kama ilivyo hivi sasa, kwani inasababisha kuwazuia wafanyabiashara, mashirika na kampuni, taasisi au watu binafsi ambao wanahitaji kuchangia mfuko huo kushindwa kufanya hivyo. Aidha tunataka kujua katika *Account* hiyo maalum, je kutakuwa na utaratibu mpya wa utoaji wa ubani au kiasi kile kilichotolewa katika ajali ya mwanzo.

Mhe. Spika, pia Kamati yangu inaiuliza serikali kupitia ahadi zilizotolewa na baadhi ya taasisi za fedha, ambazo ziliahidi kuwasomesha baadhi ya watoto mayatima walioachwa na wazee waliopoteza maisha yao katika Meli ya Mv. *Spice Islander*, je serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imefuatilia kwa kiasi gani katika taasisi hizo za Fedha, ili kujua namna gani imetekelezwa ni mayatima wangapi ambao wanasomeshwa na Taasisi hizo za Fedha zilizoahidi kwa wakati ule?

Mhe. Spika, Kamati yangu inaiomba serikali kukiimarisha Kikosi chetu cha KMKM pamoja na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, ili kuweza kukabiliana na maafa ya ajali yoyote inayoweza kutokea ikiwa kwa baharini au nchi kavu kuwa na zana za kisasa, kama vile *helicopter* ya uokozi, ambayo itakuwa na huduma ya matibabu ya dharura inapokuwa angani, ili kuweza kuokoa maisha ya wananchi wetu popote majanga yanapotokea.

Vile vile tunaiomba serikali yetu kuandaa utaratibu mzuri wa uokozi, kwani tumeona udhaifu mkubwa wakati harakati za uokoaji pale bandarini hapakuwa na utaratibu mzuri wa nani aliyekuwa na amri ya mwisho katika kuongoza zoezi zima la uokozi. Kwa mfano, tumeshuhudia vyombo vilivyokuwa vikitumika ni vikubwa, kitu ambacho kilihitajika kutumia pia na vyombo vidogo vidogo, ambavyo vingeliweza kusaidia zaidi huduma ya uokozi.

Mhe. Spika, katika hali isiyokuwa ya kawaida au fadhaa tulishangaa kuona baada ya kutokea ajali hiyo chombo cha mwanzo kwenda katika tukio kiliwaacha wazamiaji, ambao wangeliweza kusaidia kuokoa maisha ya watu wengi, na badala yake chombo hicho kilijaa viongozi wakiwemo mawaziri utadhani wanakwenda kuangalia *cinema* huko baharini, wakati wao wenyewe hawajui hata kuogelea seuze kuokoa watu waliopata ajali, kwa kweli hili pia ni funzo kubwa tunatakiwa tujipange vizuri.

Jambo jengine la kushangaza, ni kule kuona hata kuna baadhi ya boti ambazo zilikwenda kuokoa watu waliozama kusikia nazo zimemalizika mafuta huko baharini, kitu ambacho ni kibaya sana kwani kingeliweza kusababisha ajali nyengine huko baharini. Kutokana na hali hiyo, inaonesha kuwa bado hatujakuwa na mipango mizuri na madhubuti ya uokozi pale majanga yanapotokea.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaiomba serikali kufanya ukaguzi wa kina kwa vyombo vyote vya baharini ikiwemo *engine* pamoja na uwezo wa manahodha na mabaharia wanaofanya kazi katika vyombo hivyo, na wakigundulika waliokuwa na uwezo kuachishwa kazi mara moja na bora kuwa na vyombo vichache vyenye uhakika kuliko kuwa na vyombo vingi visivyokuwa na ubora au kiwango.

Mhe. Spika, Kamati yangu bado inaiomba serikali yetu kufanya kila linalowezekana kununua meli ya kubebea abiria na mizigo, kwani ni aibu kuwa sisi tunachaguliwa na wananchi, tunalipwa mishahara kupitia kodi zao, lakini tunashindwa kuwahakikishia usalama wa maisha yao.

Mhe. Spika, pamoja na serikali yetu kununua meli hizo, kwa kuwa mazingira ya nchi yetu ni visiwa sio kama watu wote wataweza kusafiri siku moja na kupanda meli hizo za serikali kwa wakati mmoja.

Kwa hivyo, bado ni lazima kutakuwa na ulazima wa kuwa na vyombo vya watu binafsi, ndio maana tukasema kuwa suala kubwa hapa ni la ulazima, yaani kuhakikisha ukaguzi wa kina kwa usalama wa vyombo vyote vya baharini, kwani hata hizo meli za serikali pia nazo zinahitajika kukaguliwa wakati zinapokuwa katika safari zao kila wakati, kwani sio kama hizo meli za serikali hazitaweza kupata ajali ikiwa nazo hazitakuwa na ubora.

Mhe. Spika, kwa kumalizia tunaishauri serikali yetu kuwa sasa wakati umefika wa kuyatekeleza maoni na ushauri wa kamati zote, aidha ilizoziunda wenyewe kama vile Ripoti za Washauri mbali mbali wa nje na ndani ya nchi pamoja na Ripoti za Baraza la Wawakilishi, kwani zina faida kubwa kwa wananchi wetu kama zitatekelezwa kwa vitendo kwa muda muafaka.

Kwa maana hiyo, vyenginevyo hata hizo idara zilizoundwa katika wizara, yaani Idara ya Utafiti zitakuwa hazina maana yoyote, kwani na wao baada ya kufanya utafiti, baadaye pia watatakiwa kutoa ripoti serikalini, na ripoti hizo kama hazikufanyiwa kazi, basi yatakuwa hayo kwa hayo (*business as usual*).

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati yangu kwa kuwa wastahamilivu, kwa kunipa mashirikiano makubwa ya kuandaa ripoti hii, kwani tuliweza kukaa hadi saa 6 za usiku na kuweza kukamilisha asubuhi hii ya leo na kuiwasilisha hapa Barazani.

Mhe. Spika, mwisho naomba niwashukuru wananchi wote wa Zanzibar pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura walionileta hapa, ili kuwatumikia na ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa uadilifu na moyo wangu wote.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba kumkaribisha Mhe. Hamad Masoud Hamad katika nyumba yetu ya *back benchers*, ili kushirikiana na sisi kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar, kwa lengo la kuwaletea maendeleo na tunakuombea kila la kheri katika kazi yako hii mpya, ambayo kwa miaka mingi uliitumikia kwa uadilifu mkubwa na tunamuomba Mwenyezi Mungu akuepushe na shari nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru na Kanuni zinatuelekeza kwamba tupokee maswali juu ya taarifa hii. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Omar Ali Shehe aanze kuuliza maswali machache na baadaye Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuuliza maswali yanayotokana na ripoti hii.

Lakini kabla ya kuanza Mhe. Spika, naomba uniruhusu nianze kuitumia fursa hii kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Hamad Masoud Hamad, aliyekuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na Mwakilishi wa Jimbo la Ole. Kutokana na maamuzi yake ambayo mimi nayaita maamuzi ya kijasiri tena ni ya kishujaa, pia ni maamuzi ya kizalendo aliyochukua katika kujiuzulu kwa nafasi hii, kujiuzulu kwake ni kuwajibika kisiasa kama ilivyoelezwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kitendo chake hichi kinamjengea heshima na sifa kubwa Mhe. Hamad Masoud Hamad mbele ya macho ya wazanzibari. Vile vile kitendo hichi kinaijengea heshima Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kitendo chake hichi kinakijengea sifa na heshima kubwa Chama chake cha Wananchi CUF. Lakini zaidi kuliko yote kitendo chake hichi kinawajengea heshima wapiga kura wake waliomchagua wa Jimbo la Ole. Sisi wenzake katika chama na Baraza hili la Wawakilishi, kitendo chake kile kinatufanya sasa tutembee kifua mbele kwa kujiamini. *(Makofi)*

Vile vile nimpongeze Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani Mhe. Rashid Seif Suleiman kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nitoe wito kwa watendaji wote katika Sekta ya Umma kuanzia mawaziri na wengine wote, kwamba waige kitendo cha Mhe. Hamad Masoud Hamad. Kwa kweli Mhe. Hamad Masoud Hamad ametuonesha dira, lakini ametufungulia mlango wa utekelezaji na uwajibikaji katika serikali. Kwa hivyo, zaidi katika yote namshukuru sana, na namtakia kila la kheri katika maisha yake na sisi tunamtazamia mema na mazuri zaidi na Mwenyezi Mungu atamuweka pahala pazuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, maswali.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, baada ya hayo naomba niulize maswali mawili.

Kwa kuwa tukio hili lililotokea hivi karibuni, na hivi usafiri unaendelea baina ya visiwa vyetu vya Pemba, Unguja na Dar-es-Salaam na Pemba Tanga na kwengineko. Mhe. Spika, inaonekana vyombo tunavyosafiria ni vile vile ambavyo vina matatizo ya hapa na pale.

Kutokana na hali hiyo, naomba niulize serikali kwamba ndani ya kipindi hichi cha leo, kesho, kesho kutwa, wiki na mwezi serikali imejiandaa vipi kidharura pindi litakapotokea tena suala lile na hilo ni la kwanza, na ninachokizungumzia hapa ni kidharura.

Mhe. Spika, jana Mhe. Rais ameunda Tume ya kuchunguza tukio lile na baadaye itatoa ripoti. Lakini kabla ya matokeo ya kazi ya tume hii iliyoundwa nakumbuka kwamba kuna ripoti nyengine iliyotolewa na tume iliyopita kufuatia kuzama wa Meli ya Mv. *Spice Islander*.

Naomba niulize serikali ni kiasi gani ripoti ile imetekelezwa, ili tujenge matumaini kwamba na ripoti hii mpya itakayotolewa itafanyiwa kazi kama ilivyo?

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, na baadaye Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nimpongeze Mhe. Hamad Masoud Hamad kutokana na tukio lake aliloliamua jana kwa ghafla. Lakini naomba nimwambie kwamba *kuvunjika kwa koleo sio mwisho wa uhunzi*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nije kwenye maswali yangu matatu tu, inasemekana kwamba Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam alisema meli ilipakia abiria 330. Je, hapa serikali inasema watu 290, hivi ni kauli ipi hasa tushike kati ya hizi mbili?

Pili serikali imeanzisha Mfuko wa Maafa na ndio *Account* ya Mfuko huo, ili inapotokea ajali yoyote iweze kutatua matokeo yake. Je, Mhe. Spika, kwa kuwa kulikuwa na baadhi ya boti ambazo zilishindwa kwenda kuokoa na kukosa mafuta ya kufikia kwenye ajali. Je, Mhe. Spika, mfuko huu ulikuwa wapi kwa wakati huo, ili boti hizo zisipate mafuta na kuwahi kwenda kuokoa?

Tatu kwa kuwa wahanga wa meli ile walilipwa na wakajitokeza baadhi ya watu ambao hawakuhusika. Je, Mhe. Spika, serikali imejipanga vipi mara hii kutokana na kujitokeza kwa watu ambao hawahusiki na matukio kama haya?

Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana, sasa ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadaye Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kidogo nimpongeze Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa ujasiri alioufanya. Lakini kama alivyosema Mhe. Omar Ali Shehe kwamba wengine wakae tayari kujiuzulu kwa kuwajibika kisiasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maswali yangu ni matatu tu. Swali langu la kwanza je, Mhe. Waziri haoni haja hivi sasa zile fedha zetu tunazodai kule upande wa pili wa Serikali ya SMT kwenda kuzidai, ili kuweza kwenda kununulia vifaa vya kisasa?

Pili, ni lini serikali itatupa ahadi ya kuwa kama hii meli hivi sasa, kutokana na uokozi wa kuwa hizi meli nyengine kuwa hazifai na italeta meli zake mpya mbili?

Mwisho nimesikia hapa kwamba tume tayari imeshatangazwa. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba iko haja hivi sasa hata kama Mjumbe mmoja wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na yeye akatiwa kwenye tume hiyo? *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunashukuru. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadaye Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha tukiwa hai na wazima.

Mhe. Spika, kabla ya kuuliza maswali yangu mawili tu, naomba na mimi nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Ole na aliyekuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kwa uamuzi wake wa kishujaa na kijasiri wa kuamua kubeba dhamana ya kuwajibika kisiasa, hata kama yeye siye muhusika wa moja kwa moja na sababu zilizopelekea ajali hii. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Masoud Hamad kama alivyosema Mhe. Omar Ali Shehe hapa kwamba amejijengea heshima kubwa sana yeye mwenyewe, amelijingea heshima kubwa sana Jimbo la Ole pamoja na wananchi wake, pia amekijengea heshima kubwa sana Chama chetu cha Wananchi CUF. Vile vile ameijengea heshima kubwa sana Serikali ya Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama sikosei nadhani Mhe. Hamad Masoud Hamad ameweka *record* kwa kuwa Waziri wa kwanza katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kubeba dhamana ya kuwajibika kisiasa kwa matokeo yaliyotokea katika wizara anayoiongoza. Kwa kweli wengi wamengoja hadi zichukuliwe hatua kwao, lakini yeye ameonesha mfano wa hali ya juu kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi sina chembe ya wasi wasi Mhe. Spika, kwamba heshima hii aliyoijenga leo Mhe. Hamad Masoud Hamad itampandisha zaidi kisiasa lakini hata heshima yake katika jamii. Naamini kabisa maneno haya yanatoka ndani ya moyo wangu, kwamba tutamshuhudia Mhe. Hamad Masoud akipanda zaidi katika ulingo wa kisiasa kwa sababu ya kuonesha ujasiri wa uongozi aliouonesha. Namtakia kila la kheri na tutaendelea kumpa mashirikiano yote katika kuhakikisha kwamba anaendeleza harakati zake za kisiasa na kijamii kama ambavyo sisi wenzake tunafanya.

Mhe. Spika, pia nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Rashid Seif, Mwakilishi wa wananchi wa jimbo la Ziwani kwa uteuzi wake wa kubeba dhamana hii nzito, tunamtakia kila la kheria. Lakini vile vile tunamwambia kazi iliyokuwepo mbele yake si ndogo. Kwa hivyo anapaswa kujiandaa na kuhakikisha kwamba anatekeleza na kusimamia vyema majukumu yake.

Mhe. Spika, sasa naomba niulize maswali yangu.

1) Mhe. Waziri anisaidie kwamba zipo taarifa kwamba hii meli ya MV. Skagit ambayo ameitolea taarifa hapa mwaka iliotengenezwa na mwaka iliyosajiliwa Zanzibar. Ziko taarifa kwamba meli hii ilifanyiwa marekebisho na kuongezewa sehemu ambayo imepelekea kuzidi uwezo wake na pengine kushindwa kuhimili vishindo vya bahari yetu. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri anieleze kwamba kwa taarifa ya serikali ambazo inazo taarifa hizi ni sahihi.

Mhe. Spika, pili sisi wengine tulishiriki kiasi tulichoweza kusaidia juhudi za vikosi vya uokozi pale Bandarini. Kilichojitokeza kinyume na taarifa ya Mhe. Waziri kwamba kulikuwa kuna muitiko wa ghafla. Muitiko ulikuwa mkubwa kweli lakini kilichojitokeza ni kushindwa kazi kwa Kamati Nzima ya Maafa na kuonekana kwamba hakuna mpango wowote ulioandaliwa kukabiliana na kitu hicho kwa kipindi hicho kilichotokea, pamoja na kuwa tumekwisha kupata athari kama hiyo chini ya mwaka mmoja uliopita.
Mimi naamini Mhe. Spika, kwamba pengine tungeweza kuokoa maisha ya watu zaidi kama Kamati ya Maafa ingejipanga vizuri. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anisaidie swali langu hili kama hivi ifuatavyo:

(a) Nini sababu pamoja na kutuletea Sera hapa na mipango mingi, lakini ilipokuja katika utekelezaji Kamati hii ikaonekana haikufanya kazi.

(b) Kwa nini viongozi wa kisiasa waliokuwa na dhamana ya Kamati ya Maafa Wasifuate mfano wa Mhe. Hamad Masoud na wao wakawajibika kisiasa kuonekana mbele ya jamii kwamba wanajali maisha ya watu wa Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa idhini yako na mimi naomba niulize maswali matatu kwa Mhe. Waziri ili niweze kupata majibu.
Mhe. Spika, meli ambayo imezama ni meli ya Kampuni ya *Seagull Sea Transport* na meli ya *MV. Skagit* ilikuja sambamba na mdogo wake anaitwa *MV. Kalama* zote zinaelezwa kwamba ni meli ambazo hazina kiwango.
Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri:

1) Kwa kuwa MV. Skagit imezama. Na kwa kuwa Wazanzibari wanaamini hizi meli kwamba hazina kiwango. Je, ni lini serikali itapiga marufuku mdogo wake MV. Kalama, Seagull, na kila meli ambayo inamilikiwa na Kampuni hii ya Seagull.

2) Mhe. Spika, tukiwa Bandarini majira ya saa 8:30 mimi pamoja na wenzangu tulishuhudia vikosi vyetu vya Jeshi na SMZ vikiwa na boti zao, lakini zimeshindwa kupata mafuta. Na wapo baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walitoa maneno makali kwa kuwa serikali imeshindwa kuwapatia vikosi vyetu mafuta na hatimaye yakaingia mafuta kwenye gari pipa tatu. Je, Mhe. Waziri ni kweli kamati ya maafa inashindwa hata kuazima mafuta ya dharura kwa ajili ya kuwapatia vikosi vyetu vya ulinzi, mpaka itimie masaa matatu ndio mafuta yapatikane.

3) Tuliwashuhudia na tulilalamikiwa na wazamiaji wazalendo kwamba walikuwa wameingia kwenye boti kwa ajili ya kufata ajali hii, lakini viongozi wa Kamati ya Maafa waliwatoa na wakamruhusu mzungu na timu yake kwenda kuokoa. Kamati hii ya

Wazamiaji ndio ile ile iliyookoa kwenye MV. Spice na ile MV. Fatihi, lakini kwa nini juzi vijana wetu hao wasiopungua 15 waliteremshwa kwenye boti ambayo wengeweza kufika mapema, na wao ndio wanaojua mazingira ya bahari ya Zanzibar na bahari ya Tanzania. Mhe. Spika, naomba majibu hayo nijibiwe.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuuliza maswali machache kuhusu kadhia hii iliyokuwepo mbele yetu. Kwanza nami nimpongeze Mhe. Hamad Masoud kwa ujasiri wake aliouonesha kwa kuondoka katika nafasi hii baada ya kutokea tukio hili la kuzama kwa hii meli.

Mhe. Spika, lakini pia ningewaomba na Mawaziri wengine na wao pale ambapo patakuwa na kadhia iliyokithiri wasione tabu kujiondoa. Kama Mhe. Juma Duni alivyosema wakati ule pindipo kama suala la ICU yeye angejiondoa. Watu waliona ajabu na walikaa midomo wazi Waziri wa Zanzibar kusema hivyo. Kwa sababu ilikuwa ni jambo la ajabu kweli kweli kwa Mzanzibari kutamka hivyo.

Mhe. Spika, kuna msemo mmoja wa Kipemba kuwa "*Mswahili ni domo la ngalawa hadi agonge*" mimi nasema kwamba serikali imeshagonga.

(a) Je, hatuoni kwa sasa kuna haja ya ulazima kabisa kabisa serikali kununua meli yake ya uhakika ya usafiri kwa sababu imeshagonga ajali mbili mfululizo hizi.

(b) Jengine ni kuwa vikosi vyetu vya uokozi havina zana hasa za kuukolea, ni lini serikali yetu itajipanga kwa uhakika kuweka vikosi vya uokozi katika hali nzuri ya kuweza kukabiliana na maafa yatakayotokea popote pale nchini ama baharini, angani au nchi kavu?

(c) Kwa kuwa serikali imeunda Tume ya Kuchunguza ajali hii, na kwa kuwa katika Tume iliyopita ilikuwa ina zaidi ya watu wale ambao waliowasilishwa na Kamati ya Maafa. Je, tume hii mara hii itakuwa ina uhakika gani kuwa ripoti itakayopatikana na kamati ya maafa ilingane na tume hii ili kuepuka udanganyifu kama ilivyotokea katika tume iliyopita. Kwa sababu tume iliyopita ilikuwa ina watu zaidi kuliko wale halisi waliotajwa ila waliingizwa watu ambao hawamo. Hizi ajali watu wamefanya kama ni mradi je, mara hii serikali itahakikisha vipi kuwa huu usiwe mradi ili kama kuna msaada uwafike waliohusika tu. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kuuliza swali, lakini kabla ya hapo na mimi naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana kaka angu Mhe. Hamad Masoud ambaye kitendo alichokifanya ni cha ujasiri na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atakulipa kila la kheri, na Mwenyezi atakupa bora zaidi kuliko ulipoondoka.

Pia nichukue fursa hii Mhe. Spika, kumpongeza sana jirani yangu Mhe. Rashid Seif ambaye amekiacha kiti hichi na amesogea mbele. Lakini namwambia *hala hala jirani asije akajisahau*. Mhe. Spika, baada ya hapo na mimi napenda kuuliza swali moja.

Mhe. Spika, kwa kuwa maafa yanapotokea huwa hayaagi, kuzama kwa MV. Spice Islander, Uongozi wa Mkoa wa Kaskazini ulilazimika kukopa fedha shilingi milioni 28 kwa ajili ya uokozi. Fedha hizo hadi leo bado hazijalipwa. Je, serikali ina mpango gani kulilipa deni hili ili

kuufanya uongozi ule ukopesheke inapotokea dharura nyengine na kuwajengea viongozi hadhi ili wasionekane matapeli.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Nakushukuru Mhe. Spika, napenda nichukue fursa hii nimpongeze kaka angu Mhe. Hamad Masoud kwa uamuzi wake ambao ameuamua, na pia itakuwa ni faraja kubwa kwa wananchi wa jimbo la Ole.
Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kama kuna uuzaji wa tiketi za holela holela, na hivyo kupelekea mara tu meli zinapopata ajali kutokuwa na idadi ya uhakika wa abiria ambao walikuwemo katika meli hiyo. Je, serikali ina mpango gani wa kuweka utaratibu mzuri kwa uuzwaji wa tiketi hizo ili kuondosha usumbufu kwa abiria wetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Hamad Masoud Hamad aliyekuwa Waziri wa Miundombinu kwa kuwajibika katika hili. Nadhani Mhe. Hamad kwa sasa ni darasa ambalo watendaji, sitaki niseme kwa watendaji ng'ang'anizi, lakini wale walioshindwa kuwajibika watafuata kisogo chake. Naamini yeye atakuwa darasa.
Vile vile napenda nimpongeze Mhe. Rashid Seif Suleiman kwa *housemate* wangu kwa kuweza kuichukua hii nafasi. Matarajio yangu kwamba katika hili na mimi makole kole kwa sababu *housemate* wangu humu nitapatapata kidogo mambo ya mawasiliano.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hapa wamesema hizi tamaa tamaa tuziwache.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sna Mhe. Spika. Mhe. Spika, roho ya mtu huwezi kuipata kwa fedha, lulu, yakuti wala kito au madini ya aina yoyote. Kwa kuwa Mheshimiwa kuna viashiria mbali mbali ambavyo vinaonesha, mbali na kupoteza roho za watu kupitia hii MV. Spice Islander pamoja na hiyo Skagit, kuna kila dalili kwamba wakati wowote roho za Wazanzibari hapa zinaweza kupotea tena kwa kundi.
Hii ni kutokana meli zinazima kiholela hapo Nungwi zinakwenda zikifungashwa kama gari. Katika taarifa ya Mhe. Waziri hakuweka mpango wa mkakati wowote wa kuweza aidha kuzuia Makampuni yale kuleta mavyombo mabovu. Mfano juzi Seagull ilivutwa na Serengeti, na halafu nayo Serengeti nayo ikakwama huko ikaenda ikafutwa tena. Huku si kucheza na maisha ya Wazanzibari.

1) Je, huku si kucheza na maisha ya Wazanzibari na kupelekea kutokea kwa ajali nyengine.

2) Pamoja na taarifa ndefu ya serikali tuliyosomewa na Mhe. Waziri lakini vile vile naye hapa hakueleza kwamba baada ya ajali hizi mfululizo serikali inafanya nini. Yeye kazungumzia tu kukabili maafa lakini sio kukinga. Sasa haoni hapa Mheshimiwa kwamba taarifa hii tulifikiria kwamba angeeleza mpango kwamba wakati wowote tutapata meli ya uhakika ili kupunguza ajali.

3) Mhe. Spika, kuna hii Kamati ya Maafa kila ikitokea maafa wao wakusanye pesa, wapelekewe nini, na laiti ingelikuwa sio ndugu zetu wa Vikosi hivi vya SMZ pamoja na TPDF kwa kazi kubwa wanayoifanya. Nadhani hii Kamati ingekwama. Mimi nadhani Mhe. Waziri akija hapa atujibu wana mpango gani wa kuiboresha hii Kamati

ya Maafa, kwa sababu ishakuwa mazoea sasa kwamba kila baada ya mwaka siye tuna maafa. Lakini kila yakitokea maafa tunaona wanaoyakabili maafa haya ni TPDF, vikosi vyetu vya KMKM, JKU na KVZ. Kamati hii wanawaboresha vipi hawa.

4) Mhe. Spika, wakati yanatokea maafa haya ya juzi kuna watu kadhaa kwa makosa hawajapata ruzuku zao zilizotoka kwenye hizi MV. Spice Islander, kuna familia zilikuwa zinapewa laki tano tano kwa wale waliofariki, na sijui laki tatu tatu kwa wale waliokuwa hai. Kutokana na makosa na juzi juzi Waziri alikiri kwamba kuna familia ambazo hazijapata ruzuku ile ya serikali, na leo limeshatokea jengine hili. Je, Mhe. Waziri tuseme wale baada ya kutokea hili wale watakuwa ndio basi au serikali itaendelea kuwamalizia wale halafu ndio iwapatie na hawa ruzuku hizi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nitahadharishe tu kwamba tupunguze maelezo tuende kwenye maswali moja kwa moja ili kupunguza kutumia muda mkubwa. Shughuli zetu ni nyingi katika Mkutano huu.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza maswali machache tu katika kadhia hii ambayo ipo mbele yetu. Pia nachukua nafasi hii kwa dhati kabisa kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Chambani, kumpongeza Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa ujasiri wake aliouonesha kujiuzulu katika nafasi ya Uwaziri. Hapa kwa kweli niseme kwamba amefanya kazi nzuri, hongera sana.

Lakini pia nachukua nafasi ya kumpongeza Mhe. Rashid Seif kuwa Waziri mteule. *Inshallah* tunamtakia kila la kheri na mafanikio mema.

Maswali yangu Mheshimiwa kwa kuwa kuna usemi wa Kiswahili unasema "*Hasara humfika mwenye dezo*" na kwa kuwa tokea tulipoanza Baraza hili si vikao vingi ambavyo hakuna masuali yanayoulizwa katika Wizara ya Miundombinu kuhusiana na ununuzi wa meli mpya itakayowasaidia Wazanzibari kuondoa kadhia hii.

1) Je, serikali ina mpango gani hasa na kauli gani sahihi ya kununua meli katika visiwa hivi.

2) Kuna hii kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam kwamba watu waliokuwepo katika meli ile ni 320, na kauli ya Serikali ya Zanzibar kwamba Kamati imesema kwamba ni watu 290 ni ipi kauli sahihi.

3) Kwa kuwa boti zote zilizosajiliwa hapa naamini kwamba zimefungua Ofisi zao. Ofisi hizi madhumuni yake ni kwa ajili ya ufanisi wa kazi pamoja na kuuza tiketi. Lakini utawakutia watu wengi ni wapambe wa ofisi hizo wanauza tiketi nje ya ofisi ile, hii inapelekea kuongeza idadi isiyokuwa sahihi katika kuingiza watu ndani ya chombo kile. Je, serikali ina utaratibu gani wa kudhibiti uuzaji wa tiketi kwa vyombo hivi ili kujua idadi halisi ya wanaoingia katika chombo kile. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe maswali yamekuwa yakianza kujirejea rejea. Nia ni kupunguza muda ili Waziri baadae ajibu maswali hayo. Nimetoa nafasi kwa waulizaji maswali mengi kwa sababu ya uzito na umuhimu wa jambo lenyewe, lakini yakijirejea itakuwa

tunapoteza muda bure. Kama kuna Mhe. Mjumbe ataona swali ambalo alilikusudia kuuliza limeshaulizwa basi anaweza akaniashiria kwamba mie nifute.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili. Kwanza na mimi ningewapongeza yule ambaye karudi nyuma na yule ambaye kenda mbele. Lakini yule aliyerudi nyuma alikuwa akiendesha baskeli ambaye alikuwa kawapakia na wenzake, mnyororo kwa bahati umekatika njiani. Sasa ili baskeli itembee kuwa iwe inakwenda kwa mnyororo.
Mimi ngependa kwa vile mnyororo unakuwa unacheni nyingi, wale wenzake na wao wakajua kwamba wajibu wao kwa vile ilikuwa tunaendesha baskeli ya pamoja, na wao wakachukua nafasi zao wakasema kwamba na sisi kwa hili tunahitajika kuondoka.
Mhe. Spika, mimi suala langu kwamba tumepata ajali ya meli tatu, MV. Fatih mwaka 2009, MV. Spice mwaka 2011 na MV. Skagit mwaka 2012. Meli hizi zote zilizopata ajali zilianzia safari yake Bandari ya Dar-es-Salaam. Moja ilipita ikenda ikatokea kuzama baada ya kupita Zanzibar. Lakini safari zote hizi zilianzia Dar-es-Salaam.

1) Ningependa kuuliza tu je, serikali sijui imefanya utafiti wowote kuhusiana na mtiririko huu. Mbona hizi meli zote zilizopata ajali zimeanzia safari bandari ya Dar-es-Salaam. Na je, pengine watafanya utafiti na kutuletea utafiti huo kwa wakati wake ili tukajua nini sababu yake.

2) Mhe. Spika, meli zetu zina usajili, je, hii meli ambayo kwa mara ya mwisho ilipata ajali ilikuwa ina vipimo vyote vya *Zanzibar Maritime Authority* au ilipata ile *Certificate* ya *Sea Worthiness.* Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nami nashukuru asubuhi hii kupata nafasi hii, niungane mkono na wale wenzangu waliompa hongera Mhe. Hamad pamoja na Mhe. Rashid.
Mhe. Spika, mimi nitakuwa na maswali mawili.

1) Mhe. Spika, eneo la Kama kwa sasa limekuwa ni eneo la kumbukumbu za wahanga waliopata ajali baharini. Je, serikali ina mpango gani wa kuwaekea alama wahanga hawa.

2) Kutokana na uvamizi wa ardhi tulionao hapa Zanzibar nimepata tetesi na kule Kama Uhamiaji unasogea karibu. Je, serikali haioni kwamba kulidhibiti lile eneo tulilolifanya ni sehemu ya ajali zinazotokea kuliwekea uzito, haioni kama hili nalo ni jambo muhimu. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuuliza swali. Kwanza niipongeze serikali kwa kujua katika kitengo cha uokozi Jumuia binafsi na Kampuni binafsi. Lakini niseme tu katika jumuia ya maendeleo ya Wavuvi wa Kojani wanacho kitengo cha ma – *diver* tena walio wazuri. Mpaka jana maiti zilizookotwa 5 kutoka Kisiwa cha Chumbe na Mwamba wa Nyange bado wanashiriki. Lakini wamekosa kutambulika rasmi kama ma- *diver*.

1) Swali ni lini serikali itawapa kipaumbele jumuia hiyo ya Wakojani wenye ma- *diver* wazuri ili na wao wawe waokozi wa kudumu hapa Zanzibar.

2) Mhe. Spika, bahari haizoeleki, fanya uizowee unavyoizowea lakini kuna siku itakupindua. Je, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na matukio haya ya kuzama kwa meli mara kwa mara, imejifunza lipi na ni lini italeta vyombo vya uhakika kwa sababu Zanzibar ni Visiwa njia yetu kuu ya baharini. Je, ni lini serikali italichukulia suala hili la kuleta meli ya serikali ili kuepukana na maafa ya mara kwa mara.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika katika hali ya usalama na uzima.
Lakini na mimi nitakuwa mwizi wa fadhila Mhe. Spika, kama sikumpa pongezi za dhati kabisa Mhe. Hamad Masoud, kwa kweli ameonesha ujasiri na ni ujasiri wa kuigwa kwa wale wangine ambao watafanya matatizo kama yake yeye na si yake yeye ni matatizo ya Mwenyezi Mungu. Lakini ameona kwa sababu yeye katika dunia ndio anaongoza ndio amewajibika. Sasa nimwambie tu mwanangu Hamad Masoud kwamba, *kujikwaa si kuanguka bali ni kwenda mbele.* Kuna rizki ambayo Mwenyezi Mungu amekuwekea na *kila likuepukalo mja lina kheri na weye*. Baada ya kusema hayo nimpe pole Waziri ambaye mteule na hongera, lakini kwanza nampa pole, maana hii wizara ni nzito na ni ngumu lakini Mwenyezi Mungu atakusaidia na pia nimpe hongera.
Mhe. Spika, niseme tu kwamba Marehemu Mzee Abeid Amani Karume katika shughuli zake alizozifanya moja aliwanunulia wananchi wake meli mbili za kusafiria. Sasa je, kwa sababu meli zile ziliuzwa je, serikali iko tayari kufidia pesa zile zilizouzwa, meli zile mbili za abiria kuhakikisha kwamba zinaongezwa pesa nyengine kununuliwa meli kwa ajili ya wananchi katika usafiri. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwanza nachukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Hamad Masoud kwa uamuzi wake ambao ameuchukua, lakini pia nachukua fursa hii kumpongeza jirani yetu na mzee wetu Mzee Rashid Seif kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara hii.

1) Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka nipate maelekezo kidogo tu kuhusiana na suala zima hili la mambo haya ambayo yanaendelea kutokea katika nchi yetu. Suala la uwajibikaji katika suala zima la mambo ambayo kuwa yametokezea ni suala moja, lakini suala la Sera katika utaratibu mzima wa vyombo ambavyo vinafanya safari zake katika visiwa vyetu vya Zanzibar na Pemba pamoja na Dar-es-Salaam.

2) Je, Wizara imejipanga vipi katika kuhakikisha kwamba inatengeneza Sera makini na imara, kuhakikisha kwamba matatizo haya yanaendelea kutokea siku hadi siku yanamalizika na yanakuwa ni hadithi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii nimuulize maswali Mhe. Waziri.

1) Mhe. Spika, kumekuwa na tatizo inapotokezea ajali kama hivi la kuweza kuzitambua maiti baada ya muda mchache tu wa kutokea lile tukio. Nataka kuiuliza serikali ni lini itakuwa na kifaa cha *DNA* ili kuweza kutambua kwa urahisi maiti zile ambazo zitakuwa zimeharibika.

2) Mhe. Spika, nilikuwa nataka kujua serikali ina mpango gani wa kupanua ile *mortuary*, kwa sababu katika maelezo ya Mhe. Waziri hapa amesema kwamba ufinyu wa nafasi ya *mortuary* unafanya zile maiti zizikwe kwa haraka, badala ya kuzihifadhi. Sasa ni lini serikali itakuwa na mpango wa kuipanua *mortuary* ili inapotokezea majanga kama haya kuweza kuzihifadhi kwa muda mrefu zile maiti, ili wenyewe waweze kuzitambua. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuuliza swali. Kwa vile uokozi unapoanza hutafuta meli yenyewe kwanza na kutafuta wahanga wakiwemo maiti na majeruhi na waathirika wengi hubaki katika meli ile.

(1) Je, serikali ina mpango gani kwanza kuifanyia ile meli kuiwekea kitu japo boya ili kuizuia na kuitambua meli ile imekwenda wapi. Kwa sababu meli ikisha inapotea kabisa na miili ya watu wengi. Kwa hivyo serikali itachukua juhudi gani kwani inaweza ikawa watu wengi wamo mle na wakawa wazima.

(2) Kwa sababu meli iliyopita ya *Spice Islander* kulikuwa kuna mtu ambaye ni wa karibu zilikuwa zinatumwa *message* tupu tupu, kwa hivyo inaonekana meli ile inakuwa na watu wengi ambao wako hai, lakini baada ya muda meli ile inapotea. Je serikali itakuwa na mpango gani baada ya kufika tu tukio lile meli ile ikaifunga boya au chochote ambacho kitaizuia meli ile. Ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, kama hivi ifuatavyo:

1) Ni kweli MV. Skagit kwa mujibu wa *operating resection* zilizotolewa Marekekani nchi ambayo ndiko ilikotengenezwa meli hii kuwa hairuhusiwi kwenda zaidi ya maili 20 kutoka bandarini.

2) Kwa mujibu wa *instruction* hizo, meli hii haikuwa na deki ya kago, hivyo haikuruhusiwa kubeba mizigo. Ni kwa nini meli hii ilikuwa inabeba mizigo tani 40.

3) Katika ripoti ya Mhe. Waziri ametueleza tulichojifunza kutokana na matukio yote yaliyoelezwa matokeo ya baada ya ajali. Je serikali imejifunza nini kutokana na matukio yote mawili ya kuzama kwa meli ya *MV. Spice Islander* na *Mv. Skagit* ili kukinga ajali nyengine zisiweze kutokea.

4) Kwa kuwa Serikali imetoa kauli juu ya tukio la kuzama kwa mweli ya Mv. Skagit ndani ya Baraza la Wawakilishi, na kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi ameunda tume kuchunguza tukio hilo. Je, serikali itakuwa tayari kuwasilisha ripoti hiyo baada ya tume kuwasilisha ili Wawakilishi wa wananchi wapate nafasi ya kuijadili na isiwe kama ile ya meli ya MV. Spice Islander iliyokuwa imetolewa.

5) Lakini la mwisho Mhe. Waziri kwa mujibu wa sheria ya usafiri baharini ya mwaka 1996, ili meli iweze kusajiliwa lazima iwe na Bima kwa ajili ya abiria na mizigo. Je meli hii inayo bima kwa ajili ya abiria na mizigo.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Ninakushukuru Mhe. Spika, kwa kuwa kujuta kutenda kosa ni kutolirejea, Mhe. Spika, bandari ya Wete kuna boti ya mbao ambayo ilizuiwa kubeba abiria kupeleka Tanga na Pemba, lakini kwa kuwa inasemekana kuna mkono wa mkubwa ina kibali sasa hivi cha kufanya hivyo. Je, ili wananchi wa kisiwa kile cha Pemba matumbo yao yatulizane kwa hofu ya kupoteza ndugu zao kila siku, serikali inachukua kauli gani ili chombo kile sasa hivi kisite kufanya hivyo. Moja.

La pili, Mhe. Spika, wananchi bado wana kumbukumbu ya kauli ya kiongozi mkuu baada ya tukio baya la kuzama kwa mweli ya Spice Islander, kwamba serikali ingelifanya iwezekanavyo tukio kama lile lisitokee tena. Bahati mbaya tukio limetokea tena kuna kauli gani nyengine dhidi ya hii.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku ulituma ombi kwamba unataka kuchangia sijui unakusudia hoja itakayokuja baadae au unataka kuuliza maswali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza na mimi uniruhusu kwa sekunde japo moja nimshukuru Mhe. Hamad Masoud rafiki yangu kwa kitendo cha uungwana alichokionesha, ni cha ujasiri na cha uzalendo na wengine waige mfano kama huu Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tumekuwa tunaambizana sana hapa kwamba hizi simu tusiziwache wazi zinaingiliana na mawasiliano ya humu ndani hili jambo hatusikii, mnadiriki mpaka wengine mnasikiliza simu humu ndani. Nitatekeleza kanuni kumtoa mtu ambaye anafanya hivi. Hilo ni onyo baada ya kuona Mhe. Jaku simu yake kaacha wazi, lakini watakaofuata sasa itabidi watekeleze kanuni. Mhe. Jaku uliza swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Serikali ina mpango gani wa kununua kifaa ambacho niliwahi kukipigia kelele kwa muda mrefu kinaitwa GMDSS ni Global Maritime Distress and Safety System, hiki chombo ni muhimu na kina sifa karibu zote ikiwemo *printer* kujulisha hali ya hewa ilivyo, GPS na Radio ili kiweze kuwekwa kwenye *signal tower* kwenye mnara wa kuongozea meli hiki chombo ni muhimu sana sana, nikikipigia kelele mara nyingi mpaka leo serikali ninafikiri itakuwa labda ikijipanga kununua kifaa hiki, nataka maelezo hapo Mhe. Spika.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Hamad Masoud na kumpongeza Mhe. Rashid Seif. Mhe. Spika, mimi suali langu litakuwa moja tu. Kwa kuwa inapotokea ajali huwa haina kinga na kwa kuwa kuna sheria ya mpanda vespa yoyote avae *helmet*, na sheria hii imechukuliwa kwa nguvu na kutekelezwa na wananchi, na kwa kuwa katika meli kuna *life jacket*, lakini *life jacket* hizi hazivaliwi mpaka inapotokea ajali. Je serikali ina mpango gani kuona kwamba baada ya kuingia katika chombo abiria wanavishwa *life jacket* kabla ya kuondoka meli hiyo.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kuuliza maswali matatu kama ifuatavyo:-

La kwanza, je ni sababu zipi zilizopelekea Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kulizuia Shirika la Meli lisikope meli mpya kubwa na ya kisasa.

La pili, je nani angepaswa kubeba dhamana ya kadhia hii ni serikali iliyo na wajibu wa kuwatafutia wazanzibari meli au Waziri wa miundombinu anayelazimika kutii agizo la serikali.

Tatu, je serikali haioni kwamba ajali hizi zinachangia kwa kiasi kikubwa na kutokuwa makini kwa mamlaka za udhibiti wa usafiri wa baharini kama vile Zanzibar Marine Authority na Sumatra.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Katika ajali ya mwanzo iliyotokea ya meli ya Spice Islander taarifa tuliyopewa ya nahodha wa meli ile alipotea, na mpaka leo hakuna ripoti yoyote iliyokuja kutueleza kwamba nahodha yule amepatikana au amefariki. Je, Mhe. Waziri taarifa ya nahodha yule ikoje mpaka hivi sasa.

Pili nahodha wa meli hii iliyopata ajali juzi ya Skagit taarifa zake za unahodha ana vyeti sahihi vya unahodha.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na taadhima ninakushukuru kunipa nafasi na mimi kuuliza swali. Lakini Mhe. Spika, kwa ruhusa yako vile vile kabla ya suali langu ambalo litakuwa la mwisho, nakuomba unipe dakika chache tu nizungumze maneno yafuatayo, na ninaamini fursa hiyo umeshanipa.

Mhe. Spika, niliyejiuzulu uwaziri ni mimi Hamad Masoud Hamad Mwakilishi wa Jimbo la Ole. Sikujiuzulu kwa sababu tu suala la kujiuzulu liko duniani, nina sababu zangu za msingi kabisa.

Mimi katika Baraza hili na katika Uwaziri Mwenyezi Mungu pamoja na kwamba keshaandika lakini kuna sababu, sababu kubwa ni chama, bila ya chama humu huingii. Baada ya tukio la tarehe 18 Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe mimi kama binaadamu kiongozi wa kisiasa nilikaa nikatafakari mwenyewe tu, na baadae baada ya kufanya maamuzi yangu nikasema maamuzi haya ngoja kwanza yapate baraka au ushauri mwengine kutokana na viongozi wangu wakuu. Maalim Seif ni Katibu Mkuu wa Chama na ni Makamo wa Kwanza wa Rais yuko India sasa hivi. Kabla ya tukio hili tumeshawasiliana katika kuulizana hali, kwa hivyo nikawa na simu yake, nikamueleza maamuzi ambayo ninakusudia kufanya, *subject to approval*. Tukachukua muda mrefu pamoja na kwamba yuko hospitali lakini tulichukua karibu dakika 20 ninazungumza nae.

Sikuishia hapo nikazungumza na Mwenyekiti wangu wa taifa Profesa Ibrahim Lipumba. *We took about one hour*, wakanambia tumesikia tupe muda halafu tutakupigia. Wakachukuwa muda mrefu kidogo, lakini saa sita za usiku simu ilikuwa wazi na ilikuwa kwenye *normal position*, Profesa akanipigia simu akanambia nimezungumza na mwenzangu Katibu Mkuu na pia nimezungumza na Makamo Mwenyekiti wa Chama hao ndio *supreme* katika chama chetu cha wananchi CUF, na baada ya mazumzo yetu sawa na niliwaambia maamuzi yangu na nimemuandikia barua Rais kwa sababu Rais ndie aliyeniteua, pamoja na kwamba kimependekeza lakini Rais angesema hapana basi vile vile ingekuwa hapana.

Basi bada ya mashauriano hayo mimi mwenyewe kabisa kabisa nimeshawishika hakuna *pressure*, wala sijasikiliza maneno ya mtu yoyote yawe ya Wajumbe wa Baraza hili au nje ya

Baraza hili. Mhe. Spika, tarehe 20 nikaandika barua tena si ya kujificha very *official*, kwa *letter head* ya Wizara kama Waziri wa Miundombinu, nikaandika barua kumpelekea Mhe. Rais hiyo ni tarehe 20. Baada ya kuandika barua ile na kui-*sign* nikaichukua mwenyewe mkononi Wajumbe mtanivumilia, moja kwa moja Ikulu nikamuomba Katibu wa Rais amuombe Rais nipate dakika mbili kuonana nae nina kitu muhimu. Barua bahati mbaya koti nililovaa leo sio nililovaa siku hiyo, lakini ningesema ulizeni mfuko wa koti niliiweka hapa. Basi kanambia sasa hivi Rais ameenda kufungua msikiti lakini nitampa salamu zako.

Saa nane na nusu siku ya Ijumaa tarehe 20 nikapigiwa simu kuwa kuna Kamati ya ulinzi na usalama wa taifa inaongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano, wewe unatakiwa uwepo na timu yako yote ya Wizara. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe nikahudhuria kikao kile ambacho kilianza saa tisa hivi lakini tulimaliza karibu saa 3.00 usiku. Baada ya kumaliza kikao kile Mhe. Rais akanambia nimepewa salamu zako basi akaniona.

Kwa hivyo kwanza hapa nina-*establish* kwamba sikuandika barua ile baada ya Kamati ya ulinzi na usalama, nikamuona Mhe. Rais nikamueleza niliyoyakusudia. *Friendly speaking he was shocked,* maana yake mtu unamsoma ile sura yake, kwa nini unafanya uamuzi wa haraka kiasi hiki *that the question* aliloniuliza Mhe. Rais. Nikamwambia Mhe. Rais ninakuomba upokee barua yangu, akaipokea mkono kwa mkono wala sikuwa nimeifunga, sitaki nimpe tabu ya kufunguafungua ikachanika ikaja ikawa sehemu nyengine amesoma ikawa imechanika hapana. Mhe. Rais akaichukua akanambia sawa ninaichukua ile barua nakwenda kuisoma na nitakwita, kwa hivyo mimi tarehe 20 nikabaki nasubiri kuitwa na Mhe. Rais.

Mhe. Rais kama kawaida yake aliwasiliana na Makamo wa kwanza wa Rais hiyo kanambia yeye mwenyewe.

Mhe. Spika: Nadhani mambo mengine ya mazungumzo ya viongozi waachie wenyewe.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Ninakushukuru. Mhe. Spika, kwa kifupi ilikuwa baada ya mazungumzo yao Mhe. Rais jana kanita saa sita za mchana nikenda kule tukazungumza mambo mengi sitaki niyaseme ni maneno gani, lakini kama nilivyosema akanambia kwamba baada ya mazungumzo yote hayo na viongozi na barua yako hii basi ninakushukuru ombi lako nimelikubali. Kwa hivyo hii ni *true story*, mwengine yoyote mwenye hadithi nyengine hiyo ni yake.

Mhe. Spika, jana nilipanga wakati ni Waziri kufanya kikao cha uongozi cha wizara, wajumbe walikuwa wananisubiri, tumekutana na wajumbe wale hawajui kilichopo, wamejitayarisha kwa ajili ya kikao nilichowaita. Lakini habari nilizowapa ni kwamba sitoweza ku-*chair* kikao hicho kwa sababu zifuatazo; mimi nimeshajiuzulu Uwaziri na nikaomba radhi tu kwamba miezi ishirini ambao nimekaa nao ni muda mrefu kibinaadamu, binaadamu ana mapungufu yake. Mimi nikawathibitishia kwamba kama kuna kosa lolote mtu yoyote amenifanyia iwe ninalijua au silijui mimi nimemsamehe *dunia fil akhera*, na wao nikawaomba wana hiari kama na wao watanisamehe.

Mimi ndie niliyejiuzulu, sababu za kujiuzulu ziko nyingi, lakini ninapingana kabisa kabisa tena wazi wazi katika Baraza hili sababu aliyoitoa Mhe. Hamza, sijajiuzulu kwa kushindwa

kusimamia shughuli zangu, nimefanya shughuli zangu miezi 20 kama una kitu cha kupimia miezi 20 hii ilinganishwe na wengine waliokaa pale miezi 60.

Mhe. Spika, namaliza mimi bado ni Mwakilishi wa jimbo la Ole, lakini pia nataka niwashukuru sana sana wale wote walionipongeza. Mhe. Spika, kitendo changu cha kujiuzulu ni kitendo cha kijasiri, cha kishupavu, na kiungwana, na kukubali kubeba dhamana ya kuwajibika kisiasa, mimi ni mwanasiasa, na ninaamini halijatokea miaka mingi hapa Tanzania atakuwa *shocked*, na wengine hawajaamini mpaka leo, hata hiyo radio ninafikiri labda yuko usingizini, ni kweli nimejiuzulu kwa sababu hizo. Na kwa malengo mafupi tu kujenga maisha yangu mimi mwenyewe, chama changu na serikali ambayo ninaitumikia.

Lakini vile vile wananchi wa Jimbo la Ole walionileta hapa kwa hivyo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima, nataka nimpongeze Mhe. Rashid kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano badala yangu mimi. Na jana nilimpigia simu mara nyingi lakini simu yake ilikuwa *busy* au haipatikani, nikampelekea *message* sitaki niisome maana yake nitafungua simu nitakuwa navunja kanuni na amri yako. Lakini yeye mwenyewe atakuwa ameiona nimempongeza kwa dhati, nimemuombea kila la kheri, na nikamwambia ushirikiano wangu mimi ni wakati wowote na popote katika hili.

Mhe. Spika, sitaki nichukue muda wako mrefu, lakini ninawashukuru tena wote ambao wamenipongeza kwa dhati. Na kwa sababu lolote utakalofanya binaadamu watasema tu liwe zuri au liwe baya, kila mtu ana namna yake ya kusema na hata wale ambao wamekejeli na wao walikuwa na haki yao ya kusema. Lakini wote kwa jumla mimi narudi *back bencher* ndiko nilikotokea. Na nitashiriki kikamilifu hata kama nina mazoea miezi ishirini katika serikali, lakini nitachangia *very very constructively* hata kama nilikuwa kwenye serikali, lakini nitachangia katika baraza hili kama ni wajibu wangu.

Mhe. Spika, nimekuwepo kule *front bench* kwa muda wa miezi 2, wenzangu wamebaki nawaombea Mwenyezi Mungu awajalie kubakia huko huko kabisa kabisa. Na kwa bahati mbaya kwa sababu limetokea ghafla sikuweza kuwaaga. Kwa hivyo nachukua fursa hii vile vile na wao tumekaa muda mrefu, bado ni marafiki, ni ndugu, kilichobadilika hapa ni uwaziri na kwamba sio kule mbele. Lakini uhusiano wetu, urafiki wetu, na zaidi Mhe.Waziri wa Fedha *is my best friend*. Ingawa urafiki huu wengine hawaupendi lakini ndio dunia huwezi ukamchagulia mtu rafiki.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa kwa heshima na taadhima mimi ni mwenzenu nimekuwa Waziri sawa, lakini pia Mhe. Spika, lilipotokea hili bahati nzuri mimi mwenyewe sikuwa kwenye *site* lakini pale ofisini nilikuwepo, tulichofanya haraka haraka ni meli zilizokuwepo ambazo hazikupangiwa kuwepo zimekuja tu moja kutoka Pemba, Dar es Salaam nendeni kule, hatukuwa na timu ya waokoaji kwenye chumba ili iletwe pale. Kwa hivyo suala la kusema kwamba imeondoka meli bila ya waokozi wakaingia Mawaziri kama vile wanakwenda kumpokea Rais si hivyo.

Ingekuwa hivyo kama waokozi wapo tayari ni wa kuwachukua tukawa tumewadharau. Unawapigia simu wengine wapo Bumbwini, mwengine yuko Donge, mwengine yupo wapi utamsubiri mpaka huyo aje, halafu ndio mwende huku watu wanakufa. Tumeokoa kadri ya Mwenyezi Mungu alivyokubali kuokoa na si kwa sababu tulidharau kuwachukua waokozi. Mhe.

Spika, suali langu katika suala hili, je Mhe. Waziri atatwambia ni nchi ngapi hadi sasa zilizotuma rambirambi au kuja wenyewe kwenye tukio hili la kuzama kwa meli ambayo imeua zaidi ya watu 60

Mhe. Spika, ninakushukuru sana.

Mhe. Spika: Nimempa nafasi Mhe. Hamad mwisho kwa makusudi, nilijua kuna baadhi ya maelezo yatahitaji majibu ambayo yamejitokeza katika masuali ambayo Mhe. Asingeweza kuyajibu isipokuwa yeye mwenyewe.

Sasa maswali ni mengi, mimi labda Waziri anambie yuko tayari lakini nilitaka nimpe muda ili akajitayarishe. Maana kuna mengine wala majibu hawezi kuyapata leo hii. Lakini akajitayarishe kwa sababu masuali haya ni muhimu, ni vizuri yakatoka majibu yaliyo mazuri yaliyo sahihi. Kwa hivyo nilichotaka kufanya ni kwamba nimpe muda ili majibu haya aje ayatoe kesho. Na hapa tuendelee na shughuli iliyopo baada ya hii. Ninafikiri huo uwe ni muongozo, mengine itabidi azungumze si kutwa pengine na wizara yenyewe, mengine itabidi azungumze na kamati yake, lakini nadhani si rahisi sana kuweza kuyatoa kwa sababu ni mengi mno. Nadhani tukubaliane hivyo nadhani Mhe. Waziri sawasawa.

Kwa hivyo baada ya hayo ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote nilitoa nafasi kubwa, pana ya kutosha, ili kwa umuhimu wa jambo hili zito wananchi hatimae wapate kuelewa juu ya jambo hili na taarifa hii ya serikali.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimkaribishe Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2012/2013

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo kunipa nafasi hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti yetu, lakini kabla sijafanya hivyo naomba kwanza nianze kuwapa pole wale wote waliopata msiba wa chombo kile cha Skagit na kuwatakia wawe na subira na *inshaallah* wale wote ambao wametangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi, na wale ambao walipata majeraha *inshaallah* Mwenyezi Mungu awajaalie wapone haraka.

Pia nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kumpongeza sana ndugu yangu Waziri mwenzangu Mhe. Hamad Masoud kwa kitendo cha kiungwana na kutuonesha njia za kiungwana sisi mawaziri wenzake linapotokea jambo kama hilo. Tutaendelea kushirikiana nae ni hazina kubwa katika nchi yetu.

Pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Rais wa Zanzibar kwa kumteua Mhe. Rashid Suleiman, Mhe. Rashid wakati nilipokuwa Waziri wa elimu ananiuliza maswali mengi

sana, siku moja nikamuombea Mungu *inshaallah* na yeye atakaa huku mbele. Sasa leo kafika karibu katika *cabinet*.

Lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wazazi wangu wawili, tarehe kama ya leo kwenye saa sita na dakika kama moja hivi, ndivyo alivyonambia mzazi wangu mama kwamba baba yako anakwenda msikitini nikakuzaa wewe. Kwa hivyo leo tarehe 24 ni tarehe muafaka, kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe kwamba wajuwe wanachangia hotuba ya kitoto kichanga hakitaki kubughudhiwabughudhiwa kidogo, isipokuwa kishauriwe zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama kamati ili lipokee, lijadili na hatimae liidhinishe makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujaalia kukutana hapa katika Baraza hili tukufu, tukiwa na afya njema na tukiendelea kushughulikia majukumu ya kitaifa katika hali ya amani na utulivu, hali hii ya amani na utulivu na maelewano yaliyopo ni nyenzo muhimu na tunapaswa kuitunza kwa maslahi ya vizazi vyetu na taifa kwa ujumla kama ambavyo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohd Shein akihusia kila mara anapozungumza na wananchi.

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako tukufu napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru na kumpongeza Dr. Ali Mohd Shein kwa uongozi wake mzuri na makini katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar, hapana shaka wananchi wa Zanzibar wanaendelea kuwa na imani na uongozi wake, ambao kwa kweli umetoa matumaini katika kipindi hiki kifupi tangu aliposhika madaraka. Mhe. Spika, Wizara inaunga mkono juhudi zake za kuwaletea wananchi wa Zanzibar.

www.kazi.go.tz

Aidha mimi pamoja na watendaji wangu tumeupokea kwa dhati wito wake wa kutaka watendaji wa serikali tubadilike na tunaahidi kutekeleza ipasavyo majukumu yetu na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Mhe. Spika, natoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa umakini na muono wake juu ya suala la maendeleo kwa wananchi, hekima zake pamoja na ahadi zake alizotoa wakati wa kampeni ya uchaguzi ya mwaka 2010 iliyopelekea kwa makusudi kuunda wizara hii ya kusimamia masuala ya kazi uwezeshaji wananchi kiuchumi na ushirika. Mhe. Rais aliwaahidi wananchi wa Zanzibar katika uongozi wake katika juhudi ya kuwatafutia ufumbuzi, matatizo ya umaskini na ajira kwa vijana. Hivyo wizara ya kazi uwezeshaji wananchi kiuchumi na ushirika imeundwa ili kutimiza ahadi hiyo ya kukidhi matakwa ya wananchi katika masuala hayo makuu.

Aidha, katika kutimiza azma hii, wizara yangu imeandaa mipango na mikakati mbali mbali, ikiwemo Programu ya Kazi Nje Nje; Programu ya Ajira kwa Vijana; kujenga utamaduni na uwezo wa ujasiriamali, ili wananchi wa makundi mbali mbali waweze kujiajiri na kunyanyua kipato chao; na kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ili kufikia kazi za staha na zenye tija. Pia wizara yangu inafanya juhudi kubwa ya kuviimarisha vyama vya ushirika vya uzalishaji mali na utoaji huduma, ili vifanye kazi kwa ubunifu, vihimili ushindani wa kibiashara, na viweze

kukidhi matarajio ya wanachama wake ya kuwanyanyua kiuchumi. Katika kufanikisha haya, Wizara inafanya kazi kwa karibu sana na taasisi nyengine za Serikali, Mashirika ya Kimataifa, sekta binafsi na Jumuia za Kiraia.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa kumshauri na kumsaidia kwa karibu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kukupongeza wewe Mhe. Spika kwa umahiri wako katika kuliongoza Baraza hili tukufu. Uzoefu, hikma na umakini ulionao katika kuliendesha Baraza hili, umesaidia sana kuliwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi, ikiwemo kuishauri serikali juu ya masuala mbali mbali yenye maslahi kwa taifa.

Mhe. Spika, napenda kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza lako tukufu inayoongozwa na Mhe. Asha Bakari Makame kwa mashirikiano wanayoyatoa kwa wizara yangu. Miongozo na ushauri wao umetuwezesha kubaini na kushughulikia changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli zetu. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, kwa miongozo na michango wanayoitoa kwa wizara yangu. Naithamini sana michango yao, kwani nayo pia imetusaidia kujiimarisha kiutendaji katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wafanyakazi wa wizara yangu, tunatoa pole kwa kuondokewa na Wajumbe wawili wa Baraza lako Tukufu, Mhe. Mussa Khamis Silima aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, na Mhe. Salum Amour Mtondoo aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azipe subra familia zao, na aziweke roho za marehemu hao mahala pema peponi, Amin. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mohammedraza kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, na Mhe. Marina Joel kwa kuchaguliwa kupitia uteuzi wa Mhe. Rais.

MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, Hotuba hii ya bajeti ya wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2012/2013 imezingatia na kulenga utekelezaji wa shughuli zitakazochangia ufikiaji wa malengo ya mipango na mikakati mikuu ya maendeleo ya kitaifa, ambayo ni Dira ya Maendeleo ya 2020 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar kwa mwaka 2010 - 2015 (MKUZA II). Bajeti hii pia imezingatia Malengo ya Milenia 2015, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015, Sera husika za kisekta na Mpango Mkakati wa Wizara. Aidha, imezingatia maelekezo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein katika hotuba zake mbali mbali, na yale aliyoyatoa wakati wa mikutano yake ya kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Pia imezingatia maoni ya washirika mbali mbali

wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa ujumla, malengo yaliyoainishwa katika bajeti hii yamejikita katika kuweka mazingira mazuri ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, kuongeza fursa za ajira hususan kwa vijana na kuweka mazingira bora ya kazi, ili kupunguza umasikini na kuleta maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, kabla ya kuandaa Mpango Kazi kwa mwaka 2012/2013, wizara ilitathmini utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ili pamoja na mambo mengine, kubaini changamoto zilizopo kuhusiana na masuala ya kazi, uwezeshaji wananchi kiuchumi na ushirika. Hivyo, imelazimika kufanya mapitio ya malengo, ili kuweza kushughulikia changamoto zilizojitokeza, ikiwemo suala zima la ajira kwa vijana. Katika mnasaba huo, Wizara kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 imejipangia kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

1. Kuongeza upatikanaji wa kazi za staha na zenye tija kwa wote, hususan vijana (wanawake na wanaume);
2. Kuongeza na kutanua programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
3. Kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa sheria za kazi;
4. Kuimarisha uhusiano kazini na utekelezaji wa viwango vya kazi;

5. Kuimarisha hali ya usalama na afya katika sehemu za kazi;
6. Kuimarisha uandaaji, utekelezaji na uratibu wa sera, mipango na programu za Wizara; na
7. Kuimarisha uwezo wa watendaji na mazingira ya kazi ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba uniruhusu nitoe muhtasari wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012, na baadae kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa malengo ambayo Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ilijipangia katika mwaka wa fedha uliopita wa 2011/2012 na malengo ambayo imekusudia kuyatekeleza kwa mwaka 2012/2013.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, wizara yangu katika mwaka wa fedha 2011/2012, ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Sitini na Nane na Laki Tano (Shs. 68,500,000/=) kutokana na vyanzo vya mapato vifuatavyo:

i) Vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni;

ii) Ukaguzi wa mikataba ya kazi;
iii) Usajili wa vyama vya ushirika; na
iv) Huduma za ukaguzi wa vyama vya ushirika.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Ishirini na Tatu, Laki Mbili Sabini na Sita Elfu, Mia Tisa Sabini na Tano (T. Shs. 123,276,975/=) zimekusanywa, sawa na asilimia 180 na kuvuka lengo, maelezo zaidi (*Angalia **Kiambatanisho Nam. 1** kwa ufafanuzi zaidi).*

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara yangu ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Arobaini na Tano (T. Shs. 1,545,000,000) kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo, Shilingi Milioni Mia Nne Sitini na Tano (Shs. 465,000,000) zilitengwa kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho za wafanyakazi na zilizobaki, Shilingi Bilioni Moja na Milioni Thamanini (Shs. 1,080,000,000) zilitengwa kwa matumizi mengineyo. Jumla ya Shilingi Milioni Tisini (Shs. 90,000,000) zilitengwa kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, Wizara imeingiziwa jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Thelathini na Tisa, Thelathini na Saba Elfu, Mia Saba Arobaini na Tisa (T. Shs. 1,939,037,749/=) kwa matumizi ya kawaida. Kati ya hizo, Shilingi Milioni Mia Tisa Arobaini na Sita, Laki Tisa Elfu Mbili, Mia Tisa Thamanini na Tano (T. Shs. 946, 902,985/=) ni kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho za wafanyakazi; Shilingi Milioni Mia Nane Sabini na Mbili, Laki Tisa Sabini na Nne Elfu (T.Shs. 872,974,000/=) kwa matumizi mengineyo yasiyokuwa mishahara ambayo ni sawa na asilimia 90 ya fedha zilizotengwa; na Shilingi Milioni Mia Moja Kumi na Tisa, Laki Moja Sitini, Mia Saba Sitini na Nne (T.Shs.119,160,764/=) ni kwa ajili ya ruzuku kwa Idara ya Mikopo. Fedha zilizopatikana kwa kazi za maendeleo hadi kufikia kipindi hicho ni Shilingi Milioni Sabini (T. Shs. 70,000,000/=), sawa na asilimia 78 ya fedha zilizotengwa kwa mwaka 2011/2012.

41

Kiambatanisho Nam. 2 kinatoa ufafanuzi zaidi kuhusu fedha zilizotengwa na kutolewa kwa matumizi ya Wizara hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Juni 2012.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2011/2012 NA MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, kimuundo wizara hii ina Kamisheni moja, Idara saba na Ofisi Kuu ya Pemba kama ifuatavyo:

1. Kamisheni ya Kazi;
2. Idara ya Ajira;
3. Idara ya Usalama na Afya Kazini;
4. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

5. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
6. Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
7. Idara ya Ushirika;
8. Idara ya Mikopo; na
9. Ofisi Kuu Pemba.

Utekelezaji wa malengo kwa mwaka 2011/2012 na malengo kwa mwaka 2012/2013 kwa kila idara ni kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya Wizara;

2. Kuandaa miradi na programu mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza sera na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar;

3. Kuimarisha mfumo wa uratibu, tathmini na ufuatiliaji wa shughuli za Wizara;

4. Kuratibu utayarishaji wa Sera na tafiti kuhusiana na masuala mbalimbali kulingana na majukumu ya Wizara; na

5. Kuhakikisha masuala mtambuka yanazingatiwa katika shughuli za Wizara.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, wizara imekuwa ikiratibu na kutekeleza miradi na programu zifuatazo:

Programu ya Kazi Nje Nje: Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) imeanza kutekeleza Programu ya Kazi Nje Nje. Programu hiyo iliyoanza kutekelezwa rasmi mwezi Machi, 2011 inalenga kuwawezesha vijana kuwa na muamko wa kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea ajira za kuajiriwa. Jumla ya vijana 32 wamepatiwa mafunzo juu ya ujasiriamali na kubadili tabia kwa lengo la kujiajiri. Vijana hao tayari wamesambazwa katika wilaya zote za Unguja na Pemba, wafanye kazi ya kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa vijana wenzao, ili wawe na muamko wa kujiajiri. Kila mmoja kati ya vijana hao anatarajiwa kutoa mafunzo kwa vijana wengine 200. Watafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na Kamati za Uzalishaji Ajira na Uwezeshaji kwa kila Wilaya.

Mradi wa Kupambana na Ajira za Watoto: Mhe. Spika, kwa kushirikiana na *"Save the Children Fund"* wizara pia imeanza kutekeleza Mradi wa Kupambana na Ajira mbaya za Watoto. Mradi huo ulioanza kutekelezwa mwezi wa Machi 2012, lengo lake ni kuwanusuru watoto 5,000 katika wilaya tisa za Unguja na Pemba dhidi ya ajira za watoto na kuzijengea uwezo wa kiuchumi familia za watoto hao ili ziweze kujikimu kimaisha. Hii itasaidia watoto hao kuepukana na madhara ya ajira mbaya za watoto, ikiwemo kukosa elimu. Mradi huu umetekeleza shughuli kuu zifuatazo:

- Kamati ya Kisekta yenye wajumbe 20 kwa ajili ya kushughulikia masuala ya ajira za watoto imeundwa. Kamati hiyo ina wajumbe kutoka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto; Jumuia ya Waajiri; Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi; na taasisi za kiraia (*TAMWA, COWPZ, PIRO na KUHAWA*). Kamati hiyo imefanya vikao viwili ambavyo vimejadili masuala mbali mbali yaliyowasilishwa kuhusiana na mradi huo.
- Vitendea kazi muhimu kwa uendeshaji wa mradi vimeandaliwa ikiwemo viwango na taratibu za ufuatiliaji wa masuala ya ajira za watoto; miongozo ya kubainisha watoto walio katika ajira na walio katika hali ngumu; na orodha ya kazi hatarishi kwa watoto.
- Taasisi za kiraia zinazoshiriki katika utekelezaji wa mpango huu, zimefanya mikutano ya uhamasishaji juu ya masuala ya ajira za watoto katika Wilaya zote za Mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja, na katika Wilaya zote za Pemba.

43

Mradi wa kuimarisha Utekelezaji wa Sheria za Kazi (Labour Laws Compliance Project): Kupitia mradi huu ambao umekuwa ukitekelezwa kwa mashirikiano na *ILO* na *"United States Department of Labour"*, wizara, pamoja na mambo mengine, imeweza kukiimarisha Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi, na pia kuwapatia mafunzo Maafisa Ukaguzi Kazi na Maafisa Ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini juu ya mbinu bora za ukaguzi. Mradi huu umemaliza muda wake mwishoni mwa mwezi wa Mei ,2012.

Mhe. Spika, idara imetoa mafunzo ya kuandaa Mpango Kazi kwa watendaji 16 wa wizara ambayo yamelenga katika kuandaa mipango yenye kuleta matokeo yanayotarajiwa. Watendaji hao wameanza kuyatumia mafunzo hayo katika uandaaji wa mipango mbali mbali ya wizara, ikiwemo Mpango wa Matumizi kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, ili kujenga msingi imara wa kuwawezesha wananchi kiuchumi, Wizara imeanza maandalizi ya Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kamati ya wataalamu inayojumuisha sekta mbali mbali (ikiwemo kilimo, uvuvi, biashara na utalii) imeundwa na imepewa jukumu la kukusanya taarifa za awali zinazohitajika kwa maandalizi ya sera hiyo. Hadidu rejea za Mtaalamu wa kuongoza mchakato wa kuandaa sera nazo zimeandaliwa na kupitishwa kwenye kamati ya Wataalamu. Mazungumzo na *ILO* yameshafanyika ili kumpatia Mtaalamu elekezi

ambaye atafanya kazi na wataalamu wa ndani katika kuandaa sera hiyo. Hatua za kupatikana mtaalamu huyo zimeanza na anatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni.

Mhe. Spika, wizara imeanza hatua ya kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa mashirikiano ya Shirika la Kazi Duniani, mtaalamu kwa ajili ya kazi hiyo tayari amepatikana na ameanza kufanya kazi hiyo. Kazi za uandaaji mfumo huo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti, 2012.

Mhe. Spika, Moja ya mikakati muhimu katika kuwawezesha wananchi kiuchumi ni suala zima la kuimarisha sekta ya ushirika. Katika kufanikisha hilo, tayari wizara imekamilisha maandalizi ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika. Rasimu ya sera hiyo, ambayo maandalizi yake yalihusisha washirika mbali mbali wa masuala ya ushirika, itawasilishwa kwenye vyombo husika kwa kuthibitishwa muda mfupi ujao. Kuwepo kwa sera hiyo kutasaidia kutoa muongozo juu ya mikakati inayopaswa kuchukuliwa pamoja na majukumu ya wahusika mbali mbali katika kuimarisha sekta ya ushirika.

Mhe. Spika, Wizara imefanya tafiti katika maeneo muhimu ya kiuchumi ili kubaini fursa zilizopo na mahitaji ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Taarifa zinazotokana na tafiti hizi zitasaidia katika kuandaa mipango ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kuzingatia rasilimali na fursa walizonazo katika maeneo yao. Taarifa hizo pia zitatumika katika kubuni mpango wa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo wadogo yatayosaidia kukuza na kuimarisha biashara zao, ili ziweze kuwa na tija zaidi na kuwapatia kipato endelevu.

Mhe. Spika, wizara yangu pia imelipa kipaumbele suala zima la uhusishaji wa masuala mtambuka katika shughuli zake za kila siku. Masuala hayo ni pamoja na utawala bora; mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya; uwiano wa jinsia; uhifadhi wa mazingira; na uzingatiaji wa makundi ya watu wenye mahitaji maalum, wakiwemo watu wenye ulemavu. Kamati ya kuratibu uingizaji wa masuala mtambuka kwenye sera, mipango na shughuli za kila siku za Wizara imeundwa na imepatiwa hadidu rejea zitazosaidia kuweka utaratibu mzuri wa kuendesha shughuli zake. Pia, kwa kushirikiana na taasisi husika, Wajumbe wa kamati hiyo wamepatiwa mafunzo juu ya namna ya kuzingatia na kuingiza masuala mtambuka katika sera, mipango na programu za wizara pamoja na kuchambua na kuandaa ripoti zinazozingatia masuala hayo.

Malengo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Wizara;
2. Kuimarisha uratibu na upangaji wa programu za Wizara;

3. Kuimarisha uwezo wa Wizara katika kufanya tafiti;
4. Kuimarisha mazingira ya kisera na kisheria kwa utekelezaji wa masuala ya usalama na afya kazini na uwezeshaji wananchi kiuchumi;
5. Kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara na wahusika wengine; na
6. Kuingiza masuala mtambuka katika sera, programu na mipango ya Wizara.

Mhe. Spika, ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira, wizara imeandaa Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana. Utekelezaji wa programu hii, ambao utaanza kwenye mwaka huu wa fedha wa 2012/2013 utahusisha pia wizara zinazoshughulikia masuala ya Vijana; Utalii; Mifugo na Uvuvi; na Ofisi ya Rais inayoshughulikia Tawala za Mikoa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa kupitia Programu hii ni pamoja na:

1. Kurasimisha sekta isiyo rasmi ya usafiri wa umma ili kuwawezesha vijana walioajiriwa katika sekta hiyo kuwa na ajira za uhakika zenye mikataba inayoendana na Sheria za Kazi;
2. Kuanzisha vituo vya kulelea wajasiriamali (*business incubators*);
3. Kujenga uwezo wa *SACCOS Bank* 16 ili ziweze kutoa huduma endelevu za kifedha kwa vikundi vya kiuchumi vinavyoendeshwa na vijana;
4. Kutoa mafunzo kwa vijana watembezaji watalii juu ya historia ya Zanzibar na taratibu za biashara ya utembezaji watalii, ili hatimaye waweze kufanya kazi hii kwa umahiri zaidi kupitia vyama vya ushirika;
5. Kutoa mafunzo maalum katika fani ya huduma na uongozi wa hoteli, na baadae kuwasaidia kupata ajira angalau vijana 30 waliohitimu katika fani tofauti kwenye vyuo mbali mbali.

6. Kununua boti mbili na vifaa vyake kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, pamoja na kuwapatia mafunzo vijana kuhusu uvuvi wa bahari kuu ili waweze kujiajiri;

7. Kuanzisha na kuendeleza skuli shamba 8 ili kuwapatia mafunzo vijana juu ya ufugaji bora wa mbuzi na ngombe wa maziwa pamoja na kuku;
8. Kujenga masilabi kumi kwa ajili ya mradi wa kukusanya taka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi utakaoshirikisha vijana; na

9. Kusaidia uanzishaji na uendelezaji wa mashamba ya kilimo cha maua (*Rosella*), kwa vikundi vya vijana Unguja na Pemba.

Serikali imetenga jumla ya Shilingi Bilioni Moja na Milioni Mia Moja (1,100,000,000/=) kwa utekelezaji wa mradi huu. Jumla ya vijana 950 wanatarajiwa kupata ajira kupitia Programu hii kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi na Saba (T.Shs.117,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, na Shilingi Bilioni moja na Milioni mia moja kwa kazi za maendeleo (T.Shs 1,100,000,000/=).

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilipangiwa kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kujenga uwezo wa utendaji kwa kusimamia upatikanaji wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi kulingana na kazi wanazozifanya;

2. Kuimarisha na kujenga mazingira mazuri ya kazi;

3. Kukiimarisha Kitengo cha Habari na Mawasiliano ili kiweze kutekeleza vyema majukumu yake;

4. Kusimamia maslahi ya wafanyakazi na mahusiano mema kazini; na

5. Kuratibu na kusimamia kitengo cha Ofisi ya Waziri kwa kuendeleza na kuimarisha mahusiano na mashirikiano ndani na nje ya nchi.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo iliyojiwekea, idara imetekeleza yafuatayo:

- Imetoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi 55 (wanawake 28 na wanaume 27) kuhusiana na sheria na kanuni za utumishi wa umma. Mafunzo hayo yalihusisha wafanyakazi wa kada ya madereva, wahudumu, walinzi, na watunzaji masjala. Pia mafunzo yamefanyika kwa watendaji 30 (wanawake 16 na wanaume 14) wa Wizara kuhusu utendaji kazi kwa lengo la kuleta ufanisi na matokeo yanayotarajiwa. Mafunzo haya pia yalilenga katika kujenga tabia ya kufanya kazi kwa pamoja na kuinua ari ya kujituma na kupenda kazi. Kufuatia mafunzo hayo, Kamati Maalum imeundwa kufuatilia hali ya utendaji kazi kwa kuzingatia mafunzo yaliyotolewa.

- Mafunzo ya sheria na kanuni za fedha na manunuzi serikalini yamefanywa kwa Wakuu wa Idara na watendaji wa kitengo cha fedha na manunuzi. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uelewa juu ya sheria na kanuni hizo ili kuleta ufanisi katika majukumu yao ya kazi.

- Idara pia imegharamia mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 11 (wanawake 6 na wanaume 5) katika fani za utunzaji kumbukumbu, ukatibu muhtasi, ukaguzi wa hesabu, uhasibu, lugha ya Kiingereza na udereva. Pia wafanyakazi wanne wamepatiwa mafunzo mafupi nchini China katika fani za usimamizi wa rasilimali watu; uongozi; wanawake na ujasiriamali; na uchumi na sera. Vilevile, mfanyakazi mmoja amepatiwa mafunzo ya uendeshaji na utumishi yaliyoandaliwa na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. *(Angalia **Kiambatanisho Nam.3** kwa ufafanuzi zaidi).*

- Vile vile, idara imelipia gharama za masomo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 8 (wanawake 2 na wanaume 6); kati ya hao mmoja amemamaliza masomo katika fani ya Usalama na Afya kazini, na 7 wanaendelea na masomo katika fani za Uhasibu, Ushirika, Mipango, Uongozi wa Rasilimali Watu na Sheria. *(Angalia **Kiambatanisho Nam. 4** kwa ufafanuzi zaidi).* Aidha, mfanyakazi mmoja mwanamke anaendelea na masomo ya shahada ya pili nchini Korea, katika fani ya Mipango ya Maendeleo ya Wanawake kwa msaada wa Serikali ya nchi hiyo.

- Katika kuwataarifu wananchi kuhusu shughuli mbali mbali zilizotekelezwa na Wizara, Kitengo cha Mawasiliano cha Wizara kimemudu kutoa jumla ya taarifa 56 kupitia televisheni ya Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*), 63 katika redio, 43 katika gazeti la Zanzibar Leo na 5 kupitia "*Zanzibar Cable TV*".

- Ili kuimarisha masuala ya afya na usalama kazini, wizara imesimamia zoezi la kupima koo, pua, masikio, sukari, uzito na shindikizo la damu kwa wafanyakazi wake. Kwa wale ambao walionekana wana matatizo walishauriwa kwenda hospitali kwa matibabu zaidi. Zoezi hilo lilihusisha na mafunzo kwa wafanyakazi juu ya namna ya kujikinga na maradhi hayo. Aidha, mafunzo ya matumizi ya vifaa vya kuzimia moto na huduma ya kwanza yametolewa kwa wafanyakazi.

Ofisi ya Waziri

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Ofisi ya Waziri imepokea wageni kutoka taasisi, jumuia na mashirika mbali mbali ya ndani na nje ya nchi, kwa lengo la kujenga mahusiano na kubadilishana mawazo. Miongoni mwa wageni waliofika katika Ofisi ya Waziri ni pamoja na Mkurugenzi wa *ILO* kwa Kanda ya Tanzania, Kenya, Rwanda na Uganda; Ujumbe kutoka *ILO* – Geneva; Ujumbe wa Kampuni ya *"Ras-Al-Khaimah Gas Zanzibar Ltd* (*Rak Gas Zanzibar Ltd*)"; Ujumbe wa Kampuni zinazojishughulisha na uwakala binafsi wa ajira; Mtaalamu wa masuala ya ujasiriamali kutoka Rwanda; Jumuia ya Mazingira na Usafi (*ZASOSE*); Jumuia ya Wanamaji Wastaafu; Jumuia ya Wafanyabiashara; na Wawakilishi wa Chama cha Mabaharia, Chama cha Walinzi, Chama cha Walimu Zanzibar na Baraza la Taifa linaloshughulikia masuala ya watu

wenye ulemavu. Aidha, jumla ya wananchi 2,063 walifika ofisini kumuona Waziri kwa masuala mbalimbali.

Mhe. Spika, Ofisi ya Waziri pia imetembelewa na Mwakilishi wa Benki ya Dunia na Mabalozi Wadogo wa China, Oman na India waliopo Zanzibar, kwa ajili ya kuzungumzia maeneo ya ushirikiano katika shughuli zinazosimamiwa na wizara. Vile vile Ofisi iliratibu shughuli mbalimbali za kimaendeleo na kijamii ambazo Waziri alishiriki akiwa mgeni rasmi. Miongoni mwa shughuli hizo ni ufunguaji wa mafunzo ya Wataalamu wa Ushauri wa Biashara na Ujasiriamali; ufunguaji wa mafunzo ya siku moja ya ujasiriamali na uwezeshaji kiuchumi kwa wajasiriamali wa Jimbo la Kikwajuni; ufunguaji wa mafunzo ya wajasiriamali yaliyofanyika Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja; uwekaji wa jiwe la msingi la jengo la kuhifadhia zana za kilimo na Afisi ya Vyama vya Ushirika vya WEZA huko Tunduni; uwekaji wa jiwe la msingi la ghala huko Mkele Kibondeni; Mkutano Mkuu wa Afya *SACCOS*; Mkutano Mkuu wa UMAWA; mechi ya mpira wa miguu kati ya *Habari Sports Club* na wasanii kwa lengo la kuchangisha fedha kwa ajili ya waliopatwa na msiba uliotokana na ajali ya *MV Spice Islander*; na maonesho ya kazi za mikono zinazofanywa na vijana kutoka katika kituo cha kurekebisha tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya, yaliyoandaliwa na taasisi isiyo ya Serikali inayojulikana kama *"Zanzibar Drug Free"*.

Mhe. Spika, Ofisi ya Waziri pia imetimiza ahadi zilizotolewa za vifaa na fedha kwa Kamati ya Maendeleo ya Skuli ya Mbuyutende; Soko la Jumapili; Ushirika wa *Visiwani Jazz Band*; vikundi vya kijamii vikiwemo Kituo cha kurekebisha tabia kwa vijana walioathirika na utumiaji wa dawa za kulevya cha Wete; Kikundi cha Ushirika cha Maziwango'mbe Micheweni; Kikundi cha Hatuna Chuki cha Tunduni; na Vikundi vya Hakuna Geni, Imani Kazi, Ndio Mambo Yetu na Kumbe vya Uzi Ng'ambwa.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, pia Waziri alipata bahati ya kushiriki mikutano na kutembelea nchi mbali mbali kikazi, ikiwemo Brazil, Burkina Faso, China, Cuba, Oman, Ras-Al-Khaimah na Uswisi.

Malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 18 ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao;

2. Kuimarisha mazingira ya kazi;

3. Kuimarisha usalama wa majengo na mazingira yanayozunguka Wizara;

4. Kuimarisha kitengo cha Habari na Mawasiliano (*ICT Unit*) cha Wizara;

5. Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na manunuzi;

6. Kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ili kuelimisha na kujenga taswira nzuri kwa umma; na

7. Kusimamia upatikanaji wa haki na maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni mia tano ishirini na tano, laki tano na hamsini elfu (T.Shs.525,550,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA UENDELEZAJI NA URATIBU WA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 idara hii ilipanga kutekeleza yafuatayo:

1. Kufanya uchambuzi wa mahitaji ya uwezeshaji wananchi kiuchumi;

2. Kupanga na kuendesha mafunzo ya kuongeza ujuzi wa ujasiriamali;

3. Kutayarisha Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

4. Kuandaa na kuendesha Mikutano ya Kamati za Uwezeshaji za Wilaya na Taifa;

5. Kwa kushirikiana na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, kufanya tafiti katika maeneo muhimu ya kiuchumi ili kubaini fursa zilizopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi;

6. Kuandaa mafunzo kwa wafanyakazi ili waweze kupanga, kuratibu na kusimamia vyema programu za kuwawezesha wananchi kiuchumi; na

7. Kuandaa mapendekezo ya miradi ili kutafuta rasilimali fedha na misaada ya kitaalamu kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 idara imetekeleza yafuatayo:

1) Jumla ya wajasiriamali 94 (Unguja 64 na Pemba 30) wamepatiwa mafunzo juu ya usimamizi wa biashara, uwekaji wa kumbukumbu, utafutaji wa masoko, uandaaji wa

Mpango wa Biashara, na uanzishaji wa mtandao wa biashara ili kutanua soko. Mafunzo hayo yalisaidia kuwajengea uwezo na ari wajasiriamali na hata baadhi yao kuhamasika kushiriki katika mashindano ya Mama Shujaa wa Chakula wa Tanzania, na wengine katika maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi, kwa gharama zao wenyewe.

2) Idara kwa kushirikiana na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, imefanya utafiti katika maeneo muhimu ya kiuchumi ili kubaini fursa zilizopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Katika hatua ya awali, taarifa zinazohusu fursa za kuwawezesha wananchi kiuchumi katika sekta za Utalii, Kilimo na Mali Asili zimekusanywa kwa upande wa Unguja. Jumla ya hoteli 11 zimetembelewa na mazungumzo yamefanywa na uongozi wa hoteli hizo ili kujua mahitaji yao na namna gani wajasiriamali wazalishaji wanaweza kuunganishwa kupata soko kutokana na mahitaji ya hoteli hizo. Hoteli zilizotembelewa ni: *Ras Nungwi Beach Resort, Double Tree By Hilton, Zalu Beach Resort, La Gemma Dell' Est Plan Hotel, Mapenzi Beach Hotel, Dream of Zanzibar Plan, Ocean View Beach Hotel, My Blue Beach Hotel, Melia Beach Hotel, Sea View Beach Hotel na Bravo Hotel*.

3) Soko la Jumapili kwa wajasiriamali wazalishaji wadogo wadogo limeanzishwa ili waweze kuuza bidhaa zao. Hii imetokana na kilio chao cha muda mrefu kuhusiana na kukosa eneo la kufanyia biashara zao. Wajasiriamali wasiopungua 60 huwa wanapeleka bidhaa zao katika soko hilo liliopo Mwembekisonge Michenzani kila Jumapili. Kupitia soko hilo, wajasiriamali wamepata fursa ya kutanua soko la bidhaa zao, kwani wamekuwa wakipata fursa ya kufunzwa kwa vitendo juu ya mbinu bora za kuendesha biashara na kuvutia wateja. Naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu watembelee kwenye soko hilo wakanunue na kujionea wenyewe bidhaa mbali mbali zinazotengenezwa na wajasiriamali wetu kwa kutumia rasilimali zinazopatikana hapa hapa nchini.

4) Katika kunyanyua hamasa ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, Wizara yangu ilibuni mpango wa kuanzisha "Vijiji vya Mfano". Kwa kuanzia, vijiji vilivyoteuliwa ni Mbuyutende kilichopo Matemwe; Unguja, na Ungi kilichopo Msuka, Pemba. Katika hatua za awali, taarifa za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo tayari zimekusanywa. Taarifa hizo zitasaidia kubaini changamoto na fursa zilizopo katika maeneo hayo kuhusiana na masuala mbali mbali ya kiuchumi na kijamii, ikiwemo suala zima la ajira, ili hatimaye mpango maalum wa kuviwezesha kiuchumi uandaliwe. Wizara imepanga kushajihisha upatikanaji wa rasilimali kutoka kwa washirika mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo.

5) Ili kuimarisha uratibu wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi, Kamati maalum ya kisekta imeundwa, ambayo inajumuisha Makatibu Wakuu wa Wizara za Serikali zinazohusiana na masuala haya zikiwemo Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo; Biashara; Kilimo; Mifugo na Uvuvi; pamoja na wawakilishi kutoka taasisi za fedha na sekta binafsi. Kamati hii imekuwa ikikutana mara moja katika kila kipindi cha miezi mitatu, ili kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji na kutoa ushauri juu ya mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

6) Mfanyakazi mmoja wa idara amehudhuria mafunzo ya muda mfupi ya wiki mbili nchini Swaziland yanayohusu uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia ujasiriamali.

Mhe. Spika, suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi linagusa kila sekta. Katika mnasaba huo, Jumuia ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima nayo imekuwa ikichangia juhudi za serikali katika kuwawezesha wananchi kiuchumi. Jumuia hiyo kwa kushirikiana na *"Tanzania Private Sector Foundation"* imekuwa ikitekeleza programu inayojulikana kama "Fanikiwa Kibiashara" *(Business Development Gateway – BDG).* Program hiyo imegawika katika sehemu mbili kuu:

1) Mpango wa uhakiki wa uwezo wa kibiashara *(Business Diagnostic Program);* na

2) Mpango wa kushindanisha mipango ya biashara *(Business Plan Competition)*

Kupitia mpango wa uhakiki wa uwezo wa kibiashara, Jumuia ya Wafanyabiashara imekuwa ikitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali waliowasilisha mawazo mazuri ya biashara. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya wajasiriamali 220 waliwasilisha mawazo mazuri ya biashara, ambapo kati yao 199 ndio waliofaulu katika hatua zote za masomo ya ujasiriamali na kupatiwa ruzuku ya jumla ya Shilingi Milioni Mia Sita Ishirini na Saba (Shs. 627,000,000/=) kwa kuendeleza biashara zao. Aidha, kupitia mpango wa kushindanisha mipango ya biashara, jumla ya wajasiriamali 40 waliwasilisha mipango yao ambayo ilishindanishwa na ile ya wajasiriamali kutoka Mikoa mingine ya Tanzania. Kati ya hao ni wajasiriamali 14 ndio waliofanya vizuri na walipewa jumla ya Shilingi Milioni Sabiini (Shs. 70,000,000/=) kama ruzuku kwa kuendeleza biashara zao. Nachukua fursa hii kuipongeza Jumuia ya Wafanyabiashara kwa juhudi zake hizo za kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati, kwa lengo la kuimarisha biashara zao na kuwaongezea kipato. Ni matumaini yangu wataendelea kushirikiana nasi ili tuweze kuwawezesha kiuchumi wananchi walio wengi zaidi.

Malengo ya Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kujenga utamaduni wa ujasiriamali na kuimarisha uwezo wa wajasiriamali, hususan vijana, katika wilaya 10 za Zanzibar;

2. Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini shirikishi ya shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;

3. Kutanua soko la bidhaa za wajasiriamali wadogo wadogo;

4. Kuijengea uwezo wa kiutendaji Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi (Shs. 110,000,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MIKOPO

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2011/2012, idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuratibu na kutoa mikopo ipatayo 1,000 (kutegemeana na upatikanaji wa fedha) kwa mwaka kwa kuzingatia ukuaji wa ajira kwa makundi yote;

2. Kusimamia na kufuatilia marejesho ya mikopo kwa wakati uliopangwa ili kwenda sambamba na malengo ya mikopo ya uwezeshaji kwa kukuza ajira nchini;

3. Kuanzisha maeneo mapya ya ukopaji, kuhakikisha taratibu za mikopo zinakuwa bora zaidi, mikopo inatolewa kwa wakati na kushirikiana na asasi nyengine katika kuimarisha huduma kwa wakopaji;

4. Kutunisha Mfuko wa Uwezeshaji kwa kuhamasisha wenye uwezo kuchangia ili kuongeza utoaji wa mikopo ya kuwawezesha wananchi kiuchumi;

5. Kuimarisha utendaji kazi wa Idara kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi, na kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi ili kuongeza ufanisi; na

6. Kuendeleza mashirikiano na taasisi za kitaifa na kimataifa katika kuwaimarisha walengwa, pamoja na kuangalia namna bora za kuongeza uwezo wa kifedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mikopo

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 idara imetekeleza shughuli zifuatazo:

1) Imetoa mikopo 195 (Unguja 130 na Pemba 65) yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Moja Arobaini na Tatu na Laki Tano (Shs. 143,500,000/=) kupitia Mfuko wa Kujitegemea Unguja na Pemba *(Angalia **Kiambatanisho Nam. 5** kwa ufafanuzi zaidi).*

2) Imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa JK/AK ambao unasimamiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar. Kupitia Mfuko huu, jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Ishirini na Tisa, Laki Nane na Elfu Themanini na Nne, Mia Nane Thelathini na Moja (Shs. 1,529,884,831/=) zimetolewa hadi kufikia mwezi Mei 2011. Kati ya hizo, Unguja zimetolewa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Hamsini na Tisa, Laki Moja na Elfu Sitini na Nne, Mia Nane Thelathini na Moja (Shs. 1,059,164,831/=) na Pemba Shilingi Milioni Mia Nne Sabini, Laki Saba na Elfu Ishirini (Shs 470,720,000/=). Ufafanuzi zaidi unaonekana katika **Kiambatanisho Nam.6.**

3) Imefanya ziara katika Wilaya zote za Unguja na Pemba kwa lengo la kukutana na Masheha na wakopaji ili kuhimiza urejeshwaji wa fedha za mkopo. Hadi kufikia mwezi Juni 2012, jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Ishirini na Mbili, Laki Tano na Elfu Nne, Mia Tatu Sitini na Nne (T.shs 122,504,364/=) zimerejeshwa katika Mfuko wa Kujitegemea Unguja na Pemba *(Angalia **Kiambatanisho Nam. 7).*** Kwa upande wa Mfuko wa JK/AK, jumla ya Shilingi Milioni Themanini na Mbili, Laki Sita na Sitini na Nne Elfu, Mia Tano Sabini na Tisa (T.shs. 82,664,579/=) zimerejeshwa *(Angalia **Kiambatanisho Nam.6)***. Hata hivyo, bado kuna changamoto katika urejeshaji wa fedha za mkopo, hasa kwa upande wa Mfuko wa JK/AK, hivyo kupelekea utoaji wa mikopo kupitia mfuko huo kutokwenda kwa kasi inayotarajiwa. Kwa mujibu wa taarifa kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar, ambayo ndiyo inayosimamia Mfuko wa JK/AK, jumla ya mikopo 80 (Unguja 38 na Pemba 42) yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Moja na Moja, Laki Saba Elfu Ishirini, Mia Tano na Sabini na Tatu (Tshs. 101,720,573/=) haijalipwa.

4) Idara imepitia taratibu za utoaji na urejeshwaji mikopo na kufanya marekebisho pale ilipostahiki, kulingana na mapungufu yaliyobainika. Mikutano na viongozi wa Wilaya, Masheha na Wajumbe wa Kamati za Uwezeshaji za Wilaya ilifanywa ili

kuwafahamisha juu ya utaratibu mpya wa mikopo na majukumu yao katika suala zima la utoaji na ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo. Madhumuni ya kufanya yote hayo ni kuimarisha usimamizi wa mifuko ya mikopo pamoja na kuhakikisha kuwa mikopo inatolewa na kurejeshwa kwa wakati.

5) Ili kutunisha Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, Kamati Maalum imeundwa na kuzinduliwa na Mhe, Rais Dkt. Ali Mohamed Shein. Kamati hiyo imeanza kazi zake na Mfuko umeshaanza kuchangiwa. Hadi hivi sasa jumla ya Shilingi Milioni Mia sita (Tshs.600,000,000/=) zimekusanywa na shughuli ya uchangiaji zinaendelea.

6) Mfanyakazi mmoja mwanamke amegharamiwa kuchukua mafunzo ya muda mrefu katika fani ya uhasibu, ngazi ya ‘‘*Post Graduate Diploma*’’ Chuo cha Fedha (IFM) Dar es Salaam. Pia mfanyakazi mmoja mwanamme amegharamiwa kufanya mafunzo ya muda mfupi katika ngazi ya cheti, fani ya rasilimali watu katika matawi ya *DAR COLLEGE* yalioko Pemba.

MALENGO YA IDARA YA MIKOPO KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2012/2013, idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kutoa mikopo 1,000 kwa vikundi vya kiuchumi na watu binafsi/mjasiriamali mmoja mmoja;

2. Kuongeza kiwango cha marejesho ya mikopo kutoka asilimia 85 hadi asilimia 95;

3. Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za mikopo ;

4. Kuimarisha mashirikiano na mitandao na washirika wengine wanaojishughulisha na utoaji wa mikopo midogo midogo;

5. Kuanzisha fursa mpya za mikopo na kuimarisha miongozo ya usimamiaji mikopo;

6. Kuimarisha uwezo wa watendaji ili kuongeza ufanisi wa kazi;

7. Kuimarisha mazingira ya kazi; na

8. Kusimamia upatikanaji wa haki na maslahi ya wafanyakazi wa Idara.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mikopo iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi Milioni Mia Mbili na Thamanini na Nane (Shs. 288,000,000/=) kwa matumizi ya kawaida ikiwemo na mishahara.

IDARA YA USHIRIKA

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara ya Ushirika ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuanzisha nafasi 3,500 za ajira kupitia sekta ya ushirika;

2. Kukamilisha taratibu za kuidhinisha Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Sheria, kanuni na sheria ndogo ndogo za vyama vya ushirika;

3. Kusimamia usajili wa vyama vya Ushirika 175;

4. Kukagua mahesabu ya vyama vya Ushirika 150 na kuanzisha taasisi ya ukaguzi inayojitegemea;

5. Kufuatilia na kuvipatia ushauri wa kitaalamu vyama vya ushirika 2,000;

6. Kutoa mafunzo kwa wanachama na viongozi 3,000, kutoka vyama vya ushirika 400;

7. Kuanzisha "*SACCOS Banks*" 14 na kuimarisha zilizopo; na

8. Kuendeleza mashirikiano na taasisi mbali mbali ili kusukuma maendeleo ya sekta ya ushirika.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Ushirika

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012**,** mambo yafuatayo yametekelezwa kupitia Idara hii:

1) Vijana 3,854 (wanawake 2,505 na wanaume 1,349) wameshajihishwa kuanzisha miradi ya kiuchumi kupitia vyama vya ushirika kwenye Wilaya zote Unguja na Pemba. Kutokana na ushajihishaji huo, jumla ya vikundi 327 vimesajiliwa kuwa vyama vya ushirika. Sehemu kubwa ya wanachama wa vikundi hivyo ni vijana.

2) Uhakiki umefanywa kwenye vyama vya ushirika, kwa lengo la kukusanya taarifa juu ya idadi ya watu walioajiriwa, ili kupata kigezo cha kupima ongezeko la ajira kupitia sekta hiyo. Uhakiki umeonesha vijana 1,009 kwa Unguja wamepata ajira kupitia vyama vya ushirika, ambapo kati yao 18 wameajiriwa moja kwa moja kwenye vyama, 792 wamejiajiri wenyewe kupitia miradi yao iliyowezeshwa na vyama, na 199 wameajiriwa na watu walioanzisha miradi iliyowezeshwa na vyama. Kwa upande wa Pemba, uhakiki umeonesha vijana 62 wamejiajiri kupitia miradi iliyowezeshwa na vyama vya ushirika. Taarifa hizo zinatokana na uhakiki

uliofanywa kwa vyama vya ushirika katika Wilaya za Mjini na Magharibi Unguja, na Chake Chake na Mkoani kwa Pemba. Uhakiki unaendelea ili kukusanya taarifa hizo kwa Wilaya zilizobakia.

3) Jumla ya vikundi 426 (172 Unguja na 254 Pemba) vilivyoomba usajili, vimepatiwa taaluma ya mwanzo juu ya dhana, misingi na taratibu za ushirika. Pia vikundi hivyo vimewezeshwa kuandaa sheria ndogo ndogo, kuchagua uongozi wa awali na kufanya uchambuzi shirikishi wa kiuchumi wa shughuli wanazoziombea usajili. Vyama hivyo vyote tayari vimesajiliwa kuwa vyama vya ushirika, ambapo kati ya hivyo 21 (18 Unguja na 3 Pemba) ni *SACCOS* na 405 (154 Unguja na 251 Pemba) ni vya uzalishaji mali.

4) Vyama 52, zikiwemo *SACCOS* 38 na vyama 14 vya uzalishaji Unguja na Pemba vimefanyiwa ukaguzi wa mahesabu yao kwa kushirikiana na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.

5) Jumla ya watendaji 15 walipatiwa mafunzo ya ukaguzi wa mahesabu ya vyama vya ushirika, ambapo kati yao watano (5) wametoka Kitengo cha Ukaguzi ndani ya Idara, na 10 kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza ufanisi katika ukaguzi wa mahesabu ya vyama vya ushirika.

6) Ili kutathmini hali ya uendeshaji wa vyama vya ushirika, Idara iliendesha zoezi la kuvihakiki katika wilaya zote 10 za Unguja na Pemba. Matokeo ya awali yameonesha idadi ya vyama hai ni 1,651 (Unguja 1,066 na Pemba 585), sawa na asilimia 30 ya idadi ya vyama 5,503 (Unguja 3,485 na Pemba 2,018) vilivyosajiliwa katika daftari la usajili. Hali hii inaonesha kwamba vyama vingi vilivyosajiliwa vimekufa au havifanyi kazi, hasa kwa vile wakati wa uhakiki havikuonekana kabisa. Hata hivyo taarifa zinazotokana na uhakiki huu zitaisaidia Wizara kujipanga katika kuviimarisha vyama vya ushirika vilivyoonekana kuwa hai.

7) Mafunzo ya uongozi yametolewa kwa viongozi 578 (wanawake 342 na wanaume 236) kutoka vyama 389 Unguja na Pemba. Pia mafunzo kuhusu dhana ya ushirika, haki na wajibu wa wanachama, yametolewa kwa wanachama 3,385 (wanawake 2,362 na wanaume 1,023) kutoka vyama 142. Lengo la mafunzo yaliyotolewa, ni kuwajengea uwezo viongozi na wanachama waweze kuviendesha vyama vyao vya ushirika kwa ufanisi zaidi.

8) Juhudi za kuanzisha na kuimarisha *SACCOS Bank* ili kuongeza fursa za huduma za kifedha kwa vyama vya ushirika zimeendelezwa. Upembuzi wa kiuchumi wa kutathmini uwezekano wa kuanzisha *SACCOS Bank* umefanywa kwenye maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Matokeo yameonesha kuna uwezekano wa

kuanzisha *SACCOS Bank* katika maeneo matano, ambayo ni Donge, Amani, Muyuni na Kizimkazi kwa Unguja na Mkoani kwa Pemba). Hatua za kuhamasisha wanachama ili kuanzisha *SACCOS Bank* hizo zinaendelea.

9) Idara pia imetoa mafunzo juu ya uanzishwaji, usimamizi na uendeshaji wa *SACCOS Bank* kwa viongozi 56 kutoka *SACCOS Bank* 9 zilizopo Unguja. Vile vile, kwa kupitia msaada wa Benki ya *CRDB*, jumla ya viongozi 52 (wanawake 32 na wanaume 20) kutoka *SACCOS* 16 (9 za Unguja na 7 Pemba) walipatiwa mafunzo juu ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za kifedha kwenye *SACCOS* hizo.

10) Jumla ya vijana 30 (wanawake 15 na wanaume 15) wa vikundi vinavyojishughulisha na usafi wa mazingira vya Mpendae (MPE SAFI) na Mwanakwerekwe (*MECCO*), wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali, ambayo pia yalihusisha suala la usafishaji wa mazingira na mbinu mbadala za matumizi ya taka taka. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha vijana kuanzisha vikundi vya ushirika ili kujiajiri na kuweza kujipatia kipato kupitia shughuli za usafishaji mazingira. Baada ya mafunzo hayo, vijana hao walipatiwa vitendea kazi mbalimbali vikiwemo mabero, pauro, reki na viatu vya mvua (*Rain boots*) kwa ajili ya kuanzia shughuli hizo.

11) Katika kuimarisha uwezo wa kusimamia masuala ya ushirika, Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) liligharamia ziara ya mafunzo kwa watendaji wawili wa wizara kwenda kujifunza uzoefu na mafanikio ya shughuli za ushirika katika Mkoa wa Kilimanjaro, Tanzania Bara na Nairobi nchini Kenya. Wizara imeanza kuyafanyia kazi baadhi ya mambo ambayo watendaji hao wamejifunza kutokana na ziara hiyo.

Malengo ya Idara ya Ushirika kwa Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuanza maandalizi ya kuanzisha Benki ya Ushirika Zanzibar;

2. Kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa vyama vya ushirika 200;

3. Kusimamia utekelezaji wa sheria katika uendeshaji wa vyama vya ushirika;

4. Kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa vyama vikuu 6 vya ushirika na Shirikisho la Vyama vya Ushirika (*Cooperative Union of Zanzibar - CUZA*);

5. Kuimarisha ushirikiano na washirika wa masuala ya ushirika; na

6. Kuimarisha mazingira ya kazi, ikiwemo mafunzo kwa wafanyakazi na upatikanaji wa vifaa.

Mhe. Spika, ili Idara **ya** Ushirika iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Sabini na Mbili, Laki Tano Elfu Tisini na Nne (Shs. 72,594,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi Milioni Thelathini (T.Shs. 30,000,000/=) kwa kazi za maendeleo.

KAMISHENI YA KAZI

Mhe. Spika**,** katika mwaka 2011/2012 Kamisheni ya Kazi ilipanga kutekeleza malengo yanayoonekana katika ukurasa wa 49 kama hivi ifuatavyo:

1. Kuzipitia baadhi ya sheria za kazi za Zanzibar ili zikidhi mahitaji;

2. Kuendelea kutoa elimu juu ya sheria na kanuni za kazi na miongozo ya kazi;

3. Kuimarisha vitengo vya Kamisheni ya Kazi;

4. Kuimarisha masuala ya UTATU na majadiliano ya pamoja sehemu za kazi; na

5. Kuimarisha mashirikiano na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa zinazohusiana na masuala ya kazi pamoja na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa yanayohusiana na sekta ya kazi.

Utekelezaji wa Malengo ya Kamisheni ya Kazi

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, shughuli zifuatazo zimetekelezwa kupitia Kamisheni ya Kazi:

1) Kanuni za sheria za kazi zinazohusu Kamati ya Utatu, Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi, Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi na Mawakala Binafsi wa Ajira zimekamilishwa na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Kukamilika kwa Kanuni hizi kutarahisisha utekelezaji wa Sheria za Kazi.

2) Mafunzo maalum ya siku 3 juu ya mbinu za kisasa za ukaguzi kazi yalitolewa kwa Maafisa Kazi na Wakaguzi Kazi 33 (wanawake na 6 wanaume 27) wakiwemo 10 kutoka Pemba na 23 kutoka Unguja. Mafunzo hayo pia yaliwahusisha maafisa habari wawili (2) wa Wizara.

3) Elimu juu ya sheria na kanuni za kazi pamoja na miongozo yake imetolewa kupitia vipindi vya redio na televisheni. Jumla ya vipindi 14 vya redio viliandaliwa, ambapo kati ya hivyo 12 vilirushwa kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar na

viwili (2) kupitia redio binafsi ya Bomba FM. Pia vipindi 5 vya televisheni viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar.
Vile vile Maafisa wa Elimu Kazi walitoa taaluma juu ya sheria na kanuni za kazi katika taasisi 7 zifuatazo: Sufa Nursery and Primary School, Trifonia Academy, SHA High School, Mazson Hotel, Samaki Lodge ya Uroa, Kilindi Hoteli ya Nungwi na The Dream of Zanzibar ya Kiwengwa.

4) Jumla ya Taasisi 327 (268 Unguja na 59 Pemba) zimefanyiwa ukaguzi kazi. Miongozo imetolewa juu ya mapungufu yaliyobainika na kuagiza kurekebishwa kwa kasoro hizo.

5) Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi kimezinduliwa rasmi tarehe 27/04/2012 kufuatia kuteuliwa kwa watendaji wa kitengo hicho na kuapishwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar tarehe 09/03/2012. Kitengo hicho tayari kimeanza kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusiana na migogoro ya kazi. Kufanya kazi kwa kitengo hicho kutasaidia kupunguza mrundikano wa kesi katika Mahakama ya Kazi, kuharakisha uendeshaji wa kesi zinazohusiana na malalamiko ya kazi na kuimarisha mahusiano mema kazini.

6) Wafanyakazi 6 (wanawake 3 na wanaume 3) wa Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi wamepatiwa mafunzo juu ya usuluhishi wa migogoro ya kazi. Mafunzo hayo yaligharamiwa na ILO kupitia mradi wa “Labor Laws Compliance”. Aidha mafunzo ya vitendo yametolewa kwa wafanyakazi wa kitengo hicho katika Ofisi za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi ya Tanzania Bara. Mafunzo hayo ya wiki tatu yalifanyika katika ofisi za Tume hiyo katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro na Dar es salaam.

7) Kamati ya Utatu (Tripartite Committee) yenye wajumbe kutoka Serikalini, Jumuiya ya Waajiri na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi imeundwa kwa mujibu wa kifungu nambari 71 cha Sheria Nam. 1 ya Mahusiano Kazini ya Mwaka 2005. Madhumuni ya kuundwa kwa Kamati hii ni kuimarisha utendaji kazi wa Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi pamoja na kuimarisha mashirikiano kati ya Serikali, Jumuiya ya Waajiri na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi. Kamati hiyo imefanya vikao viwili ambavyo vilijadili masuala mbalimbali ya kazi, ikiwemo muhtasari wa kanuni za usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kazi ya mwaka 2011 na muundo na majukumu ya Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi.

8) Mikutano ya Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi imefanyika katika kipindi cha kila miezi mitatu kama sheria inavyoelekeza. Mikutano hiyo ilijadili ripoti za utekelezaji

wa shughuli za Kamisheni ya Kazi, ilipitisha kanuni mbalimbali za sheria za kazi na kutoa ushauri juu ya mambo mbalimbali yanayohusiana na masuala ya kazi.

9) Bodi ya Ushauri wa mambo ya Mishahara inayoundwa kwa mfumo wa Utatu unaohusisha Serikali, Jumuiya ya Waajiri na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi, imefanya mkutano mmoja kama sheria inavyoelekeza. Mkutano huo ulijadili na kutoa mapendekezo ya kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi. Kufuatia mapendekezo hayo, kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi kimetangazwa rasmi na kuanza kutumika mwezi Februari, 2012. Kima hicho kimepandishwa kutoka Shilingi Elfu Sabini (Tshs. 70,000/=) hadi Shilingi Laki Moja na Elfu Arobaini na Tano (Tshs. 145,000/=) kwa mwezi kwa wafanyakazi wenye mikataba ya kudumu. Kwa wafanyakazi wa kutwa, kima cha chini cha mshahara kimepanda kutoka Shilingi Elfu Nne na Mia Tano (Tshs. 4,500/=) hadi Shilingi Elfu Kumi (Tshs. 10,000/=) kwa siku kwa wenye ujuzi, na kutoka Shilingi Elfu Tatu na Mia Tano (Tshs. 3,500/=) hadi Shilingi Elfu Saba (Tshs. 7,000/=) kwa siku kwa wafanyakazi wa kutwa wasio na ujuzi. Kwa upande wa wafanyakazi wa majumbani, kiwango cha sasa cha mshahara ni Shilingi Elfu Sitini (Tshs. 60,000/=) kwa mwezi kutoka Shilingi Elfu Thalathini (Tshs. 30,000/=) kilichopitishwa mwaka 2008.

10) Katika kuimarisha mashirikiano kati ya Zanzibar na Tanzania Bara na taasisi nyengine za kazi, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) imefanya vikao viwili vya mashirikiano na Wizara ya Kazi na Ajira ya Tanzania Bara, iliyohusisha pia Jumuiya za Waajiri na Mashirikisho ya Vyama Huru vya Wafanyakazi kutoka pande zote mbili. Kikao cha kwanza kilifanyika Zanzibar mwezi Agosti 2011 na cha pili kilifanyika mwezi wa Aprili 2012 mjini Arusha. Vikao vyote hivyo vililenga kuimarisha mashirikiano kati ya Zanzibar na Tanzania Bara na kubainisha changamoto za sekta ya kazi kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha uongozi wa Wizara, muwakilishi kutoka Jumuiya ya Waajiri Zanzibar na muwakilishi kutoka Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Zanzibar walishiriki katika kikao cha ILO cha kanda ya Afrika kilichofanyika Afrika ya Kusini mwezi Oktoba 2011. Kikao hicho, pamoja na mambo mengine, kilijadili juu ya kujenga uwezo wa nchi za Afrika katika masuala yanayohusu kazi za staha.

Malengo ya Kamisheni ya Kazi kwa Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Kamisheni ya Kazi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi, sera na programu zinazohusu masuala ya kazi;
2. Kujenga uwezo katika usimamizi wa utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya kazi;
3. Kuimarisha mfumo wa usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kazi;
4. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kupambana na Ajira za Watoto;
5. Kuimarisha uhusiano na majadiliano ya pamoja katika sehemu za kazi; na
6. Kuimarisha mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa kuhusu masuala ya kazi.

Mhe. Spika**,** ili Kamisheni ya Kazi iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Sitini na Nne (T.Shs. 164,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi Milioni Kumi (T.Shs. 10,000,000/=) kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA AJIRA

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kukusanya taarifa za wafanyakazi walioajiriwa katika taasisi mbalimbali zilizoko Zanzibar;
2. Kuongeza fursa zaidi za ajira kwa wazalendo;
3. Kushirikiana na Kamati za Ajira za Kitaifa, Mikoa na Wilaya katika kujenga mikakati ya kutengeneza na kuwapatia ajira Wazanzibari;
4. Kukiimarisha na kukipatia taarifa, kitengo cha kukusanya na kutoa taarifa za ajira;
5. Kutoa elimu kuhusu ajira kupitia njia mbalimbali;
6. Kuimarisha mashirikiano na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala yanayohusu ajira; na
7. Kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira ya Tanzania Bara, Shirika la Kazi Duniani pamoja na washirika wa masuala ya kazi na ajira katika kutekeleza Programu ya Tanzania kuhusu kazi za staha.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Ajira

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 shughuli zilizotekelezwa kupitia Idara ya Ajira ni pamoja na zifuatazo:

1) Ili kupata picha juu ya hali ya ajira nchini, Idara imekusanya taarifa za wafanyakazi walioajiriwa katika taasisi za umma na binafsi. Kwa mujibu wa taarifa hizo, katika kipindi cha Julai 2011 hadi Aprili 2012 Serikali Kuu kupitia Tume ya Utumishi Serikalini imeajiri wafanyakazi 168 (wanawake 91 na wanaume 77). Aidha idadi ya wafanyakazi 170 (wanawake 96 na wanaume 74) wameajiriwa katika Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea na vijana 137 (wanawake 117 na wanaume 20) wameajiriwa na taasisi binafsi kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

2) Vijana 71 (wanaume 38 na wanawake 33) wa Jumuiya ya ZASOSE (Zanzibar Society for Sustainable Enviroment) wanaojishughulisha na kazi za usafi wa mazingira, wamepatiwa mafunzo ya siku nne yaliyokuwa na lengo la kuwaraghibisha wabadilike tabia, wawe na moyo wa kujituma, kupenda kazi na kutochagua kazi. Vijana hao pia wamepatiwa mafunzo juu ya ujuzi wa kutambua na kubuni mipango ya biashara ili kujiajiri pamoja na kuchangamkia fursa za ajira zinazokuwepo. Mafunzo hayo yameonesha mwelekeo mzuri wa vijana hao kubadilika, kwani baadhi yao wameanzisha vikundi vinavyojishughulisha na kazi za kutengeneza makaa kwa kutumia makaratasi na unga wa mbao; ushoni na kilimo.

62

3) Mikutano miwili iliyowahusisha wawakilishi wa taasisi 75 za kazi kutoka sekta za umma na binafsi ilifanywa kwa lengo la kuwaelewesha kuhusu Sera ya Ajira na Mpango wa Kuzalisha Ajira Zanzibar pamoja na suala zima la kujenga mazingira ya kutengeneza fursa zaidi za ajira kwa vijana wa Zanzibar. Vilevile Idara imefanya mkutano na Wakurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara zote za Serikali kwa lengo hilo hilo la kuwaelewesha kuhusu Sera ya Ajira na kuwataka kuweka katika mipango yao suala la ukuzaji wa ajira kwa vijana.

4) Mazungumzo yamefanywa na Jumuia ya Wawekezaji katika sekta ya utalii (ZATI) juu ya haja ya kuwasaidia vijana kupata fursa zaidi za ajira kwenye sekta ya utalii. ZATI walionesha mwelekeo mzuri wa kushirikiana na Serikali katika suala hili na walikubali kuwashajihisha wawekezaji kwenye sekta hiyo kutoa taarifa kwa Wizara pale zitapotokea nafasi za ajira.

5) Watendaji watatu wa Idara walifanya ziara ya mafunzo katika Wizara ya Kazi na Ajira Tanzania Bara, ili kujifunza uzoefu wa Idara ya Ajira na Wakala wa Ajira

Tanzania katika kusimamia masuala ya ajira, pamoja na kukubaliana maeneo ya mashirikiano.

Mhe. Spika, Shirika la Kazi Duniani katika mwaka 1948 lilitoa Muongozo Nambari 88 unaozitaka nchi wanachama wa Shirika hilo kuruhusu na kufanya kazi kwa mashirikiano na Wakala Binafsi wa Ajira ili wasaidie katika masuala ya ajira. Aidha, Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005 inaruhusu kuwepo kwa Wakala Binafsi wa Ajira ambao watafanya kazi kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa.

Wizara yangu hivi karibuni imepitisha kanuni zinazoweka utaratibu wa kufanya kazi na Wakala Binafsi wa Ajira. Kufuatia kupitishwa kwa kanuni hizo, kampuni nne tayari zimeshaomba kupatiwa leseni ya kufanya kazi hiyo. Kampuni hizo ni:

1) Zamu Travelling Agency;
2) Reyle Company Ltd;
3) All-in-one Business Company Limited; na
4) SPS Job Centre and Travelling Agency Ltd

Kampuni hizo zote zimefanyiwa uhakiki na tayari zimepewa ruhusa ya kufanya kazi ya uwakala wa ajira baada ya Wizara, kupitia Kamisheni ya Kazi, kuridhika kuwa zimetimiza masharti ya msingi.

63

Inategemewa kwamba wakala hawa watasaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana. Wizara kupitia Kamisheni ya Kazi imeweka utaratibu mzuri wa kuratibu shughuli za wakala hawa ili kuona kuwa wanafanya kazi kama sheria na kanuni zinavyoelekeza. Utaratibu huu unahusisha ukaguzi wa shughuli za wakala hawa katika kila kipindi maalum ili kusimamia utekelezaji wa sheria, pamoja na suala zima la upatikanaji wa taarifa juu ya ajira zitazopatikana kupitia wakala hawa.

Malengo ya Idara ya Ajira kwa Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 Idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za soko la ajira;

2. Kuzalisha ajira zipatazo 2,000 kupitia sekta mbali mbali za umma na binafsi;

3. Kushajihisha jamii kuchukuwa hatua juu ya masuala ya ajira kwa vijana;

4. Kurasimisha ajira isiyo rasmi kwa kuanzia na sekta ya usafirishaji wa umma kwa kushirikiana na taasisi husika; na

5. Kuimarisha mtandao na mashirikiano na washirika mbalimbali juu ya masuala ya ajira.

Mhe. Spika, ili Idara ya Ajira iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Sabini na Tisa (T.Shs. 79,000,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yanayoonekana katika 62 hadi 63 kama hivi ifuatavyo:

1. Kufanya marekebisho na kuimarisha mpango wa ukaguzi kwa ajili ya kutathmini hali ya usalama na afya katika sehemu za kazi;

2. Kuijengea uwezo Idara ya Usalama na Afya Kazini kwa kuipatia vifaa vya kisasa na utaalamu ili kwenda sambamba na viwango vya kitaifa na kimataifa;

3. Kutayarisha Sera ya Usalama na Afya Kazini;

4. Kutekeleza mpango wa usajili wa sehemu za kazi;

5. Kukuza ushirikiano wa kazi na taasisi nyengine ndani na nje ya nchi;

6. Kufuatilia kwa karibu zaidi matukio ya ajali, maradhi na madhara yanayotokana na ajali kwenye sehemu za kazi; na

7. Kuweka utaratibu bora wa wafanyakazi kuchunguzwa afya zao.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Usalama na Afya Kazini

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Idara ya Usalama na Afya Kazini imetekeleza shughuli zifuatazo :

1) Imezikagua sehemu za kazi 231 (187 Unguja na 44 Pemba) ili kuangalia hali ya usalama na afya kwenye maeneo hayo. Ushauri ulitolewa juu ya kurekebisha kasoro zilizobainika.

2) Imekusanya taarifa za sehemu za kazi zilizosajiliwa na Bodi ya Mapato Zanzibar, Halmashauri za Wilaya, Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji na Mrajis Mkuu wa

Serikali pamoja na za Wizara zote 16 za Serikali ikiwa sehemu ya maandalizi ya kuzisajili kwa ajili ya tathmini ya masuala ya usalama na afya.

3) Katika kuimarisha mpango wa ukaguzi wa kutathmini hali ya usalama na afya katika sehemu za kazi, Idara kwa kushirikiana na washirika wengine wanaohusiana na masuala haya, imeandaa miongozo muhimu inayohitajika ikiwemo viwango vya kitaifa juu ya usalama na afya kazini na orodha (cheklist) wa mambo ya kuangaliwa katika kufanya ukaguzi wa kutathmini masuala ya usalama na afya katika sehemu za kazi. Pia kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Idara imeandaa rasimu ya muongozo wa kupima afya za wafanyakazi. Tayari rasimu ya muongozo huo imewasilishwa kwa wahusika wengine na wametoa maoni yao ambayo yanafanyiwa kazi katika kukamilisha muongozo huo.

4) Katika kuimarisha mashirikiano na taasisi nyengine zinazoshughulikia masuala haya, Kamati ya kusimamia masuala ya usalama na afya kazini imeundwa na imeanza kufanya kazi. Kamati hiyo yenye mfumo wa utatu inajumuisha wawakilishi kutoka Serikalini, Jumuiya ya Waajiri na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi.

5) Ili kuongeza uelewa wa masuala ya usalama na afya kazini, watendaji wanne wa Idara walishiriki katika ziara ya kujifunza katika Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini, Makao Makuu Dar es Salaam. Katika ziara hiyo pande mbili zimekubaliana kuendeleza mashirikiano yakiwemo kusaidiana utaalamu katika masuala ya ukaguzi wa usalama na afya kazini.

65

Malengo ya Idara ya Usalama na Afya Kazini kwa mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo wa ukaguzi wa hali ya usalama na afya katika sehemu za kazi;

2. Kukuza uelewa kwa waajiri, wafanyakazi na jamii kwa jumla juu ya Sheria Nambari 8 ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005;
3. Kuimarisha utendaji kazi wa Kamati ya Usalama na Afya Kazini;

4. Kujenga uwezo wa watendaji wa Idara katika kusimamia utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005; na

5. Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa masuala ya usalama na afya kazini.

Mhe. Spika, ili Idara ya Usalama na Afya Kazini iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Themanini na Sita, Laki Sita na Elfu Arobaini na Mbili (T.Shs. 86,642,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI KUU PEMBA.

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kusimamia shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa maana hiyo, inatekeleza malengo yaliyopangwa na Idara mbali mbali zilizo chini ya Wizara. Hivyo, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2011/2012 na malengo kwa mwaka 2012/2013 ni kama ambavyo yameshaelezwa katika maelezo ya kila Idara, ambayo yanahusisha pia na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, Ili Ofisi Kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini na Sita, Laki Mbili na Kumi na Nne Elfu (T.Shs. 156,214,000/=) kwa kazi za kawaida na Shilingi Milioni Mia Moja na Themanini (T.Shs.180,000,000/=) kwa ajili ya mishahara, mchango wa ZSSF na posho za wafanyakazi.

SHUKRANI

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendeleza mashirikiano na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa katika kufanikisha malengo iliyojipangia. Aidha, itaendeleza ushirikiano na Wizara nyengine za Serikali, sekta binafsi na taasisi za kijamii ambazo kwa namna moja ama nyengine, zinachangia katika masuala ya kazi, uwezeshaji wananchi kiuchumi na ushirika. Napenda kuchukua nafasi hii adhimu kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa, nchi wahisani na taasisi mbali mbali za Serikali na zisizo za Serikali ambazo zilishirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake katika nyanja mbalimbali. Hizi ni pamoja na: Shirika la Kazi Duniani (ILO); Mashirika ya Umoja wa Mataifa; Ofisi inayoshughulikia masuala ya Kazi ya Marekani (US Department of Labour); Save the Children; Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF); Benki Kuu ya Tanzania; Benki ya Watu wa Zanzibar; CRDB; Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima; Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (ZANEMA); na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (ZATUC). Pia napenda kuzishukuru Serikali za China, Oman na India kwa kutupatia nafasi za mafunzo katika fani mbalimbali kwa baadhi ya watendaji wa Wizara. Aidha, natoa shukurani kwa taasisi zisizokuwa za Serikali ambazo nazo zimechangia katika juhudi za Serikali za kuwawezesha wananchi wa Zanzibar, kwa lengo la kuwaletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika, natoa shukrani maalum kwa Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar pamoja na watendaji wake, akiwemo Mwenyekiti wa Mahkama ya Kazi, kwa mashirikiano wanayotupa katika kushughulikia kesi zinazohusu migogoro ya kazi. Mashirikiano ya karibu yaliyopo kati ya Mahkama ya Kazi na Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi kiliopo chini ya

Wizara yangu yamesaidia sana kuharakisha utatuzi wa migogoro ya kazi na pia kupunguza mrundikano wa kesi zinazotokana na migogoro hiyo. Shukrani zangu pia ziwaendee Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi na Kamati zetu mbali mbali kwa kazi nzuri wanayofanya. Ushauri wao umesaidia sana katika kuimarisha utendaji wa majukumu yetu na katika kufanikisha malengo ya Wizara kwa jumla.

Mhe. Spika, vyombo vya habari zikiwemo televisheni, redio na magazeti vimetoa mchango mkubwa katika kuhamasisha, kutangaza na kuelimisha jamii juu ya masuala na matukio mbalimbali yaliyotekelezwa na Wizara yangu. Napenda nitoe shukrani maalum kwa vyombo hivyo kutokana na mchango wao huo muhimu.

Mhe. Spika, nashukuru kwamba kwa kipindi chote tangu niongoze Wizara hii, nimefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na watendaji wa Wizara yangu. Nawashukuru sana Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi wote, Afisa Mdhamini na wafanyakazi wa ngazi zote kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu na kwa uwajibikaji wao katika kutekeleza majukumu mbali mbali ya Wizara. Sina wasiwasi wataendelea kufanya kazi kwa ari na bidii zaidi ili kutekeleza malengo tuliyoyapanga kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mhe. Spika, pia natumia fursa hii kutoa shukrani Maalum kwa Wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa mashirikiano wanayonipa katika kufanikisha kazi zangu za uwakilishi wa jimbo hilo. Nawashukuru sana kwa imani yao na nawaomba waendelee kushirikiana na mimi, ili kwa pamoja tutekeleze yale tuliyoyapanga na tuweze kupiga hatua ya maendeleo.

Mhe. Spika, kabla sijatoa hitimisho naomba niwatakie Ramadhani njema wananchi wote wa Zanzibar.

HITIMISHO

Mhe. Spika, ili Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu litafakari, lijadili na kuidhinisha matumizi ya jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Sita na Sabini na Tisa (T.Shs.2,679,000,000/=) kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Themanini (T.Shs.1,080,000,000/=) ni kwa ajili ya mishahara na posho za wafanyakazi na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu na Kumi na Moja (T.Shs.1,311,000,000/=) ni kwa matumizi mengineyo. Vile vile naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne na Hamsini na Tano, Laki Nane na Elfu Sitini na Moja (T.Shs.1,455,861,000 /=) kwa kazi za maendeleo, ambapo kati ya hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja na Arobaini **(**T.Shs.1,140,000,000/=) zitatolewa na Serikali na Shilingi Milioni Mia Tatu Kumi na Tano, Laki Nane na Elfu Sitini na Moja (T.Shs.315,861,000 /=) zitatolewa na wahisani. Aidha, Wizara inategemea kupata Shilingi Milioni Mia Sita na Moja, Laki Saba Arobaini na Moja Elfu, Mia Nane na Tisini na Sita (T. Shs. 601,741,896/=) kutoka ILO kupitia Mradi wa UNDAP. Pia

naomba idhini ya kukusanya mapato ya Shilingi Milioni Tisini na Tatu (T.Shs.93, 000,000/=) kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Ahsanteni**.**

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Nambari 1: Mapato Yaliyokusanywa Kuanzia Julai 2011 – Juni 2012

Idara	Kasma		Makadirio	Fedha Zilizokusanywa	Asilimia
Kamisheni ya Kazi	142212	Malipo ya Vibali vya Kazi.	57,000,000/=	108,439,975/=	190.2
	142213	Malipo ya Ukaguzi Sehemu za Kazi/Mikataba.	3,000,000/=	2,559,000/=	85.3
Idara ya Ushirika	142239	Ada ya Uandikishaji Vyama.	4,500,000/=	9,850,000/=	218.9
	142240	Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma.	4,000,000/=	2,428,000/=	60.7
Jumla Kuu			**68,500,000/=**	**123,276,975/=**	**180.0**

Kiambatanisho Nambari 2: Mapato/Fedha Zilizoingizwa za Matumizi ya Kawaida kwa Mwezi wa Julai 2011 Hadi Juni 2012

Idara	Makadirio 2011/2012	Fedha zilizopatikana (Matumizi) 2011/2012	Asilimia
1. Afisi kuu – Pemba.	90,000,000	88,944,246	98.8
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.	120,820,000	103,485,214	85.65
3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.	382,000,000	346,746,000	90.77
4. Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.	69,900,000	54,900,000	78.54
5. Kamisheni ya Kazi.	110,000,000	105,511,210	95.9
6. Idara ya Ajira.	65,000,000	55,460,000	85.32
7. Idara ya Usalama na Afya Kazini.	69,330,000	61,643,330	89.0
8. Idara ya Ushirika.	62,950,000	56,284,000	89.41
9. Idara ya Mikopo.	110,000,000	119,160,764	108.3
Jumla Kuu	**1,080,000,000**	**992,134,764**	**91.86**

Kiambatanisho Nambari 3: Orodha ya Wafanyakazi Waliopatiwa Mafunzo Mafupi kwa Mwaka 2011/2012:

S/NO	JINA	JINSI		IDARA	CHUO/ TAASISI	PAHALA	FANI	UFADHILI
		M'KE	M'ME					
1.	Rajab Dadi Rajab		X	Uendeshaji na Utumishi	Chuo Cha Usafiri (NIT)	Tanzania Bara	Udereva	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
2.	Thuwaiba Idarous Kassim	X		Uendeshaji na Utumishi	Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)	Zanzibar	Utunzaji kumbukumbu	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
3.	Nassor Abdalla Makame		X	Uendeshaji na Utumishi	Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)	Zanzibar	Utunzaji kumbukumbu	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
4.	Ali Abdalla		x	Ushirika	Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)	Zanzibar	Uhasibu	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika

5.	Ali Moh'd Suleiman		**x**	Ushirika	Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)	Zanzibar	Uhasibu	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
6.	Saade Khamis Ali	x		Uendeshaji na Utumishi	Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)	Zanzibar	Ukatibu Mhutasi (Secretary)	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika

220106	Gharama za utangazji			6 020 000.00							**6 020 000.00**
220108	Hudumа za mtandao	1 480 000.00		7 100 000.00		60 000.00				3 755 000.00	**12 395 000.00**
220111	Hudumа za studio			1 050 000.00		3 700 000.00	4 250 000.00	900 000.00	80 000.00		**9 980 000.00**
	Jumla ndogo	**4 880 000.00**	**3 750 000.00**	**36 010 000.00**		**6 674 000.00**	**5 615 000.00**	**1 000 000.00**	**490 000.00**	**4 310 000.00**	
220200	**Viburudishaji**										**-**
220201	Chakula na vinywaji	5 675 000.00	20 700 000.00	21 300 000.00		5 310 000.00	11 595 000.00	3 530 000.00	25 060 000.00	5 770 000.00	**98 940 000.00**
220202	Ununuzi wa zawadi	800 000.00		5 400 000.00					3 000 000.00		**9 200 000.00**
	Jumla ndogo	**6 475 000.00**	**20 700 000.00**	**26 700 000.00**		**5 310 000.00**	**11 595 000.00**	**3 530 000.00**	**28 060 000.00**	**5 770 000.00**	

220 300	**Gharama za safari**										**-**
220 301	safari za ndani	14 400 000.00	16 890 000.00	12 480 000.00		2 850 000.00	3 850 000.00	9 090 000.00	4 740 000.00	4 740 000.00	**69 040 000.00**
220 302	Safari za nje			24 000 000.00		13 000 000.00	11 000 000.00	8 000 000.00	1 000 000.00		**57 000 000.00**
220 303	Gharama za Visa						400 000.00				**400 000.00**
	Jumla ndogo	**14 400 000.00**	**16 890 000.00**	**36 480 000.00**		**15 850 000.00**	**15 250 000.00**	**17 090 000.00**	**5 740 000.00**	**4 740 000.00**	
220 400	**Gharama za mafuta na vilainishaji**										**-**
220 401	Gharama za petrol	3 920 000.00	4 002 000.00	31 050 000.00		7 820 000.00	6 199 000.00	7 061 000.00	3 694 000.00	1 399 000.00	**65 145 000.00**
220 402	Gharama za disel	1 520 000.00		23 000 000.00						7 208 000.00	**31 728 000.00**
220 404	Gharama za vilainishaji	1 026 000.00				56 000.00				684 000.00	**1 766 000.00**
220 407	Gharama za maji	480 000.00		600 000.00							**1 080 000.00**
220 408	Gharama za umeme	30 414 000.00		14 400 000.00						600 000.00	**45 414 000.00**
	Jumla ndogo	**37 360 000.00**	**4 002 000.00**	**69 050 000.00**		**7 876 000.00**	**6 199 000.00**	**7 061 000.00**	**3 694 000.00**	**9 891 000.00**	
220 500	**Vifaa na hudumu za ofisi**										**-**
220	Vifaa	8	4	20		4	2	2	1	2	

72

501	vya kuandika	199 000.00	004 000.00	290 000.00		614 000.00	000 000.00	971 000.00	906 000.00	108 000.00	**46 092 000.00**
220 501						3 206 000.00	1 010 000.00	3 100 000.00			**7 316 000.00**
220 504	vifaa vya kompyuta	8 100 000.00		2 760 000.00		600 000.00	2 100 000.00	920 000.00		2 225 000.00	**16 705 000.00**
220 505	vifaa vidogo vidogo			1 840 000.00						70 000.00	**1 910 000.00**
220 506	vifaa vya usafi	600 000.00		4 200 000.00						80 000.00	**4 880 000.00**
220 507	ufukizaji	400 000.00		1 500 000.00							**1 900 000.00**
220 508	Ununuzi wa magazeti na majarida	1 200 000.00		12 900 000.00							**14 100 000.00**
220 509	Malipo ya ushauri		5 000 000.00			8 200 000.00				12 000 000.00	**25 200 000.00**
220 515	Vifaa vya Michezo			5 000 000.00							**5 000 000.00**
	Jumla ndogo	**18 499 000.00**	**9 004 000.00**	**48 490 000.00**		**16 620 000.00**	**5 110 000.00**	**6 991 000.00**	**1 906 000.00**	**16 483 000.00**	
220 600	**Samani za ofisi**										**-**
220 601	ununuzi wa mazulia ,makapeti			3 000 000.00						400 000.00	**3 400 000.00**
220 602	Ununuzi wa vifaa vya									55 000.00	**55 000.00**

	jikoni										
220 603	Ununuzi wa viti meza makabati	14 000 000.00		28 400 000.00						2 060 000.00	**44 460 000.00**
	Jumla ndogo	**14 000 000.00**		**31 400 000.00**		-		-	-	**2 515 000.00**	
220 700	**matengenezo ya ofisi/nyumba**										-
220 701	Matengenezo madogo madogo	2 060 000.00		28 162 000.00							**30 222 000.00**
	Jumla ndogo	**2 060 000.00**		**28 162 000.00**							
220 800	**Matengenezo ya zana**								74		-
220 802	Ununuzi wa spare na zana			36 000 000.00						1 500 000.00	**37 500 000.00**
220 803	Matengenezo ya magari	6 000 000.00		13 000 000.00		600 000.00				1 470 000.00	**21 070 000.00**
220 804	Vifaa vya magari									1 800 000.00	**1 800 000.00**
220 806	Gharama za bima	1 000 000.00		4 000 000.00							**5 000 000.00**
	Jumla ndogo	**7 000 000.00**		**53 000 000.00**		**600 000.00**	-	-	-	**4 770 000.00**	
221 100	**Gharama za mafunz**										-

	o										
221102	mafunzo ya ndani	11 500 000.00	5 600 000.00	40 288 000.00		2 620 000.00	3 851 000.00	15 000 000.00	5 660 000.00	1 435 000.00	**85 954 000.00**
221103	mafunzo ya nje										**-**
221104	Malipo ya ada									1 720 000.00	**1 720 000.00**
221199	Vifaa vya mafunzo	7 150 000.00	4 164 000.00	5 800 000.00		6 120 000.00	9 580 000.00	6 480 000.00	20 000 000.00	8 940 000.00	**68 234 000.00**
	Jumla ndogo	**18 650 000.00**	**9 764 000.00**	**46 088 000.00**		**8 740 000.00**	**13 431 000.00**	**21 480 000.00**	**25 660 000.00**	**12 095 000.00**	
263101	Ruzuku kwa Ajili ya Mishahara				117 916 000.00						
263102	Ruzuku kwa Ajili ya Uendeshaji				170 084 000.00						
					288 000 000.00						
272100	**Misaada ya kijamii**										**-**
272108	kusaidia shughuli za kiuchumi na kijamii			5 000 000.00							**5 000 000.00**
	Jumla ndogo			**5 000 000.00**							
281401	Kodi ya Ofisi	6 000									**6 000**

		000.00									**000.00**
281 402	kodi ya Ukumb i			1 000 000.00						120 000.00	**1 120 000.00**
282 109	Gharam a za mazishi	800 000.00		1 800 000.00							**2 600 000.00**
	Jumla ndogo	**6 800 000.00**	-	**2 800 000.00**		-	-	-	-	**120 000.00**	
311 202	ununuzi wa gari					50 000 000.00					**50 000 000.00**
311 203	ununuzi wa vespa honda ,vespa na ciao	2 500 000.00	5 000 000.00	7 500 000.00			5 000 000.00				**20 000 000.00**
311 205	ununuzi wa frigi									780 000.00	**780 000.00**
311 206	Ununuz i wa AC			10 000 000.00							**10 000 000.00**
311 207	Ununuz i wa Kompy uta		3 000 000.00	22 900 000.00				2 500 000.00	3 000 000.00		**31 400 000.00**
311 208	Ununuz i wa Printa	1 500 000.00	1 600 000.00	4 900 000.00							**8 000 000.00**
311 209	ununuzi wa skana		1 000 000.00	600 000.00							**1 600 000.00**
311 210	Ununuz i wa Fotoko pi			10 000 000.00							**10 000 000.00**
311 214	Ununuz i wa TV			500 000.00							**500 000.00**
311 298	Hudum a za mawasi liano	1 450 000.00									**1 450 000.00**

	Jumla ndogo	**5 450 000.00**	**10 600 000.00**	**56 400 000.00**		**50 000 000.00**	**5 000 000.00**	**2 500 000.00**	**3 000 000.00**	**780 000.00**	
	GRAND TOTAL	**336 214 000.00**	**222 407 000.00**	**844 681 000.00**		**310 703 000.00**	**137 274 000.00**	**143 200 000.00**	**149 042 000.00**	**247 479 000.00**	**2 679 000 000.00**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Uwasilishaji huu ni utaalamu maalum ambao na Waheshimiwa wengine wakifanya Waheshimiwa Mawaziri kwa kweli itasaidia sana.

Mhe. Salim na wewe chukua nafasi kumuwakilisha Mwenyekiti.

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa heshima kabisa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu, kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia kukutana hapa katika Baraza letu, tukiwa katika hali ya uzima na afya njema, kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu na Taifa kwa ujumla. Aidha, napenda nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Baraza hili, ili kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika**,** kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, natumia fursa hii kumpongeza sana Mhe. Marina Joel Thomas kwa kuteuliwa kwake kuwa mjumbe wa Bazara hili, uteuzi ambao umekamilisha jumla ya nafasi kumi za uteuzi wa Rais. Ni imani yetu kuwa Mhe. Rais amefanya maamuzi ya busara sana hadi kufikia uamuzi wake wa kumteua Mhe. Marina. Ingawa ni nafasi ya kumalizia lakini tunaamini kuwa nafasi hii ni *" the last but not the least".*

Mhe. Spika**,** naomba kutumia fursa hii kuwatunukia taji la shukrani Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari inayoongozwa na nahodha shupavu Mhe. Asha Bakari Makame. Pia naomba uniruhusu Mhe. Spika kuwataja kwa majina Wajumbe hawa mmoja baada ya mwengine kama ifuatavyo:

1. Mhe. Asha Bakari Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Mohammed Said Mohamed - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Asaa Othman Hamad - Mjumbe

4. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
5. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Abdi Mossi Kombo - Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
8. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe
9. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu
10. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

Mhe. Spika, tunaipongeza sana Wizara kwa kutekeleza jukumu lake la msingi la kuvikagua na kuvisimamia vyama vya ushirika nchini, ili kuvipatia mwongozo unaostahiki kwa nia ya kuvikuza na kuviendeleza zaidi.

Aidha, Kamati imepokea kwa huzuni taarifa ya kwamba kati ya vyama 5,503 vilivyosajiliwa nchini, ni vyama 1,651 tu ndivyo vilivyo hai ambavyo ni sawa na asilimia 30%. Ili kuwa na vyama vya Ushirika vilivyo imara zaidi, Wizara haina budi kuchukua hatua za dharura za kuwasiliana na vyama visivyo hai kwa nia ya kuyajua matatizo yanayowakabili na kuangalia uwezekano wa kuvifufua upya, na ikishindikana basi kuwe na utaratibu wa kuvifuta.

Halikadhalika, ni vyema kuwa na utaratibu wa usajili wa vyama vya ushirika utakaowaweka karibu zaidi wanaushirika na Idara ya usajili, kwani hali ya sasa ya usajili ni mbaya na Kamati imebaini kuwa urasimu katika mpangilio wa kufanya usajili ndiyo kikwazo kikuu cha wanaushirika kutojisajili.

Mhe. Spika**,** kamati yetu inatoa wito kwa Wizara kupitia Idara ya Ushirika kutafuta wafadhili wengine ili kupata fedha za kutekeleza miradi ya vyama sita vya ushirika ambapo kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ni mradi mmoja tu wenye thamani ya shilingi 7,450,000/= ndio pekee ulioweza kutekelezwa.

Aidha, Wizara isimamie vyema mwenendo mzima wa *SACCOS Banks* zilizoanza kufanya kazi, ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yao ipasavyo na hatimaye kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, katika kutafuta suluhisho la tatizo la ukosefu wa ajira nchini, tunaipongeza Wizara kwa kufanikiwa kupata fursa za ajira kwa vijana wetu nchini Oman. Aidha, vijana 20 wa Zanzibar wanatarajiwa kupatiwa mafunzo nchini humo ili kujiweka tayari kuuzika kwenye soko la ajira. Kamati inashauri kuwa taarifa zitolewe kwa vijana wote kwa uwazi kabisa ili waweze kujitokeza kuitumia fursa hii, kwani imebainika kuwa vijana wengi huishia mitaani tu bila ya kufahamu fursa zinazotolewa na Serikali yao pamoja na taasisi binafsi. Aidha, wakati utakapofika wa kuanza mpango huu vijana wapewe nafasi hizo kwa kuzingatia sifa zao "*academic qualifications*", ili kujiepusha na kupeleka vijana wasio na sifa zinazostahiki, jambo

ambalo linaweza kupelekea kufutwa kwa nafasi hizi kwenye miaka michache ijayo na hiyo itakuwa ni hasara kubwa kwa Taifa hili.

Mhe. Spika**,** ni ukweli usiopingika kwamba waajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wale wa sekta binafsi nchini wanakabiliwa na mazingira magumu ya kiutendaji kutokana na kutowepo kwa vifaa vya kinga na usalama katika maeneo yao ya kazi. Sambamba na hilo, Kamati imegundua kwamba mafunzo ya jinsi ya kuvitumia vifaa vya kinga yanahitajika kwa watendaji wa taasisi hizo, ili kuwajengea uwezo wa kujinusuru wakati wa dharura.

Mhe. Spika, tunatoa shukrani za dhati kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, jumla ya shilingi Milioni mia moja na ishirini na tatu, laki mbili sabini na sita elfu, mia tisa na sabini na tano (123,276,975/=) zimekusanywa, ambazo ni sawa na asilimia 180 ya makadirio. Ni matumaini yetu kwamba, Wizara itaendeleza jitihada hizi za kukusanya mapato vizuri kwa mwaka huu wa fedha ili kufanya matumizi mazuri kwa mwaka unaofuata kwa nia ya kujenga Taifa.

Mhe. Spika, kamati inatoa pongezi maalum kwa Wizara kwa kutekeleza programu ya Kazi nje nje katika mwaka wa fedha 2011/2012. Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), Wizara imeanza kutekeleza Programu hiyo kuanzia mwezi wa Machi 2011, na inalenga kuwawezesha vijana kuwa na muamko wa kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea kuajiriwa, kwani hali ya upatikanaji wa ajira nchini inazidi kuwa ngumu. Katika awamu ya kwanza programu hiyo imetoa mafunzo ya wiki mbili kwa vijana 32 juu ya ujasiriamali na kubadili tabia kwa lengo la kujiajiri.

Mhe. Spika**,** kuwepo kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni muhimu sana katika kupima utekelezaji wa mipango ya Wizara. Kamati yetu inaipongeza sana Wizara kwa kuuona umuhimu huo na kuandaa mfumo wa tathmini ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi wa Agosti 2012. Ni dhahiri kuwa kupatikana kwa kipimo cha mafanikio ya miradi mbalimbali kutawafanya watendaji wawe imara zaidi, ili kuhakikisha wanafikia kiwango kikubwa pindi watakapotathminiwa, na hivyo kusukuma mbele gurudumu la maendeleo nchini.

Mhe. Spika**,** ili kupata dira ya kutuelekeza kwenye utatuzi wa masuala ya kiuchumi, Wizara imefanya tafiti katika maeneo muhimu ya kiuchumi ili kubaini fursa zilizopo na mahitaji halisi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa hatua hii na inashauri matokeo ya tafiti hizi yafanyiwe kazi kikamilifu, katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 ili tupate tija kwa maslahi ya Taifa.

Mhe. Spika**,** kamati imefarajika sana na mpango wa programu ya kuifanya sekta isiyo rasmi ya usafiri wa umma kuwa bora na endelevu, ili kuwawezesha vijana walioajiriwa katika sekta hiyo kuwa na ajira za uhakika zenye mikataba inayoendana na Sheria za Kazi. Hii ni hatua muhimu ambayo itawasaidia vijana wetu kufaidika na jasho lao wenyewe, badala ya kuwatajirisha waajiri wao pekee kama mfumo wa sasa ulivyojengeka. Aidha, mazingira mazuri ya kazi yatatusaidia kujenga tabia ya uaminifu baina ya waajiri na waajiriwa, na hivyo kuzidi kudumisha amani, utulivu na umoja wetu.

Mhe. Spika**,** hatua iliyofikiwa na Wizara kuwaunganisha wamiliki wa mahoteli na wazalishaji wadogo wadogo pamoja na wajasiriamali inatoa mwelekeo wa kuanza kulipatia ufumbuzi tatizo

la ukosefu wa soko la bidhaa za wajasiriamali nchini kwa mwaka huu wa fedha wa 2012/2013. Katika zoezi hili, jumla ya hoteli kumi na moja zimetembelewa na Wizara na kufanya mazungumzo na uongozi kuhusu umuhimu wa kutumia bidhaa za ndani badala ya kuagiza bidhaa zinazoweza kuzalishwa nchini.

Kamati inatoa wito kwa Wizara kuuendeleza mpango huu mzuri waliouanzisha na kuufanyia utaratibu mwafaka ili wajasiriamali wengi zaidi waweze kufaidika na soko hilo.

Mhe. Spika**,** pamoja na kuendelea na harakati za utoaji wa mikopo nchini, Kamati inasisitiza kwamba, Wizara itoe mikopo ambayo itawawezesha kikweli wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, tunamaanisha kuwa mikopo hiyo iwe ya kiwango kinachostahiki kwa mujibu wa mradi unaokusudiwa kutekelezwa, isiwe na riba kubwa, na miradi inayotekelezwa iwe imeibuliwa kitaalamu na kuhakikishwa kuwa italipa baada ya muda fulani.

Aidha, Kamati yetu imefarajika sana na mpango wa Serikali wa kuanzisha Benki ya Wanawake nchini. Hatua hii ni muhimu katika kuleta ukombozi wa mwanamke kutoka katika hali ya utegemezi na kufanya shughuli ndogo ndogo za kiuchumi hadi kufikia kuwa wamiliki wa biashara kubwa kubwa zenye kutoa fursa za ajira kwa wengine. Ni dhahiri kuwa hii ni nyota njema inayohitaji kuendelezwa kwa maslahi ya wananchi wa Taifa hili.

Mhe. Spika**,** ili kutimiza malengo ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waichangie, waijadili na hatimaye waipitishe bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ambayo ni jumla ya shilingi za Kitanzania 2,679,000,000/=.

Mhe. Spika**,** mwisho kabisa, natoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa utulivu na usikivu wao, tunamuomba Mola mtukufu awape nguvu na hekima katika kuliongoza Taifa hili kwa umakini na uadilifu mkubwa.
Kwa niaba ya Kamati yangu, na wananchi wangu wa jimbo la Mtambwe naunga mkono bajeti hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na naomba kuwasilisha. Ahsante,

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Salim Abdalla Hamad. Kwenye uchangiaji wa jumla naomba nianze kumkaribisha Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadae Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi asubuhi hii ili kutia baraka wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Mhe. Spika, kwanza muwasilishaji wa ripoti hii aliyewasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti nampongeza sana, lakini kuna suala kidogo limenishtusha alilozungumza hapa, imenibidi mimi nianze kuchangia kabla ya kuendelea na kifungu hadi kifungu.

Mhe. Spika, amesema anashukuru sana kwa kuanzishwa kwa benki ya kinamama. Sasa kama nimesikia hilo, ningeomba basi aje Waziri ili anihakikishie kama hiyo benki imeshakuwa tayari ama yumo katika kushawishi ili nimuunge mkono tushawishi hii benki ili iweze kufanywa kwa haraka, kwa sababu gani. Juzi Mhe. Spika, nilikuwa nimepumzika nyumbani nilimsikia Waziri wa kule Bungeni alisema kuwa wako tayari katika harakati za mwisho kabisa kuweza kufungua benki hii ya kinamama. Mimi nikasema pamoja na hayo na sisi Zanzibar tuna haja ya kuwa na

benki hiyo ya kinamama na sisi tuharakishe haraka sana, kwa sababu kinamama sasa hivi ndio wanaodhalilika na kukosa ajira kwa wingi sana katika sehemu husika.

Mhe. Spika, nikiingia katika ukurasa huu wa idara ya utafiti. Namuomba sana Mhe. Waziri wangu hili ni fungu kubwa sana la utafiti, kuna mambo ambayo sitaki nije kulizuia fungu hili, lakini ningeomba sana nitakapoanza kuchangia anisaidie ufafanuzi ili fungu hili mimi nisije kulizuia au nikaja kupiga buti sio lengo langu kubwa. Naomba sana kuna mambo katika kifungu cha 4 hapa, kuratibu na kutayarisha sera za utafiti kuhusiana na masuala mbali mbali kulingana na majukumu ya Wizara. Ningeomba kama kuna *activity* tayari amezikusanya ningeomba aje kunieleza ule mpangilio wenyewe, naomba sana Mhe. Waziri kwa hapa aje na *activity* zake ili ziende sambamba na fungu kuu, ili tuje kwenda vizuri.

Mhe Spika, katika ukurasa wa 13, mradi wa kupambana na ajira za watoto. Mhe. Spika, bado hizi ajira za watoto niseme kuwa linatushinda kwa asilimia kubwa sana. Kwa sababu ukiangalia inasikitisha sana watoto bado wanaendelea kutumwa na wazee wao, na watoto wanadhalilishwa kutokana na hii hali, kila siku tunapanga miradi hiyo au programu hizo, lakini kazi zake zinakuwa hazikamiliki vizuri. Naomba sana Mhe. Spika, hapa ndipo pa kuweza kukaza sasa hivi, kwa sababu hili wimbi limekuwa kubwa sana na inasikitisha. Watoto wadogo kabisa wanapewa zile sinia za kuuzia vitu zinawazidi kimo, kwa sababu sinia kubwa yeye mwenyewe mdogo. Naomba sana Mhe. Spika, hapa ili uweze kufika pahala pazuri tukubaliane mimi na wewe twende vizuri, basi nakuomba Mhe. Spika, hili suala ulikemee na sheria sasa iweze kufuata mkondo wake ili kuweza kuwapa adabu wale wazee ambao wamekuwa wakaidi wa usikivu kwa suala kama hili.

Mhe. Spika, nikiendelea niingie katika masuala ya Idara ya Vyama vya Ushirika. Hivi vyama vya ushiriki kwanza niipongeze idara hii kwamba sasa hivi ina taaluma zake nzuri, kwamba kikundi hakiwezi kusajiliwa mpaka ionekane jinsi gani utendaji wake wa kazi unaendelea vizuri.

Mhe. Spika, maofisa wetu wanazidi kurudi nyuma sana kuvipitia hivi vyama vya ushirika, ili kuweza kuwaelimisha jinsi gani hiki chama kinataka kusajiliwa na kinalenga katika kufanya miradi ya aina gani, kwa sababu kuna wengine huko nyuma tuliviingiza vikundi vyetu kama kwa utashi tu, kwamba tuonekane Waheshimiwa tumesajili vyama vingi, lakini baadae vinakuwa havina kazi yoyote ya kuweza kufanya na mwisho vinavunjika.

Kwa hivyo, naomba idara hii iendelee sana na umakini wa kutoa taaluma halafu baadae ndio waweze kusajili. Vile vile wasikae muda mwingi sana kuweza kwenda kule kunakohusika, kwa sababu wanapoitwa basi wawe watu mahiri sana wa kuweza kufika, la kama hawana vyombo basi naomba wizara iwatafutie vyombo, na kama hawana vespa basi hata hizi baskeli za sehewa nazo laini sana ziweze kuwasaidia ili kuweza kufika kwa wakati mzuri sana.

Mhe. Spika, nikienda katika suala jengine kwa haraka, kwa sababu wizara hii mimi ninakuwa sina makeke nayo sana, kwa sababu mara nyingi huwa nafanya nao kazi kwa karibu, ndio maana unaona narukaruka natafuta zile *point* zilizokuwa mantiki na mimi kuweza kusaidia.

Mhe. Spika, niingie kwenye ukurasa wa 54, katika uimarishaji mashirikiano kati ya Zanzibar na Tanzania Bara na taasisi zake. Mhe. Spika, hapa kidogo ningemuomba mtaalamu wao kwa

sababu maalim Haroun yeye ni mwalimu, akiniambia Tanzania Bara, mimi kidogo ananitia wasi wasi. Hebu naomba kwanza haya maelezo anitafutie lugha iwe nzuri nielewe Tanzania Bara, Zanzibar kidogo ningemuomba anisaidie sana katika masuala kama haya. Lakini kwa kuendelea katika sentensi hii anasema kuwa, kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani leo kimefanyika kikao. Sasa vikao hivyo, nataka niwaombe kidogo niwajue Wazanzibari wangapi nao wanahudhuria katika vikao hivi, ili tuone ni jinsi gani Zanzibar tuna maasi gani.

Kwa hivyo, sisi Wawakilishi wajibu wetu ni kuyafuatilia na kuyauliza. Hii Mhe. Spika, sio haramu sisi kuuliza maswali kama hayo, kwa sababu tunavyoambiwa kwamba tumeungana. Sasa tukiungana basi tuungane kwa mambo yote. Mhe. Spika, hilo sisi tunapata tabu Waheshimiwa Wawakilishi. Mimi naona hilo, ndio maana nikauliza kuwa tunaingiza *master* wangapi kwenye vikao hivi, ili kupata kujua ile *balance* yetu ikoje, kwa sababu watu wengine kwa upeo wao finyu hawaoni wala hawataki kujua, sasa wanaharibu maelezo yetu.

Mimi naomba Mhe. Spika, uwaruhusu watu hao huko nje waje kuchukua *hansard* zetu tunazozizungumza hapa, kwa sababu matamshi yangu siwezi kuyapinga. Hivi sasa yanakwenda moja kwa moja kwenye *hansard*, hili ndio suala ambalo linatupa mashaka sana, wasikae huko vibarazani wakasema maneno yaliyokuwa siyo. Tunachozungumzia ni suala ambalo tunaangalia uwiano wetu ukoje hapa katika vikao hivi, hili ni suala la mambo ya kazi. Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Spika, hilo wapewe ruhusa ili watu waje kuchukua *hansard* zetu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 55, Malengo ya Kamisheni ya Kazi kwa Mwaka. Mhe. Spika, hapa kidogo nitoe pongezi halafu nipambane nako. Ni kweli kabisa wana malengo mazuri kusimamia utekelezaji wa sera za kazi na sera za programu zinazohusu masuala ya kazi, kujenga uwezo katika usimamizi na utekelezaji na mikataba ya kimataifa ya kazi, kuimarisha mifumo ya usuluhisho na uamuzi wa migogoro ya kazi.

Mhe. Spika, hapa mimi nimpe hongera sana Mkurugenzi muhusika, anajitahidi sana tena sana tu. Lakini Mhe. Spika, kitu ambacho kitanisikitisha zaidi, nikiendelea na masuala ya ajira, hii haina tofauti sana kati ya ajira na hii Kamisheni ya Kazi, tofauti yake ni ndogo sana kwa mantiki ambayo ukiiangalia.

Mhe. Spika, Mkurugenzi anastahili sifa, anafanya kazi baada ya saa za kazi. Lakini twende kwa maofisa wake. Maofisa wake Mheshimiwa ndio wanaomfanya yeye aonekane mbaya kutokana na uzorotaji wa maofisa wake. Tunaambiwa tusiwasemee wananchi, lakini hizi ripoti tumezipata kwa wananchi na tutawasemea wananchi. Kwa sababu siku hizi tuna utandawazi, tuseme ukweli, wananchi wetu wanatupigia simu panapotokea tatizo, na sisi tunapopata lile suala huwa tunakimbilia kwa muhusika ambaye ndiye huyo Mkurugenzi, tunakwenda kusokotana naye na anafika pahala anafanya kazi yake kwa uadilifu, anakwenda kunakohusika anatuletea ripoti zinazohusika.

Lakini niseme hivi Mhe. Spika, hebu tuangalie sheria unajua sasa hivi ma-PO wengi sio Wazanzibari, hili tukubaliane nalo, tutafute sheria na halafu tuwe na *limit time* ya kuwa wale ma-PO wawe na muda fulani wanamaliza ili waje wengine, kwa sababu PO anapokuwa kwenye madaraka yale kwa muda wa miaka mingi, ndipo anapokuwa mkorofi, anafanyakazi anapotaka yeye mwenyewe, anajiona yeye bwana mkubwa pale ameshafika. Jamani mabadiliko ya sheria

tuna uwezo wa kufanya hilo suala, kwa sababu tutunge sheria ambayo itaweza kuwasaidia wananchi wetu na kuwaondoa katika hali ya umaskini.

Mhe. Spika, tumetangaza mambo ya utalii yawepo kwa lengo la makusudio mazuri tu, ili vijana wetu waweze kufanyakazi na kuondokana na kukaa vibarazani. Lakini sera ile haimnufaishi Mzanzibari. Hilo mimi nasema Mhe. Spika, na *Wallahi* nitaendelea kusema na nitaendelea kusema tena, sitoogopa chochote, nitasema ukweli ulivyo. Kwa sababu sisi ndio tunaokaa na wananchi, sisi ndio tunaojiwa na wananchi. Jamani kusema ukweli sio dhambi, dhambi ni kutokuitetea haki yako ndio dhambi kubwa, kwa hivyo haki yako hutaki kuitetea unaogopa tu. Mhe. Spika, mimi niko tayari na ninyang'anywe kadi, lakini ukweli nitausema, hakuna tatizo lolote kwa sababu nasema kitu chenye mantiki ambacho kinawaokoa Wazanzibari.

Twendeni tukafanye hesabu, wamo Wazanzibari wangapi mahotelini. Mhe. Waziri mimi niko tayari nitagharamia mafuta gari twendeni tukafanye hesabu Wazanzibari wako wangapi kwenye mahoteli, mimi niko tayari Mhe. Spika, na hili suala nimelisema zamani, sio jana na leo, jamani tuwe na programu maalum, wakati ndio huu sasa hivi wa kusajiliwa hawa ndugu zetu, lakini hili hatulifanyi. Sasa hapa ndipo nitakapozuia kifungu, maalim Haroun hapa nakuomba radhi, hapa mimi nitazuia kifungu. Nipewe hesabu ya Wazanzibari ambao wamo mahotelini ni wangapi. Usajili sasa hivi unaanza.

Mhe.Spika, kuna sehemu ambayo unaambiwa Idara ya Ajira, wanasema hivi, katika hiyo idara ya ajira ya kukusanya taarifa ya wafanyakazi walioajiriwa katika taasisi mbali mbali zilizokuweko Zanzibar. Nakubaliana nayo, lakini sijapata takwimu, nataka nione takwimu ziko wapi. Kuongeza fursa zaidi za ajira kwa wazalendo. Hakusema Mshimba hiyo. Kuongeza fursa zaidi za wazalendo.

Mhe. Spika, leo wananchi wa Jimbo la Kitope Kiwengwa wana mahoteli kibao, lakini hawana fursa ya kupata asilimia kubwa ya kufanya kule kazi na walijitolea kwa nguvu zote, wananchi wa Kiwengwa walifunga njia na walitoa mambo mengi tu. Leo kapige hesabu watu wa Kiwengwa ni wangapi wamo kwenye mahoteli, wanafukuzwa tu bure kwa haki zao. Mtu kwenye ardhi yake mwenyewe inamgeukia. Lengo la kutoa ardhi ili upate utajiri si ndio ilivyo, Mkurugenzi huyo atafanya kazi mara ngapi. Maofisa wako nao wawajibike wamsaidie Mkurugenzi, atafanya kazi hizo mara ngapi, ana mikono kama mungu wa kibaniani kuwa ana mikono huku na huku, haiwezekani Mhe. Spika, ni lazima na yeye apate usaidizi wa watu kuweza kumsaidia. Anafanya kazi nzuri sana huyu Mkurugenzi, lakini anafika pahala na yeye anagonga ukuta, kwa sababu yeye mtu mmoja peke yake tu.

Mhe. Spika, nasema hivi niko *serious*. Juzi nilimwambia kuwa wananchi wangu wa Kiwengwa wamefukuzwa kazi, ardhi yao wenyewe wamefunga njia wao wenyewe, ile neema leo hawanufaiki nayo wanalia kwa umaskini hawapati haki zao kwa nini, halafu naambiwa nisiwasemee. Nitawasemea wananchi wangu, wala sitorudi nyuma, kwa sababu ndio haki yao na mimi ndio haki yangu hapa ndipo pa kusema hapa, siwezi kwenda nje nikapiga kelele kama mpiga ngoma tu, haikubaliki hiyo. Sheria hapa ndiko ninakotunga mimi, na mimi ndiye ninayeona katika jimbo langu jinsi wanavyokufa na umaskini kwa kutopewa haki zao wenyewe.

Mhe. Waziri naamini hilo kwa kupitia Mkurugenzi wako kuwa mtalifanyia kazi kwa uangalifu kabisa. Usajili unafanyika sasa hivi, tena unafanyika kwa nguvu zote. Kwa hivyo, naomba tujipange sasa hivi. Kila wananchi waliokuwa chini ya mahoteli basi tuhakikishe sio lazima asilimia 50, lakini angalau ionekane tu kuwa pale na wao wamenufaika kwa asilimia kuanzia 30 mpaka kuendelea. Kubwa tunaambiwa Wazanzibari hatuwezi kazi za mahoteli. Mhe. Spika, nakataa hichi kitu sio kweli, tumeamka sasa hivi na tuna Chuo chetu kiko pale. Nenda katizame sasa hivi, tuna Chuo kizuri tu kinawaelimisha.

Lakini mimi nataka kutoa rai yangu Mhe. Waziri kwa kupitia kwa Mhe. Spika, kwamba Mhe. Waziri ameshaziruhusu kampuni za binafsi, lakini mimi ningeomba kwamba kuna mipango aipange kwa makusudi ili kampuni hizi nazo wasizisafirishe watu nje, na wa ndani awatafutie kazi, awaite awaelimishe jinsi ambavyo na huku ndani kuwe. Sasa wale wenye mahoteli wakitaka ajira waende kwenye kampuni zile, tutakuwa tumeuondoa mzigo mgumu kwa sababu wananchi wa Zanzibar watapata kazi na wataondokana na umaskini. Kwa hivyo, mimi naomba sana hilo Mhe. Waziri uwaite wale wenye mahoteli, na kuwaambia kwamba hiki kitu tumekisajili kwa mujibu wa sheria, sasa kazi zote wanazozitaka washirikiane, hiyo kampuni ishirikiane na Chuo cha Utalii ili kutoa watu wazuri kabisa na wenye vyeti vyao waende kufanya kazi huko, ni lazima wapitie hapo. Lakini sio leo mtu anakwenda moja kwa moja, Mhe. Spika, huo sio utaratibu hata kidogo

Mhe. Spika: Unazo dakika tano kumalizia.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, zinanitosha. Lakini niseme suala moja, hivi karibuni mimi nimekwenda Austria, kule kuna hoteli moja ambayo ni kijimkahawa tu. Kuna shefa mmoja amefanya kazi pale kinyume na utaratibu. Amedanganya kuwa yeye hakuzaliwa pale, lakini kadanganya kuwa kazaliwa Spain, cheti chake kumbe cha uongo. Kilichojitokeza Mhe. Spika, hoteli ile imefungwa yote na yule mtu akaondoshwa mara moja. Seuze sisi tunaogopa nini hapa Zanzibar, watu wanadanganya vyeti vyao, watu sio wazaliwa wa hapa na vitambuliso mpaka leo wanavyo. Nawashukuru sana Idara ya Vitambulisho wamekwenda kuwanyang'anya na watawanyang'anya wamesema sasa hivi, na nawashukuru sana kwa kazi nzuri waliyoifanya na wanaendelea. Wameshaunda Tume kamili watapita kwenye mahoteli na kuhakikisha suala hilo linafanyika, nawapa pongezi sana kwa kuwa wasikivu. Lakini pamoja na nyinyi muungane nao kwa kuifanya kazi hiyo.

Mhe. Spika, sitaki nipoteze muda wako kama nilivyosema. La mwisho Mhe. Spika, nije kwenye Mahakama yetu ya Kadhi, Mheshimiwa isaidie sana mahakama yetu. Niwashukuru sana wamehukumu kesi vizuri sana. Hata yule mwanamama aliyedhalilishwa nasikia amepata pesa nzuri, lakini kwenye utu kwa milioni tatu, lakini hata hivyo si haba *Alhamdulillah*, nimesikia tayari wale Kampuni ya *Residence* kule wameshalipa, ninawashukuru sana na yule jamaa aliyefanya kitendo kile ameshafukuzwa kazi, hivi ndivyo tunavyotaka niwashukuru sana.

Kuna kesi nyengine ilifanyika kule hoteli ya mjini niliyoisahau jina. Kuna dada mmoja ambaye alifukuzwa kazi, lakini mahakama imehukumu na hoteli ile kule mjini ambayo nimeisahau jina. Mhe. Spika, na wao pia wamefanikisha mahakama imehukumu na amepata pesa zake, hivyo ndivyo tunavyotaka. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba sana kwamba mahakama yako uiwezesha

vizuri, ili kesi zisirundikane. Pale unaye jaji mzuri wala hapendelei huku wala huku anafuata sheria kwa mujibu wa taratibu na haki zake.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba suala hili la kuwatafutia haki Wazanzibari tuliwekee kipaumbele, kwa sababu sote tuna haki ya kuyatetea maslahi ya Wazanzibari na kuwapatia fursa kwa mujibu wa katiba. Tunachozungumza sisi ni kwa mujibu wa katiba. Sisi wengine tukisema ukweli wanatuona kama hatuupendi. Lakini mimi Mhe. Spika, naupenda sana Muungano, na kauli yangu nasema Muungano tuwe na marekebisho ya kuleta uchumi kwa maslahi ya Wazanzibari. Hiyo ndio *Hansard* yangu na nitaendelea kusema hivyo. Nitatetea haki za Wazanzibari kuwatafutia haki zao kwa mujibu wa katiba, sitogeuka wala sitovunja kanuni za chama. Nitafuata utaratibu wa katiba ya serikali na nitafuata kanuni za chama vile vile zinavyotueleza katika itikadi hizo za chama, sitokiuka hata kidogo, haki ya Mzanzibari wajibu wangu kutetea, nitaitetea sana.

Mhe. Spika, hukusema kuwa tupelekwe kule na sisi tukadai fedha zetu sio kosa, kwa sababu ni haki yetu. Inawezekana mimi leo nikaja kutangazwa kuwa Naibu Waziri, si nimeshaingia na mimi huko huko, ndio nikasema hivyo, inakuja hiyo Mhe. Spika. Ahsante sana kwa hayo machache, nitaunga mkono baada ya Mhe. Waziri wangu kuja kunipa mambo mazuri. Lakini nashukuru sana, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii. Vile vile naomba nimshukuru Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, maalim wangu Maalim Haroun Ali Suleiman kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake, ambayo imepangika vizuri na maelezo yake fasaha, yanajieleza vizuri na unaelewa nini alichokusudia kukifanya yeye na watendaji wake, nampongeza sana mwalimu wangu kwa hilo.

Mhe. Spika, kama kawaida naomba kabla sijaingia kwenye maudhui ya hotuba, kuna vifungu hivi naomba akija Mhe. Waziri anisaidie maelezo ya matumizi katika hili buku la mswada wa makadirio ya mapato na matumizi.

Mhe. Spika, kwanza ningeomba maelezo katika Ofisi Kuu Pemba, kwenye ukurasa wa 444 wa buku hili, kwenye vote 220408 gharama za umeme, ambapo mwaka huu zimetengewa shilingi 30,414,000 ukilinganisha na shilingi milioni 2,400,000 za mwaka jana. Kwa hivyo, nilikuwa naomba anieleze ni kwa nini fungu hilo limepanda kwa kiasi hicho.

Vile vile Mhe. Spika, kuna vile vifungu vya kawaida katika idara zote naomba maelezo. Mfano Idara ya Mipango Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Ajira, Idara ya Mikopo na Idara ya Ushirika zote kwa jumla, juu ya suala la kuwa na posho maalum fungu ambalo tayari limesheheni vizuri tu, lakini na baadae kunakuwa na posho la vikao na kamati, nalo likiwa limenona kwa kiasi hiki ambacho limenona, sina haja ya kuzitaja idara moja moja kwa sababu kama nilivyosema vinajirejea katika idara zote, naomba katika idara zote akija anipe maelezo.

Mhe. Spika, pia katika fungu la viburudishaji vile vile inaonekana kama kawaida kunakuwa na ongezeko kubwa ukilinganisha mwaka jana na mwaka huu katika idara nyingi, naomba maelezo,

ikiwa ni katika Idara ya Mipango Sera na Utafiti, Idara ya Uwezeshaji na Utumishi na idara nyengine vile vile.

Lakini Mhe. Spika, fungu la safari pia linaendelea kuwa limenona katika maeneo mengi. Naomba vile vile akija Mhe. Waziri anisaidie maelezo katika idara mbali mbali. Mhe. Spika, ukiondoa hayo ya jumla ambayo yanajirejea kila pahala, yako mengine yaliyokuwa mahususi haya pia naomba maelezo yako kwenye idara moja moja tu.

Kwa mfano Mhe. Spika, katika fungu la Idara ya Uendeshaji na Utumishi, kwenye ununuzi wa magazeti na majarida kwenye ukurasa wa 448, umeongezeka kutoka shilingi 4,778,000 mwaka jana hadi kufikia milioni 12,900,000 kwa mwaka huu. Kwa sababu siamini kwamba magazeti yamepanda bei kwa kiasi hiki ambacho ongezeko hili linaonekana. Pia nilikuwa naomba maelezo mahususi katika idara hii ya uendeshaji na utumishi katika fungu la 220800 kuhusu matengenezo ya zana. Mhe. Spika, hapa kuna ongezeko kubwa sana kutoka shilingi milioni 7,840,000 mwaka jana hadi shilingi 53,000,000, mwaka huu. Kuna matengenezo ya zana 36 milioni, kuna matengenezo ya gari 13 milioni na halafu kuna gharama za Bima milioni 4. lakini fungu hili ni tofauti mno na lilivyokuwa mwaka, nilikuwa naomba maelezo.

Mhe. Spika, vile vile katika maeneo mahususi naomba maelezo katika idara ya mikopo, hii kidogo nimestaajabu. Idara ya Mikopo imeandikwa ni idara, lakini hapa imeombewa ruzuku, haina maelezo ya vifungu kama ilivyokuwa idara nyengine, kuna ruzuku kwenye mishahara na ruzuku kwenye uendeshaji kama vile ilivyokuwa mashirika au taasisi zinazojitegemea. Sasa nashangaa kwa nini idara iitwe idara halafu ina utaratibu huu wa bajeti. Naomba Mhe. Waziri akija anipe maelezo katika hili.

Mhe. Spika, sasa tofauti na kule kwenye Idara ya Utumishi na Uendeshaji ambapo fungu la matengenezo limenona, nikiiangalia Idara ya Usalama na Afya kazini kwenye ukurasa wa 453 kwenye hili buku la makadirio katika matengenezo ya zana, kuna ziro mwanzo mpaka mwisho, wakati mwaka jana palikuwa na milioni 10,990,000, kwa hivyo nikawa najiuliza hizi zana zimeondoka mwaka huu mzima Waziri kakusudia kwamba hategemei kutengeneza chochote, yaani kufanya matengenezo, kidogo nimeshindwa kuelewa. Kwa hivyo, naomba maelezo katika suala hili.

La mwisho kabisa katika vifungu Mhe. Spika, naomba niende katika Idara ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kwenye ukurasa wa 456 wa buku hili la makadirio. Kwa hapa nataka niwapongeze kwa sababu fungu la safari ni tofauti na mule mwengine limepungua. Mwaka jana ilikuwa shilingi milioni 29,765,000 na mwaka huu limekuwa shilingi milioni 5,740,000 nawapongeza sana kwa uzalendo wao. Ninachoomba maelezo hapa ni kwamba mwaka jana inaonekana tuliidhinisha milioni 22,050,000 kwa safari za nje kwa Idara hii ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija anisaidie tija ya fedha hizi milioni 22,050,000 tulizoziidhinisha, ziliingizwa ngapi katika fungu hili na hizo safari zilizokwendwa zimeleta tija gani katika nchi yetu. Naomba hili Mhe. Spika, akija waziri anisaidie.

Mhe. Spika, nikiondoka katika vifungu, naomba sasa nije katika maudhui ya wizara. Mhe. Spika, mimi bado nina *observation* moja ya jumla, naomba niiseme kabisa. Siku nilipokuwa

nikichangia bajeti ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto, nilisema sioni kama kuna tofauti kubwa ya kazi zinazotendwa na wizara hizi mbili. Nilisema kwamba ninapata wasiwasi kwamba matokeo yake shughuli zinazofanana zinatengewa bajeti mbili tofauti, halafu zilizokwenda kwa wananchi sio tatizo, lakini kuna uwezekano hapa Mhe. Spika, nilisema kwamba mwananchi anaweza kwenda katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika akienda kuomba msaada na akienda tena katika Wizara ya Ustawi wa Jamiii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto akienda kuomba fedha, kwa sababu hawatambuani vikundi vile viwili ikawa mwananchi yule anafaidika, kwa sababu hazijawekwa katika wizara moja ikawa inasimamia jukumu hilo.

Lakini zaidi Mhe. Spika, ni suala zima la gharama za utawala, ukiunda wizara na maidara yake, hayo yote yanachukua gharama kubwa za utawala, kama unavyoziona hapa. Kwa hivyo, ingekuwa zimewekwa chini ya wizara moja, basi ingetusaidia mno kwamba tungepunguza sana gharama za utawala na pengine fedha zile zingepelekwa huko kwenda kuwawezesha wananchi kiuchumi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nafahamu kama jukumu hili ni la Rais, wajibu wake uko kikatiba na Waziri nitakuwa namuonea tu kwa sababu yeye siye anayepanga wizara. Lakini hapa ndio pahala petu pa kuiambia serikali kwa ujumla.

Kwa hivyo, mimi nadhani bado Mhe. Rais aone na afanye uchambuzi zaidi kwamba je, kuna haja ya kuendelea kuzitenganisha wizara hizi mbili kama alivyofanya baada ya uchaguzi, ili kuzinusuru fedha za walipa kodi.

Mhe. Spika, baada ya hayo ya jumla. Sasa naomba niende katika yale mambo ambayo yanasimamiwa na Wizara hii. Mhe. Spika, ukitizama mambo ambayo yanasimamiwa na yaliyozungumzwa katika hotuba hii, mengi yanategemeana mno. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri hebu anapokaa na wenzake walizungumze suala la Mapinduzi, kwa sababu tunaweza tukambebesha kazi kubwa maalim wangu Mhe. Haroun Ali Suleiman, lakini kama kuna idara nyengine hazifanyi kazi yake, ikawa kazi yake inakuwa ngumu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, kazungumza ajira za watoto hapa katika ukurasa wa 13 wa kitabu chake. Hebu tujiulize, kwa nini ajira za watoto zinaongezeka katika nchi yetu, ni kwa sababu wananchi wetu wanaendelea kuwa maskini, hawana njia ya kujitosheleza kwa mahitaji yao. Kwa hivyo, inafika pahala badala ya mtoto kumpeleka skuli akasoma, anapewa biashara ndogo ndogo akafanye ili asaidie kipato cha familia. Sasa ingekuwa Mhe. Spika, tuna utaratibu mzuri wa kuwaongezea kipato wananchi wetu kwa kuwaongezea ajira, na kuwa na ajira zenye stara na heshima kama anavyopenda kuziita Mhe. Waziri wa wizara hii, nadhani ingekuwa moja kwa moja inapunguza tatizo la ajira za watoto. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kusema kwamba kuna maeneo ambayo nadhani tunahitaji kuyafanyia kazi.

Kwanza ni suala zima la kupata ajira na kuweka nafasi za kazi. Kuna lile suala moja ambalo Mhe. Waziri alituambia la nafasi za kazi nje ya nchi. Mimi ningemuomba bado Mhe. Waziri hili alitazame tena, mara nyingi tumekuwa tukimuambia. Mhe. Waziri alituambia hapa kwamba alifanya juhudi kubwa sana yeye ya kwenda kutafuta kazi katika baadhi ya nchi za kiarabu. Lakini baada ya kuwa mambo yamekamilika wenzetu upande wa pili wakaingia wao mkataba, kwa hivyo ile kazi nzuri aliyofanya Waziri wetu ikaenda ikanufaisha upande mwengine. Pengine kwa sababu ya utamaduni na kwa sababu ya maingiliano ya kihistoria, hizi nchi zingeweza

kuajiri vijana kutoka Zanzibar, lakini tumezikosa. Kwa hivyo, tunarudi pale pale tunakwenda kubembeleza kwa yule ambaye yeye kazipata baada ya Waziri wetu kufanya kazi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri alitazame.

Zaidi mchango wangu katika hili Mhe. Spika, uko katika nafasi za kazi za ndani. Nilisema mapema hapa Mhe. Spika, kwamba inawezekana Mhe. Maalim Haroun akawa anajitahidi sana, lakini kama sehemu nyengine hazifanyi kazi yake tutakuwa tunamkwamisha. Mimi sidhani kama tunategemea tuzalishe ajira kwa kuunda vikundi vya ushirika tu na kwenda kutafuta *SACCOS* na *ZASOZE*, mimi siamini Mhe. Spika. Mimi naamini waziri wetu angependa sana uje uwekezaji wa maana katika nchi yetu, ukazalisha ajira za maana zikawaongezea ujuzi na uwezo wananchi wetu, wakapata kipato kinachowaridhisha. Sasa Mhe. Spika, mara nyingi nimepiga kelele. Kuna miradi mingi mikubwa imeletwa mapendekezo yake, tangu serikali ya awamu ya saba imeingia madarakani na mawaziri wanalifahamu hilo. Lakini kumekuwa kuna urasimu wa ajabu katika kushughulikia miradi hii. Wawekezaji wengine mpaka wameamua kuondoka.

Mhe. Spika, naujua mradi mmoja ambao ulikuwa unagharimu, ni wa masuala ya ujenzi wa nyumba hizi, ambapo ungebadilisha mandhari ya mji kabisa. Gharama za chini alizozikisia mwekezaji ni dola milioni 100. Sasa huu mradi ungekuja katika masuala ya ujenzi, huduma pale na ukishakamilika ukatoa ajira. Lakini mpaka leo, unakaribia kuingia mwaka wa pili Mhe. Spika, bado serikali haijafanya maamuzi. Sasa huu urasimu uvunjwe.

Kuna miradi tulitajiwa hapa Mhe. Spika, ya uwekezaji katika bahari kuu na sisi ni visiwa tumezungukwa na bahari. Mradi umekuja, maamuzi yanashindikana kufanywa. Kuna watu wametaka kujenga maduka makubwa makubwa, kwa sababu wangepata ajira watu wetu mule, lakini maamuzi mpaka leo yamekwama Mhe. Spika. Kuna miradi mingi sana wala siimalizi hapa, lakini bado kuna tatizo la urasimu. Kwa hivyo, nasema hili tutakuwa tunamuonea bure Mhe. Waziri, kwa sababu pengine mamlaka inayohusika na kuruhusu wawekezaji inakwamisha, kwa hivyo zile ajira haziji na Mhe. Waziri tulompa kazi ya kuzitafuta hizo ajira na kuzisimamia hana kazi, isipokuwa anategemea kusubiri *SACCOS* na *ZASOZE* na kuwezesha Mikopo ya AK na JK. Mhe. Spika, suala hili nasema bado serikali inapaswa ijipange vizuri.

Mhe. Spika, katika hili kuna miradi imetajwa hapa, na mimi nilikuwa nadhani serikali itizame na ninashukuru Mhe. Waziri ameliona na ametaja hapa habari ya Miradi ya Kilimo, Uvuvi pamoja na Maliasili. Mhe. Spika, mimi naamini katika Maliasili amekusudia pia pamoja na maliasili ya mafuta na gesi asilia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tulisema hapa kwamba kila tukijichelewesha sisi katika kuchukua hatua katika hili tunajikosesha fursa nyingi sana Mhe. Spika. Kwa hivyo, nilikuwa nasema tena nadhani vijana wetu wengi wanazikataa kazi kwa mfano za kilimo, kwa sababu hawajaoneshwa kwamba kuna uwezekano wa kufanya kilimo cha kisasa ambacho si lazima ukashike jembe la mkono kama walivyozoea.

Mhe. Spika, je wizara katika hili iniambie imejipanga kiasi gani kushirikiana na Wizara na sekta zinazohusika katika kuwapanga vijana wetu na kuwapa elimu pamoja na mafunzo, na kuwaonesha kwamba unaweza ukawa mvuvi au mkulima wa kisasa. Kwa mfano, kuna miradi

ambayo imefanywa na wametoka watu mjini wanaisimamia na ndio wanaoiendesha miradi ile, kama vile Kilimo cha Umwagiliaji wamewekeza pale fedha nyingi na wameajiri watu wengine.

Sasa miradi kama hii inatakiwa iwe mingi Mhe. Spika, kwa ajili ya kuzalisha ajira nyingi, hili naomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie, yaani wamejipanga vipi katika suala hili?

Lakini katika hili Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri aje anisaidie kitu kimoja, miradi kama hii mara nyingi inajikita katika ile miradi tunaiita *Small and Medium Enterprises (SMES)*. Mhe. Spika, Benki Kuu ya Tanzania ambayo ni chombo cha Muungano tunavyoambiwa ilikuja na *Program* Maalum ya ku-*sponsor* benki zilizopewa leseni na Benki Kuu kuweza kutoa mikopo ya aina fulani kwa watu wanaotaka kuwekeza katika sekta kama hizi Mhe. Spika.

Kwa kweli benki hizi ziko za Bara na Zanzibar na nyengine zina matawi hapa, lakini kila mzanzibari akenda hapati mikopo hii. Mhe. Spika, mimi ninalo *file* ofisini kwangu la kijana mmoja wa Mji Mkongwe ambaye amefanya mradi ambao tayari ule mradi thamani yake akeshakuwekeza yeye ni takribani shilingi milioni 300 mradi wa kilimo na ufugaji pamoja.

Sasa anataka kuupanua ili apate kuajiri watu wengi zaidi pamoja na yeye ajiongezee tija, ametumia fursa iliyotangazwa na *BOT* mpaka amechukua na Gazeti la *The Guardian* ambalo limetangaza, lakini alipokwenda benki anahudumiwa na wala hapati mkopo, aliuliza kimepungua nini katika masharti yenu haya na wala hakuna alichokipata.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, suala hili alifuatilie na tutaendelea kukosa haki zetu kila siku. Sasa haya ndiyo yanayowafanya wananchi wetu wakafika pahala wakasema wanataka kupumua Mhe. Spika, kwa sababu wanaona kila fursa inayokuja inanufaisha upande mmoja na upande wa pili hainufaishi, wakati hizi tunasema ni taasisi za Muungano.

Mhe. Spika, pia namuomba Mhe. Waziri ajiangalie pamoja na kuiangalia Wizara yake katika suala la kusimamia haki za wafanyakazi. Mhe. Spika, niliwahi kusema hapa Mhe. Spika, kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi ambao ni vijana wa kizanzibari wanalalamika kuwa wanafanyiwa visivyokuwa ndivyo katika maeneo yao ya kazi zinakiukwa sheria zao za kazi na kuja kuripoti katika wizara ya Mhe. Waziri.

Lakini baadaye kunatoka mawasiliano katika wizara kwenda kwa wale wenye mahoteli ambao wameajiri wale na kuwauza wale vijana kwamba fulani amekuja kuripoti hapa. Kwa hivyo, matokeo yake badala ya kuhudumiwa anafukuzwa kazi na kumalizwa kabisa. *(Makofi)*

Sasa hili namuomba Mhe. Waziri alitizame vizuri katika wizara yake, kuna nini hapo na vijana Mhe. Spika wanatuhumu kwamba kuna rushwa, kwamba kuna watu ambao wameekewa mishahara kwenye hoteli za pembeni na kazi yao kuhujumu haki za wananchi wengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapo hapo nizungumzie kuhusu haki za wafanyakazi na limezungumzwa hapa suala la ajira katika Kampuni ya *ZANTEL*. Mhe. Spika, niliwahi kumwambia Mhe. Waziri mwaka jana hapa, na kuniahidi atalifuatilia na kwa muda mrefu nimeliacha, isipokuwa siku moja nililiuliza

katika maswali ya nyongeza hapa na kuliacha, lakini Mhe. Spika nasikitika kwamba suala hili bado halijafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, karibu ya siku ya kuja kutoa hotuba ya bajeti hapa wale wafanyakazi wameitwa wale waliokuwa walinzi na kuambiwa wajazishwe mikataba. Lakini mikataba ile ninayo hapa *sample* ni tofauti na ile waliyopewa wenzao, wao wamekuja na hichi kima cha chini ambacho amekitaja Mhe. Waziri cha shilingi 145,000/=, wakati wenzao ambao waliopewa ajira kama hizi na wamenilitea *sample* za mikataba hapa, wengine wanalipwa shilingi 368,000/= wengine shilingi 670,000/= na ile ile kuna *double standards* baina ya wafanyakazi wa *ZANTEL* walioko Bara na hapa Zanzibar.

Kwa kweli kampuni hii ni ya wazanzibari, yaani Serikali ya Zanzibar ina hisa katika kampuni hii, yaani inahudumiwa kwa kiasi fulani na fedha za walipa kodi, lakini leo inawanufaisha wa mbali, imegeuka kivuli cha mvumo na hawa waliochini ya mti hawanufaiki Mhe. Spika. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja anipe maelezo ya kina.

Vile vile kuna fursa za posho mbali mbali walitakiwa wazipate hawa, lakini wao wameambiwa katika mkataba mpya wasaini ile shilingi 145,000/= na zile fursa zote zimeondoshwa na Mhe. Waziri akitaka nitampa aone hii mikataba imekuwa inatofautiana.

Mhe. Spika, suala hili kama sijapata maelezo sitaipitisha bajeti ya wizara hii, kwa sababu kama ninavyosema suala limechukua muda mrefu na wala siridhiki kwa kampuni ambayo Serikali ya Zanzibar ni mmoja wa wamiliki, lakini ikawa wazanzibari wananyanyaswa.

Nikiendelea na hiyo Kampuni ya *ZANTEL*, nimuombe Mhe. Waziri afuatilie eneo jengine sasa na hili ni la vijana walioajiriwa katika inaitwa *Core Centre*. Mhe. Spika, kuna vijana 139 ambao wameajiriwa katika *Core Centre*, na hawa waliajiriwa baada ya *ZANTEL* kuwasiliana na *Zanzibar University* na wakaingia nao mkataba kwamba wawapatie vijana wale na wanafanya kazi ile.

Lakini jambo la kustaajabisha ni kwamba, mpaka leo bado hawajapewa mkataba, wakiuliza hawajijui kama wameajiriwa na *Zanzibar University* au *ZANTEL*, yaani kote hawana mikataba na yale makubaliano yaliyoingiwa baina ya *ZANTEL* na *Zanzibar University* wao hawayaelewi.

Lakini zaidi Mhe. Spika, ni *double standards* ile ile katika malipo, wenzao walipokuwepo Bara *Core Centre* Mhe. Spika, walikuwa wakilipwa shilingi 3,000/= kwa saa, hawa walipohamishiwa Zanzibar wazanzibari wanalipwa shilingi 1,200/= kwa saa. Sasa wanajiuliza hivi kwa nini mzanzibari kila siku anaendelea kudhalilika katika nchi yake, tena kwa kampuni ambayo anailipia gharama zake kwa sababu ya zile kodi anazozilipa.

Mhe. Spika, hata Sheria za Kazi hazifuatwi na Kampuni ya *ZANTEL*, watu wanaachishwa kazi ovyo bila ya kufuata taratibu, kuna vitisho katika kazi wakidai haki zao, wanaambiwa *Core Centre* itarejeshwa Dar-es-Salaam wakose ajira, kutopatiwa huduma muhimu za kazini. Kwa mfano, wenzao wakati *Core Centre* ilipokuwa Bara walikuwa wakipewa kama *motivation*, yaani muda wa maongezi fulani, chai, ilipohamishiwa Zanzibar zote zimekatwa hizo.

Lakini Mhe. Spika, kwa sababu uongozi wote umeshikwa na watu kutoka upande wa pili Mrima huko, kwa hiyo hata wanapotoa malalamiko yao hayashughulikiwi. Mhe. Spika, najua unanitizama namalizia. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie ufafanuzi.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tano.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie maelezo ya kina.

Vile vile nimalizie hilo kuhusiana na utaratibu wa mikataba, kwamba wengine wamepewa kujaza mikataba ya muda. Kwa mfano, walipewa mkataba wa miezi sita kutoka tarehe 15/08/2009 mpaka 14/02/2012, na halafu hivi sasa wamepewa mwengine wa tarehe 01/07/2012 mpaka 31/12/2012.

Mhe. Spika, huu si utaratibu mzuri na Mhe. Waziri aliahidi kulifuatilia hili, hivyo naomba maelezo ya kina na kwa nini nipitishe bajeti baada ya kushindwa kusimamia haki za vijana wa kizanzibari ambao wanaofanyakazi katika Kampuni ya *ZANTEL*. Mhe. Spika, naomba sana suala hilo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba niungane na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ajira katika Sekta ya Utalii. Kwa kweli Sekta ya Utalii ndio sekta Kuu ya Uchumi kwa Zanzibar hivi sasa, na wengi wanategemea ajira katika sekta hii.

Lakini kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwamba vijana wetu hawapati ajira, na siku ya kupitisha Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kamisheni ya Utalii hapa Mhe. Spika nilitoka nje wakati tulipokuwa tunapitisha vifungu hapa, kwa sababu ya kushindana juu ya kifungu ambacho tulitaka kipaumbele wapewe wazanzibari.

Sasa nimeheshimu demokrasia, kwa sababu walio wengi waliamua kwamba kibakie kipaumbele kiwe kwa Mtanzania badala ya kuwa Mzanzibari, lakini tuliahidiwa hapa na serikali kwamba katika Kanuni itawekwa kuwa Mzanzibari apewe kipaumbele kwa zile nafasi ambazo wazanzibari wanapatikana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja aniambie amelisimamia kiasi gani katika kuona sekta hii muhimu katika uchumi wetu wa Zanzibar inawafaidisha Wazanzibari.

Mhe. Spika, katika hilo la utalii kuna ajira zinazotokana na Sekta ya Utalii, ambazo hazipaswi kufanya waliokuwa si Wazanzibari. Kwa mfano, sheria zetu zinataka mambo ya Watembezaji Utalii *(Tourist Operators)* zifanywe na wenyeji Wazanzibari. Lakini hizi kuna wamiliki wa holeti wageni kutoka nje ya Tanzania na hata kuna kampuni kutoka nje ya Zanzibar zinazotoka Bara zinafanya kazi hizi, kwa nini tunashindwa kusimamia ili ajira hizi zibaki kwa Wazanzibari.

Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Mji Mkongwe kule kumechafuka na maduka ya Tinga tinga na Vivyago. Sasa Mhe. Spika, kwanza huu si utamaduni wetu, lakini hawa kwa sababu wanazalisha kwa wingi na gharama zao zinakuwa ndogo. Kwa hivyo, wanauza vitu vyao kwa bei

ya chini ambayo inaua Sanaa za Zanzibar, na pamoja na Kazi za Mikono zinazofanywa na Wazanzibari.

Matokeo yake ajira hii na mapato haya yanavuka bahari na kwenda kunufaisha wengine badala ya vijana wetu sisi, na hapa tunazo kazi zetu za mikono Mhe. Spika, kama vile Sanaa za Kuchora tunao wachoraji wazuri sana hapa, tena nina hakika Mhe. Waziri anawatambua Wazanzibari wengi.

Kwa hivyo, tunawafanya nini katika kusimamia ajira kama hizi, ili kuona vijana wetu wanafaidika, pia Mji Mkongwe unanusurika kuwa Mji wa Vinyago na Tinga tinga na urejeshe katika sifa yake ambayo ulikuwa nayo katika Sekta ya Utalii.

Mhe. Spika, kwa haraka nataka kumpongeza Mhe. Waziri katika hili ambalo nimelisema kwamba alifanya kazi na Jumuia ya *Zanzibar Drugs Free* katika kushiriki kwenye Maonesho yake ya Kazi zao za Mikono. Mhe. Spika, hawa ni vijana ambao wanaacha na utumiaji wa dawa za kulevya na wanataka kuingia katika jamii wakiwa ni wazalishaji. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri kwamba aendelee kuwatizama, kwa sababu hawa akiwasaidia na wala hasaidii ajira tu, lakini anawasaidia kuondosha vishawishi vya kurejea kutumia dawa za kulevya, naomba wizara yake iendelee kuwatizama sana.

Jambo la mwisho Mhe. Spika, dakika moja tu, ambalo linahusu Vikundi vya Ushirika vya kujitolea ambavyo baadaye vinaajiriwa. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili alifuatilie kwa makini, ikiwa yeye mwenyewe au watendaji wake ama vipi.

Lakini kuna malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kwamba bado kuna upendeleo wa kisiasa, inawezekana si kwa nia ya makusudi, lakini tunahisi kipaumbele kinatolewa kwa vikundi vinavyotoka katika upande fulani na hivi sasa tumekuja na Mfumo wa Umoja wa Kitaifa, na tunataka tuone wananchi wote wanatendewa haki sawa na kupewa fursa sawa.

Mhe. Spika, wapo vijana wanaojitolea kama vile hao wa *ZASOZE* katika mambo ya usafi wa mazingira, lakini hawapewi fursa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, suala hili alifuatilie.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba nitaunga mkono hoja Mhe. Waziri wa wizara hii ni mwalimu wangu amenisomesha kabisa ameshika chaki wakati mimi niko darasani Mhe. Spika. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja anipe maelezo kuhusu suala la Kampuni ya ZANTEL, ili nimpitishie bajeti yake kwa sababu kama si hivyo patakuwa na mbinde na Mhe. Spika nakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa tumkaribishe Mhe. Abdi Mossi Kombo.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Mhe. Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa fursa hii leo ya kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais kwa kumchagua Mhe. Rashid Seif Suleiman kukamata kiti cha Uwaziri wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. *(Makofi)*

Vile vile nampongeza Mhe. Hamad Masoud Hamad, ambaye alikuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kwa uamuzi wake wa kujiuzulu kwa hiari yake, ili kuweka nafasi vizuri na kujiwekea nafasi nzuri pamoja na kujijengea heshima katika taifa letu hili la kimaendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika mchango wangu kwenye kitabu hichi ukurasa wa 28 Idara ya Uendeshaji na Uratibu wa *Program* za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mhe. Spika, nchi yetu ya Zanzibar hivi sasa ina vijana pamoja na wananchi wengi, ambao bado wako nyuma kiuchumi.

Kwa hivyo, tunaiomba serikali kupitia wizara hii, kwamba vijana wengi wanahitaji kuelimishwa kiuchumi na kupewa mikopo kwa ajili ya kujiendesha. Kwa mfano, nchi zote za dunia hivi sasa zinagombania uchumi, elimu, kwa sababu elimu ya kiuchumi wananchi wetu wa Zanzibar hawajaipata, pia serikali bado haijawawezesha wananchi wa Zanzibar.

Katika dunia kuna nyanja nyingi sana za kuweza kuchumishwa wananchi. Kwa mfano, tunazo hoteli pamoja na Sera za Hoteli, lakini bado wananchi wa Zanzibar hawajapewa kipaumbele ya kuwezeshwa kuwekeza hoteli kama wenzetu, yaani bado Zanzibar wawekezaji wote ni wazungu, kwa nini serikali haiwawezeshi wananchi na kuwakopesha fedha kwa ajili ya kuwekeza. Kwa mfano, tunao vijana wengi sana hivi sasa ambao wanaweza kufanya kazi, lakini serikali bado haijawatizama.

Vile vile kuna akinamama wengi sasa ambao wanaweza kufanya kazi, lakini serikali bado haijawatizama, pia kuna walemavu bado hawajapewa kipaumbele. Kwa mfano, kwenye majimbo yetu ya mashamba kama vile Matemwe wako walemavu pamoja na vijana, lakini bado hawajapewa kipaumbele katika kuwezeshwa.

Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia Wizara yetu hii ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kwamba waende makusudi hasa kuwakusanya vijana, ili kuwakopesha fedha au zana za kuweza kujiendesha, kwa sababu bila ya kuwapa zana wananchi za kujiendesha basi hawawezi kujiendesha. Kwa maana hiyo, naomba serikali kupitia wizara yetu hii iwafikirie sana wananchi kuwezeshwa. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu kuhusu suala la uwezeshaji, pia kuna wafanyakazi ambao bado na wao hawajawezeshwa kiuchumi. Kwa mfano, kwenye sehemu za mahoteli kuna matajiri ambao wanawanyanyasa vijana, wanawanyima mishahara yao, kama vile nyongeza zilizoongezwa hoteli nyengine bado hawajapewa. Kwa hiyo, naiomba wizara ifuatilie sana zile hoteli ambazo vijana hawajapewa mishahara yao, wangali wananyanyaswa na wawekezaji.

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie suala la mikopo. Kwa kweli mikopo wanayopewa wananchi bado ni midogo kwa ajili ya kujiwezesha na wala haijakidhi haja. Kwa hivyo, naiomba wizara iwaongeze wananchi mikopo.

Mhe. Spika, bila ya kuchukua muda wako Mhe. Spika, ninavyojua kwamba wananchi wanahitaji elimu, mikopo pamoja na ajira, kwa sababu vijana wengi hawana ajira, ambao wamesoma lakini hawapati ajira. Kwa mfano, sehemu za mahoteli vijana wa Zanzibar wengi hawapati ajira wanaambiwa hawakusoma sijui kule hoteli kunataka elimu gani. Kwa hiyo, wizara iangalie sana vijana tuliokuwa nao na sehemu zetu tumezungukwa na bahari, ambayo ina samaki.

Kutokana na hali hiyo, Wizara yetu ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika iwanunulie boti vijana wawape, ili waweze kuvua samaki kwa uhakika.

Mhe. Spika, nikiendelea katika suala la uwezeshaji. Hivi sasa tuko katika dunia ya *science and technology*, yaani kila nchi inahitaji iwe na uchumi, viwanda na hii nitakuja kusema wakati wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Lakini katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika inayo haki ya kujenga viwanda na kuwakopesha wananchi Viwanda Vidogo Vidogo na huko ndio kuwezesha, bila ya kuwajengea viwanda wananchi na kuwapa au kuwakopesha viwanda vidogo vidogo, basi bado wananchi watakuwa wanahangaika tu hawana ajira.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza muda wangu mimi nitakomea hapa. Lakini naiomba serikali iwaangalie vijana, kwa sababu hivi sasa wako wengi tena wamesoma, lakini bado vijana wakienda kwenye maidara yale ya kuwezeshwa kazi wanaambiwa mmm! Anatizamwa na kuulizwa wewe Bin Kinana na kama si Bin Kinana hupati kazi, kwa nini? Kwa hivyo, tuache na tuwaangalie pamoja na kuwawezesha vijana pamoja na wananchi.

Mhe. Spika, ahsante sana na kwa ruhusa yako naomba kukaa kitako. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Mhe. Nassor Ali Salim.

Mhe. Nassor Ali Salim: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ndogo ya kuweza kuchangia Hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Kwanza Mhe. Spika, nichukue fursa hii ya kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea hotuba hii nzuri iliyopangika yenye matarajio mema huko mbele. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, naomba nizungumze machache na nianzie kwenye ukurasa wa 35 kuhusu Idara ya Mikopo. Mhe. Spika, kwenye idara hii ambapo Mhe. Waziri ametueleza kwenye kitabu chake hichi, kwamba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, wizara imejipangia kutoa mikopo 1000 kwa Vikundi vya Kiuchumi na Watu Binafsi pamoja na Wajasiriamali Mmoja Mmoja.

Mhe. Spika, ukirudi nyuma katika mwaka wa fedha 2011/2012, wizara hali kadhalika ilikuwa na mpango huo wa kuwezesha kama ambavyo ameeleza kwenye kitabu hichi. Lakini mikopo ambayo imetolewa katika mwaka huu wa fedha 2011/2012 na waliofaidika na mikopo ile ni 195, kwa upande wa Unguja ni 130 na Pemba 65.

Sasa wasi wasi katika kipindi hichi cha mwaka 2012/2013 wizara itakuwa imejipanga vipi kuweka mikakati kuhakikisha kwamba lengo na madhumuni yanatimia na wananchi kuweza

kupata mikopo ile, ili kuweza kujikimu kimaisha pamoja na kuendeleza kuijenga nchi yetu katika kuleta maendeleo kwa taifa letu.

Mhe. Spika, katika mikopo hiyo kwenye taarifa ya kitabu hichi Mhe. Waziri ametueleza kwamba kwenye maelezo ambayo yamo katika kiambatanisho, Mkoa wa Mjini Magharibi ni kikundi kimoja tu ambacho kimepata mikopo hiyo.

Sasa nadhani Mhe. Waziri ipo haja ya kushirikiana na watendaji wa wizara hii, na nikikumbuka katika taarifa zake Mhe. Waziri kwenye Baraza hili Tukufu, kwamba aliwahi kutoa tamko kuwa atahakikisha kila jimbo linafaidika na mikopo hii angalau basi kila jimbo katika majimbo yote 50 ya Unguja na Pemba, basi kila jimbo liwe linapata mkopo.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri, kwa sababu majimboni tunavyo vikundi pamoja na *SACCOS* nyingi lakini kumekuwa na malalamiko mengi, kwamba kila wanapokwenda wizarani mikopo hawapati, na kwa kuwa tunashikwa mashati sisi Wawakilishi katika majimbo yetu, kwa ajili ya kutaka kujua mwenendo mzima wa masuala haya ya mikopo.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba suala hili analifikisha katika majimbo, basi na yeye namuomba kwamba awe akifanya ziara katika kila jimbo, ili kuhamasisha na kushirikiana na Wawakilishi wa Majimbo pamoja na Viongozi wa Majimbo, ili mikopo ile basi ifike katika kila jimbo kwenye nchi yetu hii.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Idara ya Ajira. Kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuweza kusajili wale Mawakala ambao wameomba kushughulikia suala zima la kutatua au kusaidia kuwatatulia wananchi wetu, kwa ajili ya kuwatafutia vijana ajira katika nchi mbali mbali. *(Makofi)*

Kwa kweli tatizo hili liliwahi kuja hapa katika Baraza lako Tukufu, yaani malalamiko yalikuja katika kampuni hizi ambazo zimesajiliwa, lakini nashukuru Mhe. Waziri ameweza kueleza ile mikakati na mipango madhubuti ya kuweza kwamba kampuni zile zinatekeleza kazi zao kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, mbali na hayo kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa wananchi, vijana huko majimboni kwamba bado kumekuwa na tatizo kwa kampuni hizi za mawakala kupokea fedha za wananchi wanyonge, na fedha hizo wanazitoa kwa ajili ya kupata ajira, ili kuweza kujikimu kimaisha pamoja kuzisaidia familia zao katika kujikwamua na maisha magumu ambayo tuliyonayo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri ni mikakati na mipango gani ya kuhakikisha kwamba wale wananchi ambao wanatoa fedha zao kwa hawa mawakala, kuhakikisha kwamba wanapotoa fedha zao, basi ajira zile wanapata, kwa sababu lengo la kutoa fedha zile ni kwa ajili ya kupata hizo ajira. Kwa mfano, ikiwa nchi za nje kama vile nchi za Uarabuni huko au nyenginezo mbali mbali, lakini lengo na madhumuni ya kutoa fedha zile ni kupata ajira.

Sasa kuna uhakika gani kwa wananchi hawa ambao wanatoa fedha zao na sisi Wawakilishi majimboni tunachangia fedha hizi, yaani tunashikwa huko majimboni na wananchi wetu,

kwamba Mheshimiwa nimekuja kuna ajira hivi na vile, basi unatoa fedha kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wako.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja aje atueleze kwamba ana mikakati gani ya kuhakikisha kuwa wale wanaotoa fedha zao katika kampuni hizi za mawakala wanapata ile haki wanayoitaka.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba nimuulize Mhe. Waziri kuna suala hili la wananchi ambao ni wageni wanaokuja kutoka nchi mbali mbali katika kutafuta ajira hapa kwetu au hapa Zanzibar kwenye sehemu tofauti ikiwemo mahoteli na sehemu nyengine. Kwa mfano, wananchi wanaokuja kutoka Kenya, Uganda pamoja na nchi nyengine majirani zetu wanaokuja hapa kwa ajili ya kutafuta ajira.

Mhe. Spika, sasa kuna kazi ambazo wanazoweza kupata wananchi wale wageni, basi kazi zile zinaweza kufanywa na wananchi ambao ni wazaliwa, ambapo vijana wetu hapa kama nilivyozungumza awali wanatafuta ajira nje ya nchi, lakini pengine nafasi zile wanazopewa wale wageni wanaokuja wanaweza kuzifanya wananchi wetu, ndugu zetu, vijana wetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja atueleze mikakati gani inayofanywa hasa katika sehemu ya mahoteli, kwamba zile ajira ambazo zinazoweza kufanywa na wananchi wetu, basi wananchi wetu wanapata ajira zile.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja Hotuba hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Ahsante sana Mhe. Spika.

96

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Waheshimiwa karibuni tuendelee na majadiliano. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia machache katika Bajeti hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, mimi katika mchango wangu wa leo nitaomba kwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 28 kifungu cha 32, ambapo kuna Idara ya Uendeshaji na Uratibu wa Program za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 wizara hii ilikuwa na malengo ya utekelezaji katika kufanikisha shughuli zake kama ifuatavyo. Kwanza kabisa walijiwekea malengo ya kufanya uchambuzi wa mahitaji ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie Taarifa ya Ripoti ya Uchumbuzi huo.

Pili kupanga na kuendesha mafunzo ya kuongeza ujuzi wa wajasiriamali. Katika taarifa ya kitabu hichi tumekuta kuna wafanyakazi zaidi ya 90 ambao wameweza kupata taaluma hiyo, nachukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa kufikia malengo hayo.

Tatu kulikuwa na malengo ya kutayarisha Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, nimejaribu kuchambua sana hichi kitabu lakini sikukuta maelekezo ya utekelezaji wa hatua hiyo.

Nne ilikuwa kuna kuandaa na kuendesha Mikutano ya Kamati za Uwezeshaji za Wilaya na Taifa, pia nimejaribu kuchambua humu na wala sikuona maandalizi ya mikutano hiyo au ufanyikaji wa mikutano hiyo katika ngazi hizo ambazo zilikuwa zimeainishwa katika mwaka wa fedha uliomalizika.

Mhe. Spika, jambo la tano kulikuwa na malengo kwa kushirikiana na Idara ya Mipango Sera na Utafiti, kufanya utafiti katika maeneo muhimu ya kiuchumi, ili kubaini fursa zilizopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Maeneo hayo kwa furaha kabisa nimeyaona na imeonekana Mhe. Waziri katika sekta hii wamejitahidi kutembelea hoteli kwa hatua ya kwanza na kuona hali halisi inayoendelea.

Sita malengo yaliyowekwa ilikuwa ni kuandaa mafunzo kwa wafanyakazi, ili waweze kupanga utaratibu wa kusimamia vyema *Program* za Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Spika, baada ya kuingia ndani ya kitabu hichi nimeona kwamba kuna mfanyakazi mmoja tu ndiye ambaye ameweza kupatiwa mafunzo hayo, ambayo yalikuwa kwa muda wa wiki mbili tu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa tutaomba atuelekeze au atuambie pamoja na Baraza lako Tukufu, ni kwa nini wafanyakazi hawa amepatikana mmoja tu. Je inatokana na kwamba hana watu wa kuweza kwenda kupata taaluma hiyo au uwezo wa kifedha umemkwaza ikabidi ashindwe kutekeleza au kutimiza yale malengo ambayo kuwa ameyakusudia.

Saba ni kuandaa mapendekezo ya miradi ili kutafuta rasilimali fedha kwa misaada ya kitaalamu kwa lengo la kuwawezesha wananchi. Katika taarifa ambayo nimeisoma kwenye kijitabu hichi hatujaona bado hao watu ambao kuwa wamelengwa kwa ajili ya kuweza kukamilisha kazi hiyo.

Baada ya uchambuzi huo mdogo tu, kwa heshima na taadhima kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Kikwajuni, naunga mkono hoja na naomba nipewe maelekezo ya kina kuhusiana na masuala yangu. Ahsante sana. Mhe. Spika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Haroun Suleiman. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Kwanza nimpongeze kwa kuleta hotuba nzuri iliyopangika, iliyoeleza maendeleo yote katika Wizara yake kwa kipindi kilichopita na malengo mapya katika mwaka huu tunaokwenda nao.

Mhe. Spika, nije katika hotuba moja kwa moja ukurasa wa 13 ambao unaeleza kwamba hapa kuna mradi wa kupambana na ajira ya watoto. Niishukuru Wizara kuliona hili. Hivi sasa dunia nzima imekumbwa na wimbi kubwa la watoto kufanyishwa kazi ambazo nyengine si nzuri na zinawarudisha nyuma kimaendeleo. Mimi nashukuru kwamba katika hotuba yake ameeleza kabisa kwamba ana malengo kwanza kuanza na Wilaya 9 kwa Unguja na Pemba. Nia yake awanusuru watoto wasiopungua 5000 katika mradi huu, ili waweze kama kusoma wapate haki za kusoma na waweze kujiendeleza na hatimaye wenyewe waweze kujitegemea.

Mhe. Waziri naomba nimwambie kwamba ajira za watoto zipo za aina mbali mbali. Mimi nitamtolea mfano wa aina mbili.

1) Mtoto akiwa hali ya umasikini nyumbani huwa anajituma mwenyewe. Anaweza akatoroka akenda akashinda Malindi au Pwani kwa kupara samaki au kazi nyengine yoyote ile atakayojaaliwa kuipata.

2) Ajira nyengine wazee ni masikini na wanataka kula mavazi na huduma nyengine. Sasa utakuta wazee wale wale wanafanya vitumbua, pengine kaimati, wanampa mtoto akauze. Zote hizo ni ajira lakini zina tofauti vile vile.

Ningeomba nimshauri sana kwamba gurupu la kwanza la kuangalia sana ni wale watoto ambao wanajitoa wenyewe nyumba kwenda magengeni kufanya kazi. Wale wangechungwa wakaweza kutafutwa kwamba wanaishi wapi, wakarejeshwa majumbani ili wakahudumiwa kwa kuweza kusoma na baadaye wakajitegemea.
Humu mmesema kwamba pia mtafuatilia mpaka familia, ili mziwezeshe ili watoto waondoshwe kwenye ajira hii. Nadhani haya yote mawili yafanyike wakati mmoja ili tuweze kunusuru katika hali nzima ya vijana wetu ambao baadaye wao ndio watakaokuja kushika nafasi mbali mbali katika nchi hii.

Pili nimuulize kwamba pamoja na hayo umetaja tu kwamba Wilaya 9 Unguja na Pemba, lakini hukuziainisha wilaya gani na gani la kama umeziainisha sikuziona ni Wilaya gani na gani. Naomba ukija unifafanulie ni katika shehia zipi kwa sababu Wilaya ni kubwa, kuna nyengine zina shehia 200, kuna nyengine zina shehia 60, 30 inategemea ukubwa wa Wilaya. Ningeliomba pia utwambie ni Shehia zipi ambazo utaanza zoezi hili, ili pengine kama tunahusika na maeneo haya tuweze kusaidia tushirikiane na wataalamu wako ili vijana wetu waweze kufikia kwenye malengo yaliyokusudiwa.

Suala la pili katika ukurasa wa 14 umezungumzia juu ya mradi wa kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi. Kwanza nakupongeza kwa kuliona hili na umesema mradi huu umemaliza muda wake mwishoni mwa mwezi wa Mei, 2012.Tunashukuru na nadhani sasa hivi kazi tayari imeanza, na tayari mmeshakagua taasisi 327 Unguja 268 na Pemba 59, ambazo tayari hizo mmeshaanza kuzifanyia kazi.

Mimi katika kijarida hicho ulichotupa ambacho kinaendana na hotuba hii, yamo masharti humu ya mambo ya kazi. Kwanza imezungumzia saa za kazi. Utakuta kwamba hivi sasa maeneo mengi hili hawalijali sana, wanajali watu wafanye kazi. Mfano hivi sasa muda mwingi hupata nafasi ya kwenda Shamba kufanya Semina za Mafunzo, kila tunapokwenda tunakuta vijana wale kwa wale. Juzi nikamuuliza mmoja nyinyi mnakaa muda gani. Wakasema sisi hapa mapumziko yetu mpaka aumwe mtu ndio atoke. Lakini pakiwa na wageni hapa tunaweza tukapiga mwezi mzima nyumbani huwendi.

Ukitizama sharti hili kwa jibu nililolipata kule halijafanya kazi bado. Ningelishauri tusiwe tunaandika kwenye vipeperushi, lakini na utekelezaji ufatwe. Vile vile jengine limeandikwa malipo ya ajira. Tumeuliza mishahara wanayopata wengine haifahamiki. Anaweza akaenda mwezi mzima akalipwa laki mmoja. Anaweza akaenda mwezi mwengine akalipwa shilingi elfu tisini. Akiuliza anaambiwa safari hii hatukupata wageni wengi. Hili halihusiani baina ya mfanyakazi na kupata wageni. Wewe mtu umemuajiri mmekubaliana kama laki moja na ishirini, mgeni akiwepo laki moja na ishirini asiwepo laki moja na ishirini. Lakini sasa hoteli zetu nyingi

mgeni kama hakuja na wewe wanakukatia humo humo. Nadhani na hili Mhe. Waziri na wataalamu wako katika mradi huu mngelifuatilia ili likafikia yale malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, jengine ni kiinua mgongo ambalo hili muda mwingi tunalizungumza kwamba kiinua mgongo kinaleta matatizo kwenye mahoteli. Kwa sababu sheria bado inawazuia. *Mathalan* mimi nimefanya kazi tuseme *La gemma*, nimefanya kazi mwaka mmoja, mwaka wa pili nimefukuzwa, lakini nimepata kazi nyengine Mnarani Nungwi, nimefanya kazi miaka miwili, mitatu nimefukuzwa, nikenda kutaka kiinua mgongo changu naambiwa kwamba mpaka nitimize miaka 60. Hili kwa kweli linarudisha nyuma, miaka 60 kwa vijana wa sasa hivi si wengi wanaofika.
Mhe. Spika, tungeshauri wataalamu wako pamoja na wanasheria tungejaribu kufanya utaratibu kwamba mtu anapomaliza kazi yake kafukuzwa apewe chake aende kwengine. Lakini kusema tusubiri miaka 60 vijana wengi watarithiwa. Ningeliomba na hili la sheria lingerekebishwa ili mtu ukimaliza kazi kama miezi sita upate chako, kama mwaka upate chako, kuliko kuweka sheria ya serikali ikachanganya pamoja na kazi za watu binafsi, kuweka miaka 60 ni mingi sana.

Mhe. Spika, jengine kuhusu suala la saa za malipo ya ziada. Pia tumebaini sehemu nyingi mtu anaweza akafanya kazi mchana mpaka jioni akapumzika kidogo akaingia na usiku, lakini malipo ni yale yale. Sasa na hili pia wataalamu wangepita kwa wafanyakazi wakawauliza ili wakasema lile tatizo walilonalo. Bado saa za ziada hazilipwi inavyopaswa katika hoteli nyingi na taasisi nyingi za watu binafsi. Tungeliomba na hili vile vile likafanyiwa kazi.
Mhe. Spika, likizo za kawaida vile vile hili wafanyakazi wengi hawazipati hata upande wa serikali, utakuta watu wengi sasa hivi likizo hawaipati na hawa wakiipata haina malipo. Naomba na hili lingezingatiwa ili huu mradi ukafikia pale ulipokusudiwa. Nadhani tukienda hivyo itakuwa miradi yetu imefanikiwa na yule aliyouchangia mradi huu watakuwa wamenufaika kwa pesa zao walizozitoa na zikatumika kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, niendelee katika mchango wa Wizara hii nije kwenye ukurasa wa 40, Idara ya Mikopo. Hapa wamekusudia kwamba katika kipindi hichi tunachokwenda nacho cha mwaka 2012/2013 wamekusudia watoe mikopo 1000 kwa vikundi mbali mbali vya watu binafsi pamoja na SACCOS. Mimi nadhani niungane na wenzangu waliokwisha kutangulia kwamba tumebaini vikundi vipo vingi lakini fedha wanazokopeshwa ni ndogo kutokana na hali ilivyo.

Mfano mimi nitatoa kwenye jimbo langu. Kwenye jimbo langu nilikuwa nina vikundi vinafika 50 wafugaji kuku, wafugaji ng'ombe wa maziwa, walima miti, wafanya *nursery*, utakuta mtu anakopeshwa laki moja na ishirini akafuge kuku. Wakati sasa hivi polo la kuku la chakula kwa kuku wa mayai linauzwa Sh. 85,000/-, sasa sijui afuge kuku wangapi, watano au sita. Nadhani na hili lingeangaliwa yule mtu mnaetaka kumuendeleza mumuangalie uwezo alionao, na kitu gani anachopewa angalau kiweze kumfikisha pale palipokusudiwa. Wengine wanapewa Mkopo shilingi elfu hamsini, akirudisha elfu hamsini anapewa laki, akirudisha laki anapewa laki mbili. Utakuta hata ile faida ya kuweza kwenda mbele zaidi inachukua muda kwa sababu mtaji anaoupata ni mdogo.

Ningelishauri kwanza fedha sasa hivi wangepewa taaluma ya kutosha ya kibiashara ama ya ufugaji au ya kilimo inategemea mtu mradi alioanzishwa, kwa lengo kile anachopewa kiweze kumuendeleza afikie pale palipokusudiwa. Utakuta mtu unampa ng'ombe wa maziwa wa milioni moja lakini hana uwezo hata wa kununua gunia la chakula. Kwa sababu gunia la pumba la

ng'ombe wa maziwa linauzwa elfu thamanini, dogo la kuramba kilo kumi linauzwa elfu ishirini na tano, hujakata majani. Utakuta mtu kama yule baada ya kumpa tija aende mbele unaanza kumtia umaskini. Ataanza kuuza baskeli, itakwenda atauza godoro, alalie busati. Inakuwa humpeleki mbele katika mradi unakuwa unamrudisha nyuma.

Ningeshauri na hili ile miradi ambayo wanaianzisha wananchi wangeshauriwa mradi gani unaweza kwenda kwa mujibu wa uwezo wake kuliko mtu unampelekea ng'ombe wa maziwa halafu unaondoka, kwa hiyo tunawapa shida wananchi wetu. Ningeliwashauri na hili wataalamu wangeangalia miradi ya kuwapa wananchi, kwa lengo la kuweza kuondosha huo umasikini tulioukusudia.

Mhe. Spika, nikiendelea nije ukurasa wa 56 Idara ya Ajira. Hii pia wameeleza kwamba wana nia ya kuongeza fursa za ajira lakini zaidi kwa wazalendo. Hii niungane na wenzangu waliotangulia kuzungumza kwamba bado hili halijafikiwa, na kama tutalifanyia asilimia basi nadhani kwenye mia tuko kwenye asilimia 20. Lakini wageni wanapewa nafasi kubwa sana. Tatizo sijalijua ningeomba hii yeye Waziri kama ana wataalamu akaona ni taaluma, ni kuogopa ajira, ama ni kitu gani.

Watu wengi wanahisi kwamba kazi za mahoteli wafanye watu wa nje tu, hiyo haiwezekani, kazi za hoteli vijana sasa hivi wameshasoma na wao wapate nafasi waweze kufanya. Kwa sababu hata ukiwa pale hoteli au kaa baa hunywi wewe eti, wewe unahudumia tu pale. Ningeliomba na hilo vile vile lingetizamwa ili fursa kubwa tukapata vijana wetu waliokuwepo hapa Wazalendo.

Pia imeelezwa humu kuwa mradi huu ni kufanya utafiti ni wafanyakazi wangapi walioajiriwa na taasisi mbali mbali ambao wametoka kwenye nchi yetu hii. Na hii tukiifanyia tathmini tutaweza kujua kwamba tumefikia hatua gani katika kuajiri vijana wetu. Hili ni muhimu kwa sababu kila tukiwa na takwimu ndio tutaweza kujipanga vizuri. Ningemshauri Mhe. Waziri bado vijana wengi wamo mitaani na wengi sasa hivi na vyeti na chuo tunacho cha utalii, vijana wapewe kipaumbele katika kuendeleza nchi yao na wao kujitoa kwenye umasikini wa ajira.
Mwisho kabisa nije kwenye kiambatanisho Nam. 6. Mkopo wa JK na AK. Mheshimiwa tulipata faraja sana baada ya kuandaliwa mikopo hii, lakini kwa bahati mbaya sana kwamba ile dhamira na malengo hayakufikiwa. Sasa sijui taaluma tulichelewa kuwaandaa wananchi kitaaluma sielewi, unaweza ukatujibu wewe. Lakini mpaka hivi sasa mimi jimboni mwangu sidhani kama kuna vikundi ambavyo vimepata mikopo hii. Sasa kama wewe unavyo huko naomba wakati wa majumuisho nambie Mfenesini kuna kikundi cha Mwakaje *SACCOS* fulani, Michungwa miwili *SACCOS* fulani, Chuini *SACCOS* fulani, ili na mimi kama kuna uwezo wa kushirikiana nao nikajua.

Mikopo hii mingi imetolewa kimya kimya kupitia Shehia, wakati sisi ni viongozi katika majimbo taarifa hizo hatuna. Sasa naomba kama mimi kwangu yapo basi unieleze ili na mimi nipate faraja na halafu niwatembelee nijue wamefikia hatua gani. Kwa sababu imeonekana hapa ulipaji bado ni mgumu. Mkopo huo umekusudiwa nikipewa mimi nilipe ili apate mwenzangu. Ni mfuko ambao unaozunguka, sasa kama mtu atakaa nao yeye tu halipi kama kaambiwa alipe kwa mwaka analipa miaka mitano, kwanza anaudhorotesha ule mfuko hauendi mbele. Lakini pia anawanyima haki kama aliyoipata yeye.

Mhe. Spika, ningeliomba kama jimboni mwangu viko vikundi vimepata unambie ni vikundi gani na ni kiasi gani na wanalipa vipi, ili nisaidie deni lirudi waweze kupewa wengine kwa manufaa kama walivyokusudia Maraisi wetu wawili waliouweka mfuko huu.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huo mfupi, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Mfenesini tunaunga mkono bajeti hii.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi kwa upande wangu kwa mara nyengine tena nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini vile vile nikushukuru wewe kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia wizara hii muhimu sana kwa wananchi wetu kwa maendeleo ya vijana katika suala zima la kuwawezesha wananchi wetu wote kiuchumi.
Mhe. Spika, mimi kwanza kabla sijaingia katika kuchangia hii bajeti nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Tunajua kuwa majukumu aliyopewa ni magumu na ugumu wake unakuja katika suala zima la kuanzisha wizara. Tunaamini kwa umahiri wake na uadilifu wake katika kazi na kwa kuwa alikuwa ni mwalimu basi naamini wizara hii ataweza kuijenga na kuweza kuiwekea mazingira mazuri, ili wananchi wetu waweze kuishi katika hali ya kuweza kuwawezesha kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ana kazi kubwa kwa sababu kuwawezesha wananchi kiuchumi hiyo hasa ndio program ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kuondoa umasikini hapa Zanzibar yaani MKUZA, inasema mpango Mkuu wa Kupunguza Umasikini hapa Zanzibar. Suala la kuwawezesha wananchi ni suala zito na linahitaji umahiri mkubwa na bidii kubwa ili kuhakikisha wananchi wetu wote wa Zanzibar tunawawezesha kiuchumi ili kuweza kumudu maisha yao. Namtakia kila la kheri Mhe. Waziri katika wizara hii, ili kuweza kutimiza ile kiu ambayo wananchi wanaohitaji. Nataka niseme kwa nini nikasema Mhe. Waziri nimi nataka nimpongeze na vile vile naamini ataweza kutekeleza majukumu yake.

Katika miaka ya 2000 mpaka 2010, Mheshimiwa wetu huyu aliwahi kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Katika wakati wake huo Mhe. Spika, tumeshuhudia maendeleo makubwa katika sekta ya elimu, ikiwemo katika suala zima la kuimarisha skuli za Sekondari lakini vile vile hata uanzishwaji wa vyuo Vikuu kwa hapa Zanzibar. Jambo ambalo ni gumu na tunajua kwamba alipata misukosuko mikubwa wakati alipokuwa akianzisha hivi vyuo vyetu vikuu. Kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar masuala ya Elimu ya Juu ni Masuala ya Muungano. Lakini pamoja na hayo Mheshimiwa kwa jitihada zake yeye hakuweza kusema kwamba amejitahidi baadae akapumua. Yeye hakuamua kupumua, aliamua kuchapa kazi, aliendelea na mpaka sasa hivi tunashukuru ni jana tu tulikuwa tunasoma bajeti ya Wizara ya Elimu ambayo imebakisha matunda yake mengi ya uanzishwaji wa vyuo vikuu hapa Zanzibar, kwa hilo Mhe. Waziri tunampongeza sana.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri aliwahi kupata sifa kubwa sana, mimi siku hiyo nilikuwepo pale Rahaleo tulipokuwa tukikabidhiwa vile vitabu vya Skuli ya Sekondari. Kwa mpango ule wa kuwezesha skuli zetu za Sekondari kuwa na vitabu vyake. Alikuwa pale Mkurugenzi wa Shirila la Maendeleo ya Marekani USA bibi *Pamella White* na alimtangaza pale kwamba Mhe. Harouna Suleiman, ule ubora wake hakustahili kuwa Waziri wa Elimu Zanzibar lakini alistahili kuwa Waziri wa Elimu wa Afrika. Naamini Mheshimiwa sifa hizi ataziendeleza kuwa Waziri Bora katika kuanzisha hii Wizara iliyokuwa nzito.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nilikuwa nataka kumpongeza Mhe. Waziri katika kazi aliyoifanya iliyotukuka aliweza kutunikiwa nishani ambayo hata jana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu alithibitisha kwamba Mhe. Waziri wetu huyu alitunukiwa nishani na *UNESCO* kwamba ni Waziri Bora katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba niende katika kuchangia hoja. Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo Wizara hii kwa kweli ni ngumu. Tulipokuwa tukichangia bajeti ya Wizara ya Utumishi wa Umma Mheshimiwa rafiki yangu, swahibu yangu maalim Harouna nilijaribu kumpa angalizo. Angalizo langu lilikuwa kuhusu vijana wa Zantel ambao walikuwa wamefanya kazi kwa muda mrefu wale walinzi.

Lakini vile vile na vijana wetu waliofanya kazi katika Mahoteli ambao bado mpaka leo hawajapata mikataba. Namshukuru sana Mhe. Waziri ndani ya wiki ile ile baada ya kulizungumza suala la mikataba kwa wafanyakazi walinzi wa kampuni ya Zantel, aliweza kuwatafuta akanishirikisha na mimi vijana wale nikaenda nao ofisini na kwa kweli wameanza kupata hiyo mikataba. Mikataba hii kwa sababu ilidaiwa kwa muda mrefu, lakini kwa kuwa Waziri wetu huyu msikivu jambo unalomwambia siku ya pili analifanyia kazi, tunashukuru mikataba ile imepatikana, ingawa mikataba ile bado ina matatizo lakini naamini Mhe. Waziri atakaa tena na wale vijana.

Mimi nimeiona ile mikataba, kuna mikataba ya walinzi ambayo malipo yake ni makubwa, lakini ile mikataba waliopewa vijana wetu nadhani baada ya shindikizo la Mhe. Waziri wakaona kwa sababu Mhe. Waziri alitishia kuichukulia hatua Kampuni ya Zantel kama hawakuweza kuwapa wale mikataba. Kwa hivyo nadhani Kampuni ya Zantel wakafanya haraka haraka ndio maana wakatengeneza ile mikataba ya haraka haraka.

Nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wetu wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni kuhakikisha kwamba kama walivyoweza kutoa mikataba ya kada ile ile wa ulinzi na kwa wale waajiriwa wengine, na wale wa Zantel wahakikishe zile stahiki walizokuwa wanapata wenzao na wao waweze kupata zile zile. Nchi yetu ni nchi ambayo inaongozwa na utawala bora, demokrasia, hakuna ubaguzi wa rangi, dini, kabila wala jinsia. Tunaomba katika sehemu ya ajira, Kampuni zote na Mashirika yote kama yalivyo ndani ya serikali kwamba hakuna ubaguzi katika ajira, katika kuwalipa watu mishahara basi na huko tunaomba iwe hivyo.

Mhe. Spika, lakini bado namuomba sana Mhe. Waziri najua hili ni gumu sana, kwa sababu mahoteli ya Zanzibar yapo mengi lakini aweze kulisimamia kuhakikisha na hawa wafanyakazi wote wa mahoteli wahakikishiwe wanapewa mikataba. Si busara mtu kufanya kazi ndani ya nchi yake akageuka kama Manamba, ni mtu ambaye anafanya kazi leo kesho akiondoka anakuwa hana chake. Sasa hatutaki kuwa na Manamba katika nchi yetu ya Zanzibar. Namuomba hilo Mhe. Waziri alifanyie kazi na naamini kwa umahiri wake kama kawaida yake atalichukulia hatua zinazostahiki.

Mhe. Spika, vile vile nilikuwa naomba Mhe. Waziri aweze kulisimamia hili kwamba hivi sasa kuna baadhi ya kampuni binafsi na taasisi binafsi wanawafukuza watu ajira kama wanafukuza kuku, yaani leo mtu anafanya kazi siku ya pili anafukuzwa, hakuna taarifa, hakuna onyo, hakuna muda wa kujitetea. Mhe. Spika, hata ndani ya serikali tumeweka utaratibu wa vyama vya

wafanyakazi, tumeanzisha vyama vya wafanyakazi ili kuangalia mpaka maslahi yao katika masuala ya mishahara.

Mhe. Spika, hili vile vile tunamwambia na Waziri wa Utumishi wa Umma anapopanga stahiki za wafanyakazi lazima ahakikishe anakaa na wale wadau wa wafanyakazi (Vyama vya Wafanyakazi), ili kuangalia. Katika suala zima la maslahi inatakiwa lazima kuwepo na utatu yaani kwa upande wa Serikali, Muwakilishi wa Wafanyakazi, vile vile kwa upande wa Muwakilishi ili kutenda haki kwa jambo lolote linalofanyika la maslahi katika masuala mazima ya ajira. Nilikuwa naomba, hata hao wenye Mahoteli wenye Kampuni na Mashirika katika masuala mazima ya kuweza kutoa ajira. Lakini vile vile kufukuza, lazima wahakikishe kwamba mfanyakazi anapofukuzwa lazima kiwepo kikao cha utatu. Hapa nawaomba wafanyakazi wote wa Zanzibar kuhakikisha kwamba wanajiunga na jumuia za Wafanyakazi, ili iwe watetezi wao pale inapotokezea migogoro baina ya waajiri na waajiriwa.

Hili nilikuwa namuomba Mhe. Waziri awaite vyama vya wafanyakazi, viongozi wa vyama vya Wafanyakazi awaite, awape muongozo, wapite katika Wizara, wazungumze na wafanyakazi ili kujiunga na jumuia hizi endapo yanapotokezea matatizo iwe kuna mwamvuli wao wa kuweza kujadili masuala yao, hasa katika masuala ya maslahi na ajira. Nilikuwa naliomba Mhe. Waziri aweze kulisimamia.

Jengine katika hii sekta ya utalii. Mhe. Spika, tulipokuwa tunapitisha Mswada wa Wizara ya Habari kuhusu suala zima la Mswada wa Sheria wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Utalii. Miongoni mwa waliokuwa wakitetea kwamba *priority* katika suala zima la ajira hasa katika maeneo haya ya utalii katika sekta ya utalii ilikuwa tulipendekeza iwe *priority* Wazanzibari.

Kuna wananchi wengi ambao suala hili wanalizungumza kwa kulipotosho huko mitaani kwa kusema kwamba, labda sisi hatuwapendi Watanzania wenzetu. Lakini Mhe. Spika, sio sahihi, katika nchi zote za Visiwa Mhe. Spika, katika suala zima la ajira lazima ajira ya ndani lazima wale wananchi husika katika visiwa vile wanatakiwa walindwe.

Mhe. Spika, ukiangalia wenzetu *Mauritius* au *Malaysia,* moja katika vigezo vyao ajira hata zile za majumbani kwa mtu wa kawaida yeyote mgeni ambaye hatoki katika nchi zile hawezi kupata mpaka kwa utaratibu maalum. Lakini sisi tumeachia kila kazi inakuwa kiholela. Ndio maana tukaweka *priority* katika ajira ya ukanda wa Mahoteli au katika sekta ya utalii awe ni Mzanzibari.

Mimi nataka niwambie wale wananchi wenzetu ambao wanajaribu kupotosha ile dhana wakasema kwamba sisi hatuwapendi Watanzania, Mhe. Spika, waangalie sheria ya Uzanzibari. Sheria ya Uzanzibari tuliyoipitisha hapa Barazani mtu yeyote wa Tanzania anapofika hapa miaka mitano akiomba kuwa mkaazi basi anapata haki hiyo. Sasa je, hapo palikuwa kuna ubaguzi wa kusema kwamba labda Watanzania tunawakataa. Hata Watanzania ambao sio wenye asili ya Zanzibar ile miaka mitano tumeiweka ili mtu kuchunguzwa tabia zake, mambo yake na matendo yake ili tusije tukampa mtu ukaazi ambaye pengine ni jambazi au pengine ni mtu ambaye ni muhalifu.

Mhe. Spika, nilikuwa najaribu kuliweka sawa hilo tu. Tulipokuwa tunatetea Wazanzibari na hata hao wenzetu kutoka Tanzania Bara na wao vile vile wakishakutimiza miaka mitano na wao vile vile wanakuwa ni Wazanzibari. Kwa hiyo tulikuwa hatuna lengo la ubaguzi lakini lengo letu ilikuwa ni kutetea na kulinda ajira za Zanzibar.

Mhe. Spika, imezungumzwa huku kama kuna Idara ambayo itakayoshughulikia masuala ya kutafuta ajira. Mimi nadhani Mhe. Spika, hata wenzetu Uingereza pale hata ukiangalia wale Wazanzibari waliokimbia hapa Zanzibar kipindi kile cha siasa kali, alipofika Uingereza kule walipokelewa, na walipokelewa kwa sababu kule kuna maeneo kuna taasisi ambazo zinaitwa *Job Center*, zile zimewekwa makusudi ili kuwatafutia watu waliokuwa hawana ajira kuweza kupata ajira. Miongoni mwa vijana waliopata msaada wa kupata ajira kule Uingereza zilikuwa ni hizo *Job Center*.

Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akae na hiyo timu yake ya Idara ya Kazi kuangalia kutafuta taasisi au kujenga kitengo ambacho kinakuwa kama ni *One Stop Center* ili yale masuala yote ya ajira pale kuwe kunapatikana taarifa zote za ajira. Kwa hivyo vijana wetu wakishamaliza skuli wanakwenda pale katika kituo wanaangalia ni eneo gani linahitaji wafanyakazi, kama kuna kiwanda kimeanzishwa wanapeleka pale maombi yao ya ajira, ingekuwa pale tunawarahisishia.

Lakini leo Mhe. Spika, kuna vijana wetu wamemaliza diploma pale Chuo cha Hoteli ya Utalii Maruhubi, lakini mpaka leo wanahangaika, hawana kazi. Mimi nadhani kwa kuwa tumeanzisha hichi Chuo chetu cha Hoteli na Utalii, basi *priority* katika suala zima la ajira basi wangelianza kuangaliwa wale ambao waliopata vyeti kutoka katika chuo chetu cha Hoteli na Utalii.

Mhe. Spika, Chuo kile ni chuo cha Serikali, tunaamini mafunzo yanayotolewa pale ni mafunzo bora. Ina maana pale mtu akiondoka anakuwa ameiva. Sitaki nivibughudhi vyuo vyengine lakini inawezekana vyuo vyengine mtu akienda akapewa cheti pengine hata ile taaluma yenyewe anayoisomea hajaipata, kwa sababu unajua mtu anapoanzisha taasisi, taasisi inapokuwa ya kibiashara zaidi haangalii quality yeye anaangalia mimi nitapata fedha kiasi gani. Mfano huu umejitokeza hata baadhi ya taasisi ambazo wameanzisha wengine vyuo vya Afya, matokezeo yake vijana wameshasoma zaidi ya mwaka mmoja na nusu, amelipa kijana anachukua cheti anakwenda kuajiriwa pahala anaambiwa cheti chako hiki hakijakuwa *qualified* yaani hakijatambulikana. Sasa lakini chuo chetu cha Hoteli na Utalii kina walimu wazuri waliobobea, vile vile na sisi tunapitisha bajeti kodi za wazee wao kwa ajili ya kukiendeleza chuo kile. Kwa hivyo chuo kile lazima tukijenge ili vijana wetu wengi wanapomaliza skuli wahakikishe wanakwenda kujiunga na Chuo chetu cha Hoteli na Utalii kwa ajili ya kuweza kutafuta hizo ajira.

Mhe. Spika, ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa kutembelea vikundi mbali mbali vya Saccos na ahadi nyingi alizozitoa mimi ninaamini atazitekeleza, lakini kama tulivyosema Mhe. Waziri amepewa Wizara hii ngumu, wizara mpya haina *capital*. Kwa hivyo sasa hivi tumeziona juhudi zake anakwenda kutafuta kwa kushirikiana na yule Waziri wa Kazi wa Tanzania Bara wanakwenda nje, hata katika mkutano uliofanyika safari hii kule nadhani kama sikosei ilikuwa Qatar au Marekani atakuja kunisahihisha yeye mwenyewe kwamba kulitakiwa Tanzania tupeleke vijana kwa ajili ya kutafuta ajira katika nchi za Qatar na Mashariki ya Kati.

Lakini hili ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa sababu yuko makini hakuamua kulichukulia haraka haraka. Mhe. Spika, tumeshashuhudia kuna vijana wetu wengi ambao wamerudi katika falme za kiarabu wakaja wakalalamika zile ajira walizokuwa wanafanya sizo zile walizoahidiwa. Lakini vile vile kuna mambo mengine mabaya yaliyokuwa yanafanyika ambayo wao sio malengo waliyoendea kule na vijana wale walirudi, lakini tunaamini Mhe. Waziri kwa kuwa yuko makini, aliamua ajira hizi kwanza aziangalie, azichuje na baadae akishathibitisha na akeshajua wale ma-*agent* ni watu ambao *pure* hawana matatizo ataweza kuziruhusu ajira hizi ili vijana wetu waweze kupata ajira. Lakini jengine ninalomuomba Mhe. Waziri tusitegemee tu kupeleka vijana wetu kwenda kutumwa tu nje ya nchi.

Mimi nadhani wakati umefika sasa kuimarisha vyuo vyetu vya amali, Mhe. Spika, wala Mhe. Waziri asione aibu, wala asione tabu kuvisaidia vyuo vya amali alivyovianzisha yeye mwenyewe. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji alipokuwa Waziri wa Elimu alianzisha vyuo vya amali na alivijenga tunashukuru. Kuna vijana wetu ambao walitoroka madarasani hawakumaliza skuli wamekwenda pale wamepata mafunzo, na sasa hivi mafundi wazuri wanajitegemea na wala hawasubiri ajira kutoka serikalini.

Mhe. Spika, kwa wakati huu tuliokuwa nao kwa kuwa tayari tuna vyuo vikuu vingi Zanzibar, tayari kuna vijana wengi wenye diploma wenye digrii na wengine sasa hivi wana masters, *PHD* kwa hivyo tunaomba Serikali kupitia Wizara ya Elimu, lakini vile vile kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi kuandaa mitaala maalum ya wale vijana wetu wa vyuo vikuu kwanza kusomeshwa *course* za *management* huko huko katika vyuo vyao. Kwa sababu wanaposoma *course* ya *management* ndio maana tayari wameshatengenezwa katika ngazi ya Utawala.

Kwa hivyo ina maana wakiondoka pale katika vyuo wasilenge zaidi kuiangalia serikali itawafanyia nini, lakini serikali kwa kuwa wao wamefika vyuo vikuu serikali tayari imeshawafanyia nini, sasa wao tunavyowataka wakitoka kule kwenye vyuo vikuu waanzishe kampuni zao binafsi ili kuweza kutoa ajira kwa wengine.

Mhe. Spika, mimi ninaamini vijana wa vyuo vikuu wakiweza kujikusanya vijana kumi kumi ninaamini wataweza kutengeneza miradi, miradi ambayo itaweza kutoa ajira kwa vijana wetu hapa Zanzibar. Na kwa kuwa wao ni watu wenye elimu ninaamini wataweza kutoa muelekeo wa kuweza kutoa ajira ambayo itaweza kuleta manufaa kwa wananchi wetu.

Lakini Mhe. Spika, hivyo vyuo vya amali lakini vile vile hata hao vijana wetu wa vyuo vikuu watakapomaliza wakisema wajiunge waunde kampuni zao, sasa tujiulize mtaji wa kufanyia kazi wataupatia wapi. Sasa hapa Mhe. Waziri ninakuomba tena ushirikiane na Mhe. Waziri wa wanawake maendeleo ya vijana na watoto ili ile benki ya maendeleo ya wanawake pamoja na benki ya maendeleo ya vijana, sasa hivi Mhe. Spika, jukumu lile tunaliondoa ile kazi tuliyompa Waziri wa Wanawake na watoto, sasa hivi kazi hii rasmi tunakukabidhi Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Kiuchumi tuhakikishe bajeti ya mwakani unatwambia unakuja kutuanzishia benki ya maendeleo ya vijana, lakini vile vile benki ya maendeleo ya wanawake hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, hili hasa ni jukumu lako, Mhe. Spika, ninaamini kwa umahiri wako kuanzia leo ukitoka hapa utaanza kumtafuta gavana wa BOT, utawatafuta ma-meneja wa benki wote walioko Zanzibar ili wakushauri utatumia mbinu gani za kuweza kuanzisha benki hizi mbili ili kuweza

kutoa mikopo kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, hizo *Saccos*, vikundi vya ushirika, hao vijana watakaojiunga kutoka vyuo vikuu kuanzisha hizo kampuni, bila ya kuwa na mtaji Mhe. Spika, kwa kutegemea mfuko wa AK na JK *nothing can happen* hakuna chochote kitakachoweza kutokezea.

Mhe. Spika, uokozi wa ajira na uwezeshaji wa wananchi ni kuanzisha benki, na benki hizi ninaiomba serikali kutoka katika mfuko mkuu wa serikali, *capital* ya kuanzisha benki hizi mbili itoke katika mfuko mkuu wa serikali, na suala hili tunakuomba Mhe. Waziri ulisimamie na mimi nikiwa Mwenyekiti wa kamati ya wenyeviti, mwakani tunapopitisha bajeti ya serikali katika vile vipaumbele kimoja tutaanza kukahakikisha bajeti ya mwakani unakuja mtaji kutoka mfuko mkuu wa serikali wa kuanzisha benki hizi mbili au moja katika hizi mbili, aidha ni wanawake au hii ya maendeleo ya vijana.

Mhe. Spika, kwa umahiri wa Maalim Haruna na ninavyomjua hapendi kupigiwa buti sana basi hili akija akisimama atajibu ndio nimekubali, na ataomba tushirikiane katika hili na hili tunaamini tutashirikiana kwa pamoja.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba pamoja na mtaji lakini elimu inahitajika, kwa hivyo tunaomba sasa hivi Mhe. Waziri wa Kazi na Uwezeshaji, tunakuomba tena jambo uwasaidie sana JKU. Mhe. Spika, JKU tumewapa kazi kubwa tumewapa kazi ya kuwalea vijana wetu baada ya kumaliza skuli, lakini vijana wale wakienda JKU hawana zana zile za kufanyia kazi. Vijana wetu wa JKU wanafundishwa ufundi mchundo, ufundi seremala, ufundi ujenzi lakini hebu nenda JKU Mheshimiwa hawana nyenzo za kufanyia kazi, kwa hivyo naomba katika ziara zako utazokwenda kutafuta uwezeshaji wananchi naomba kakae na kamanda wa JKU umsikilize mipango yake, umsikilize malengo yake, uhakikishe katika safari zako unamuombea misaada ili kuimarisha JKU, kwa sababu JKU wakiweza kuwafundisha vijana wetu kazi za mikono, Wizara ya Elimu wakiwafundisha elimu ya amali, mimi ninaamini tutaweza kutengeneza taifa, vijana ambao wana mawazo ya kujitegemea, sio yale mawazo finyu ya kutegemea kwamba kila ajira ziweze kutoka serikalini.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa kabisa nataka niendelee kumpongeza tena Mhe. Waziri kwa jambo moja ambalo nimelisahau. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Elimu wakati pale mwisho mwisho alipokuwa anakung'uta kapu alipokuwa anamaliza mwaka 2010 alihangaika mpaka Marekani na akaweza kupata msaada wa kuanzisha elimu ya kufundisha wanafunzi kwa njia ya kompyuta, kuanzia elimu ya msingi ambao mradi huo unaitwa teknohama.

Mhe. Spika, nataka nimthitibitishie Mhe. Waziri ile jitihada yake aliyoifanya ili wanafunzi wetu mpaka wa *primary* waweze kusomea kutoka kwenye kompyuta, sasa hivi katika skuli yangu ya Shaurimoyo tayari nina darasa ambalo linaitwa la teknohama. Sasa ninakuomba Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri aandae siku maalum, kwa sababu umetengeneza wewe mwenyewe ule mpango, lakini kompyuta hatuna basi ututafutie huko katika safari zako japo kompyuta nne uwaletee pale skuli ya Shaurimoyo. Na nije niwatangazie kwamba huu mradi wa teknohama huyu ndiye aliyeuanzisha, kwa hivyo yupo bado nyuma yao katika kujitahidi kuutengeneza.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwa mara ya mwanzo kabisa sijakosoa naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Haroun Ali Suleiman kwa kuweza kutupatia nafasi zaidi pamoja na kuweza kuwapongeza watendaji wote wa Wizara yake, hasa kwa mipango mizuri ya Wizara hii ambayo imeweza kuwapa wajasiriamali kuweza kujiwezesha kulihudumia taifa vizuri.

Kwanza Mhe. Spika, sina budi nimpongeze kwa utendaji mzuri wa sehemu zote unazopangiwa kufanya kazi, hivyo hongera tunakupa sana sana, kila nafasi unayopewa wewe unakuwa namba moja, hivyo hatuna budi tukupongeze sana na tuweze kukupa jina zuri sana kwa utendaji wako, tuweze kukupa yule Rais wa Marekani moja kwa moja unafanana nae. Zaidi ya hayo naweza kukupa nafasi ya kwanza kukupa utendaji bora katika sehemu zote hasa vijijini kwa unavyotusaidia, lakini hata hivyo usisahau kuwapa vijana nafasi kubwa zaidi ya kuwa wajasiriamali vizuri, hasa kuwapatia vyombo vya kisasa kuweza kujitegemea, ukizingatia zaidi hasa watendaji wetu sehemu za pwani pwani, tungependelea zaidi kuweza kuwapatia mikopo, kuweza kuimarisha vizuri hasa kwa mambo yao ya uvuvi. Ni vizuri zaidi kama utaweza kutusaidia hata Jimbo langu la Koani lina matatizo sana hasa upande wa uvuvi hatuna boti za kisasa, ni afadhali ungelituchangia tukaweza kupata boti tukaweza kujiimarisha katika utendaji wa mambo ya uvuvi na sehemu nyengine.

Vile vile kuweza kuwachangia akina mama wa Jimbo la Koani hasa wakulima wa mwani kama ulivyukuja katika sehemu yangu ya Uzi ng'ambwa ukatuahidi, mimi naomba usichoke tena ili kutupatia mikopo kinamama hawa kuweza kukiimarisha kwa mambo ya ukulima wa mwani, ili tukapata fedha za kigeni hasa vile kama ninavyokuahidi tutapokwenda sisi *back benchers* katika safari zetu kuwatafutia pesa za kigeni ili kuuza mwani wao kwa bei juu.

Vile vile ninakukumbusha kwamba tunazo sehemu nyingi sana za kuweka uwekezaji sio karafuu peke yake kama vile tulivyozoea, kwa vile ninakuahidi kama utatupatia mikopo mizuri na vitu vya kutendea kazi, ninakuhakikishia kwamba majimboni mwetu tutaweza kuimarisha mambo mapya na tukaweza kupata fedha za kigeni wewe mwenyewe ukashangaa. Pesa utazokopesha ni ndogo lakini malipo ninajua utapata mengi sana. Hivi sasa kwa kweli tumejiimarisha vijana wa pwani pwani kuweza kupata viwanda vidogo vidogo pamoja na vitendea kazi. Ningelipenda kwamba vijana hivi sasa waimarishe vizuri ili kuwapatia viwanda vidogo vidogo, ambao wao wenyewe wajiimarishe kuweza kuchonga angalau milango na madirisha ya kisasa ili kujipatia ajira.

Na kama utatupatia mikopo hiyo ninakuhakikishia hasa katika jimbo la Koani tunaweza tukajenga maskuli yote hayo tunayotakiwa kutokana na hizo ambazo tunaweza kuzitengeneza sisi. Mhe. Waziri ningelipenda sana ahadi zako ambazo unazitoa kwa wajasiriamali uzitekeleze kwa wakati ili tuweze kuimarisha mambo ambayo yale unayoyapenda kuyaona kila wakati yanafanyika. Hasa sasa kwa vile tumejiimarisha kwenye ufugaji tungelipendelea katika jimbo langu tuongezee ng'ombe wa maziwa, ingawa umetupatia hivyo nakupa hongera sana katika jimbo langu wamepata ng'ombe wa kisasa lakini kwa kweli hawatoshi, tungelifurahi zaidi ungelitupatia ng'ombe wa kisasa tukahakikisha kwamba tunapata maziwa hasa kuwanywesha vijana wetu wa maskuli bila ya kununua sehemu nyengine. Sisi jimbo letu tungelihakikisha

kwamba tunaweza tukanywesha maziwa kama vile yalivyotokea ya mwaka, kuweza kuimarisha kunywesha vijana bila kununua sehemu nyengine.

Mhe. Spika, kwa kweli Wizara hii naipongeza sana kwa ujasiri wa shughuli zake hasa wakati ule wa matatizo madogo madogo kuweza kupata kazi ndogo ndogo za kufanya, ningelitoa nafasi zaidi kuwapatia vijana zana za kilimo ili kulima mboga kwa ajili ya kuweza kupeleka mahotelini, na hasa kwa vile mahoteli yetu yananunua sehemu nyingi kutoka nje vifaa vyake tungeliweza kujilimia sisi wenyewe katika majimbo, na mahoteli ambayo yamo katika majimbo yetu, tukalisha wenyewe na sio kutoka sehemu nyengine. Kila jimbo likapewa uwezo wa kulisha kitu kimoja, kama tunalipa mapapai tujue mapapai yote yanatoka Koani. Kama tuna machungwa, machungwa tunajua yanatoka koani, kama tunalima mboga, mboga zote mpaka mananasi tunajua yanatoka Machui.

Kwa hivyo ninahakikisha kwamba Jimbo la Koani lipewe kipaumbele kulipatia mikopo ili tuweze kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira bila ya kuhangaika kwenda mijini tukaweza kukaa katika sehemu zetu hasa tukaweza kuendeleza mambo ya michezo ambayo tunaipendelea sana. Kwa hivyo Mhe. Spika, nafasi hii ambayo iko wazi hivi sasa tunaomba Mhe. Waziri nafasi kubwa aipe Jimbo la Koani, hasa kwa vile ni watendaji wazuri sana kwa kila kitu kihakikishe kwamba kama kawaida yake Jimbo la Koani liko mbele, ahakikishe fedha nyingi mara hii, fedha nyingi zinapata mikopo kwenda jimbo la koani.

Ahsante sana kwa mchango wangu huu mdogo nisipoteze muda mwingi sana na wakati muda umemaliza sina zaidi, naipa hongera Wizara hii naunga mkono mimi na wananchi wangu wa jimbo la Koani asilimia mia. Ahsante sana.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, ahsante sana, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu *subhana llahu wataala* aliyetujaalia uhai, uzima tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Spika, naomba na mimi uniruhusu nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Hamad Masoud kwa kujiuzulu kwake, nasema hicho ni kitendo cha kishujaa na cha kiungwana. Lakini pia nichukue fursa hii kuweza kumpongeza Mhe. Rashid Seif kwa kushika nafasi hiyo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nianze sasa kumpongeza Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri kwa hotuba hii, ameiwasilisha kwa utaalamu sana kwa vile yeye ni muwezeshaji wa wananchi kiuchumi tena alikuwa mwalimu. Mhe. Spika, baada ya utangulizi wangu huo sasa nianze mchango wangu katika ukurasa wa 13 unaosema kupambana na ajira za watoto.

Mhe. Spika, watoto huwa wamezaliwa na wana mama zao, mama zao ndio sisi ambao tumesimama kwenye Baraza lako tukufu. Mhe. Spika, hapa petu Zanzibar kwa wakati huu ajira za watoto zimeendelea sana kuzaana, kiasi kwamba sasa zinatishia hali halisi ya ukuaji wao mwema. Mhe. Spika, hili haliwezi kuja tu kama bahati mbaya, ni dhahiri kwamba uchumi wananchi wa Zanzibar haukidhi haja, na hivyo basi hawamudu wazazi au wale ambao wanakaa na watoto hawa, hivyo basi hufanyika hayo ili kuweza kusaidia ama familia zao ama wazazi wao ili waweze kupata kujikimu kimaisha. Huu ni ukweli usiofichika.

Hivyo basi nimefurahi mno kuona kwamba Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, naomba hapa anieleze au atufahamishe yeye kwa sababu Wizara yake inahusika na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, ukiiangalia kwa kina Wizara hii kidogo inagusana sana na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto. Hivyo watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu wapo katika Wizara ile, lakini uwezeshaji kiuchumi ndie yeye. Je, Mhe. Waziri anashirikiana vipi na Wizara hiyo ili kuona kwamba wale vijana wanaoishi katika mazingira magumu unawawezesha wazazi wao, ili waweze kujinasua na maisha hayo na kuweza kuwafanya vijana wetu au watoto wetu wakakua katika mazingira yanayokubalika kabisa. Hali hii kiukweli wanawake ndio walezi wakuu, kutelekezwa baada ya talaka kuachiwa watoto ama wanaume kutojali, Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi naomba aina yake ya upendeleo kuona wanawake unawawezesha ili waweze kulea familia.

Mhe. Spika, sasa niende katika ukurasa wa 35 katika Idara ya Mikopo. Kabla ya mchango wangu niangalie kiambatanisho namba tano ambacho umepambanua katika mikoa yote ya Zanzibar ambayo umeipatia mikopo. Mikopo hiyo katika mazungumzo hapa umeonesha kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kusini, Kaskazini na Kusini Pemba.

Mhe. Spika, hapa nimeona kwamba wale ambao walipatiwa mikopo zaidi ni watu binafsi au mmoja mmoja. Nimeangalia kwenye vikundi hapa kwa Mkoa wa Kaskazini kwa vikundi hakuna hata kikundi kimoja ambacho kimepatiwa. Je, kuna sababu gani ambazo zimepelekea kwamba wasipatiwe hawa kwenye vikundi na badala yake wakapata mmoja mmoja je, Mhe. Spika, hapa hapapiti mambo ambayo si mazuri? Kwa sababu wananchi kujikusanya kwao kwa pamoja ni kuonesha nguvu zao, na serikali ndio wajibu wake wale waliojikusanya kuwapatia mikopo hii. Lakini kwa kiambatanisho chako hiki naona dhahiri kwamba waliopata mikopo hii wengi wao ni wale ambao wako binafsi.

Baada ya kusema hayo niseme tena mikopo hii Mhe. Waziri wakati inapotoka inaonesha dhahiri kwamba mikopo hii inakuwa midogo sana, lakini pia wale ambao wanapatiwa mikopo hii inakosa taaluma na ubunifu wa miradi endelevu na badala yake fedha hizo hutumika ovyo ovyo bila ya kuwa na utaratibu maalum, na hatimae kushindwa kurejesha mikopo hiyo na wengine pia kusita kupata fedha hizo.

Mhe. Spika, hili linajionesha dhahiri kwani kuna vikundi vingi katika mikopo ile AK na JK, ambazo fedha hizo hazikurejeshwa na wengi walithubutu kusema wakati sisi tukiwa katika kamati ya ustawi wa jamii na maendeleo ya wanawake na watoto kwamba fedha hizo ni za baba na haziwezi kurejeshwa. Hivyo basi ni dhahiri inaonesha kwamba hawakuwa na taaluma ya kuelewa kwamba nia na dhamira kubwa ya mikopo hiyo ni kuweza kujinasua wao kiuchumi, kuweza kujikidhi na badala yake waliona ni ruzuku imekuja tu watumie.

Hivyo basi naomba mikopo hii itolewe, lakini itolewe kwa utaratibu unaokubalika na utaratibu ambao unawaunganisha wazanzibari wote bila ya kujali bali kufuata utaratibu unaokubalika wa kutimiza masharti.

Mhe. Spika, sasa niende katika ukurasa wa 41 Idara ya Ushirika. Mhe. Spika, umeeleza sana kuhusu vikundi vya ushirika. Vikundi vilikuwa ni vingi sana vilivyoweza kusajiliwa, lakini uendelezaji wake sasa vimebaki vichache, hili Mhe. Spika, linatupa mashaka sana. Ni dhahiri

kwamba vikundi hivyo vilisajiliwa bila ya utaratibu au mpango madhubuti ulioonesha kwamba wanamudu au wanaweza, naweza nikasema hilo. Kwa sababu kama vikundi hivyo vilikuwa katika utaratibu na vilijengewa misingi imara nadhani vingekuwepo kwa sasa.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kwamba watendaji wako Mhe. Waziri katika utaratibu wa usajili wa vikundi vya ushirika basi hawajawa makini katika kuwaona wale ambao wameamua kujikusanya pamoja, ili kuweza kujikidhi au kuweza kujikusanya kwa kufanya shughuli yao kwa ajili ya kujiendeleza kimaisha. Kwa kuwa Wizara yako hii inahusika na hilo, ni ukweli usiofichika kwamba ni vikundi vingi katika wilaya yangu Kaskazini B Unguja, vikundi hivyo havijapatiwa usajili wake viko zaidi ya mwaka mmoja miezi minane miezi sita nenda rudi zimeongezeka, na hili ni kuwakatisha tamaa wale ambao wameamua kujikusanya kwa nia ile ile ya kujikidhi katika maisha yao kujiondolea umaskini.

Mhe. Spika, vikundi hivi ni vikundi vya uvuvi, ufugaji wa samaki, ukulima, lakini vikundi hivyo kwa masikitiko makubwa Mhe. Waziri hadi hivi nikisimama hapa vikundi hivyo havijapata usajili, sijui nadhani utakapokuja hapa na mimi utanielewesha yale masharti yanayotakiwa ni yepi ambayo hawakuyatekeleza. Kwa sababu wamejaza fomu, wamepewa fedha kwa ajili ya kiingilio kama ada lakini majibu yao ni nenda rudi mpaka wanakata tamaa hii si nzuri na haipendezi sana kwa wananchi ambao wanaishi katika misingi ya haki sawa kwa wote hapa, na kwa kweli serikali yetu ya umoja wa kitaifa lengo lake ni kuwaboreshea wananchi wetu hao au kuwatekelezea yale yote kwa nia moja bila kujali itikadi zao za kisiasa.

Hivyo basi Mhe.Waziri nakuomba sana hata wale ambao wamepata *registration* katika usajili basi ukiwaangalia kwa kina utakuta wapo katika mpango mmoja tu. Hii Mhe. Waziri nakuomba sana uwaangalie wote ni wazanzibari, wote ni vijana wetu, wote ni wanawake wa taifa hili, wana haki sawa, naomba kwa moyo mmoja uwaangalie kwa moyo wa imani ili tuweze kuliendeleza taifa letu kwa mapenzi na umoja wetu tuweze kufikia malengo.

Mhe. Spika, nikiendelea sasa niende kwenye Idara ya ajira katika ukurasa wa 56. Mhe. Spika, hapa umesema kwamba una nia ya kuongeza fursa zaidi za ajira kwa wazalendo, huu ndio msingi mkuu kwamba hao wanaohangaikiwa na kupiga kelele, na sisi kusimama hapa na mwenyewe Rais kusema ni Wazanzibari ndio ambao wanahitaji ajira hizi. Hili umelisema ni kweli, lakini Mhe. Waziri nami nichukue nafasi hii kukwambia ni ukweli usiojificha, nimefanya mwenyewe tafiti, nimekwenda katika mahoteli ikiwemo *Sea Cliff*, walioajiriwa ni wageni zaidi kuliko Wazanzibari hususan hata wale ambao kuna kazi za bustani ambao wapo karibu na zile shehia ambazo ardhi zao ndizo zinazotumika kwa ajili ya shughuli hizo basi wanakosa ajira.

Hili nakuomba sana Mhe. Waziri uliangalia na ulitizame kwa kina, na ipo haja ya kufanya utafiti maalum ukaweza kujua takwimu yote ya wafanyakazi wote wa mahotelini ukatueleza kwamba Wazanzibari halisi ni wangapi na wageni ni wangapi, kwani ni ukweli usiofichika katika kanda zetu za pwani wanaofanya kazi ni kutoka sehemu tofauti lakini ni wageni.

Mhe. Spika, jengine katika ajira hizi serikali imetangaza ongezeko la mishahara lakini wafanyakazi hao wa mahoteli basi waajiri wao wamekuwa na ridhaa zao katika kuwaongezea mishahara bila ya kujali utaratibu uliowekwa. Wanawapa mishahara hiyo kama watoto wao wanaokwenda skuli, wengine wamewaongezea shilingi elfu tano, wengine kumi na wengine

hawakupewa kabisa. Kwa hivyo basi, utaratibu huu nadhani si mzuri ipo haja kwa wizara yako kuliona hili na kuweza kuwafikiria vijana wetu hawa, ili waweze kufanya kazi katika misingi ya haki kabisa katika nchi yao.

Mhe. Spika, hivyo hivyo ni kusema kwamba wanaofanya kazi huko basi wote ama watakuwa wako bustanini au upishi, nafasi zilizobakia zote Mhe. Spika ni dhahiri wanazifanya wageni. Hili halileti picha nzuri ukizingatia kwamba sisi tumejenga Chuo cha Utalii na tunasomesha vijana wetu kuna nini? Kwa sababu chuo chetu kinatumia fedha na tunawasomesha vijana wetu ambao dhana ya utalii kwa wote inafaa iwaguse hawa vijana wetu ambao uwezo wao unaruhusu kuajiriwa katika sehemu hiyo, lakini matokeo yake unakuta wakati wa ajira hizo kuna mambo maalum, mambo ambayo wakati mwengine mila na utamaduni wetu unapokwenda kuomba kazi kule, ukipeleka barua yako hali ya kwamba umevaa baibui na mtandio ambapo ndio vazi la Kizanzibari unaonekana huwezi kazi.

Hayo yote Mhe. Spika, sikuyabuni ni mambo ambayo yapo, yanatendeka na yanafanyika wazi wazi. Hili Mhe. Waziri nakuomba sana hii dhana ya utalii kwa wote basi katika Wizara yako uiangalie kwa mapana makubwa wakati wa ajira.

Mhe. Spika, pia katika hilo ni kuona kwamba wanawake ambao wanafanya kazi katika hayo mahoteli ni kweli kabisa wanafanya kazi nyingi tena ngumu bila ya vipimo maalum, bila ya kuwa na posho, bila ya muda wa ziada, wao wako kazini masaa 24 yote, ikiachwa wakati mwengine hata kuzingatia katika ajira zao wale ambao wamepata ujauzito basi hawana hata muda wa kunyonyesha, ama wanapojifungua pengine ndio wanapoteza ajira zao baada tu ya kubeba ujauzito hawawezi kurudi tena kazini. Ile dhana ya utalii kwa wote wanakosa haki zao za msingi. Hili jambo linawagusa wote na ni haki za wote.

Lakini pia Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa utalii kwa sasa ndio ambao unalipatia taifa letu pato kwa asilimia 80, hebu tujiulize katika hii dhana ambayo umejipangia Mhe. Waziri ili uweze kuwakomboa hawa vijana wetu, umeandaa mpango gani madhubuti ambao utawagusa moja kwa moja, kuona kwamba wanazalisha na wanapata kutoa mazao yao ili kuona sasa wanaingia moja kwa moja kuweza kupata ajira hiyo pamoja na ile kuajiriwa mahotelini. Lakini sasa kuzalisha ili wakaweza kutumia mahoteli hayo kwa ajili ya kupeleka kile ambacho wanakizalisha.

Lakini pia wavuvi ambao wanavua na wao ni Wazanzibari katika utalii kwa wote wana haki. Je, kuna utaratibu au mpango gani uliowawekea ili kuona pale ambapo wamepata samaki ambao wanakubalika, ili kwenda kuona na kuweza kujua ni bei gani hasa mahsusi ambayo inapatikana na inalingana na soko lilivyo.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri muda uliobaki ni mchache mno kwa kumpa Mhe. Abdalla naye kutoa mchango wake, basi tusitishe shughuli zetu hadi kesho tarehe 25/07/2012 saa tatu za asubuhi.

(Saa 8:20 Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 25/07/2012 saa 3:00 asubuhi)